# Nipashe

Jumatano Februari 20, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0579846

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper


## Babu ateketea kwa moto aliowasha shambani kwake

UKURASA 3



Ukurasa 18

NJELU KASAKA MWANASIASA MKONGWE ALIYEIBUKA KIVINGINE

MAKALA: EAC itatue changamoto kabla ya kufikia ngazi ya shirikisho

Ukurasa 14

KIMATAIFA: Mabilioni ya Qatar yatuliza munkari Gaza, lakini

Ukurasa 15

siasa

JUMATANO FEBRUARI 20, 2019 Nipashe HABARI BORA NA KAMILIFU

Bila ya kuwa na demokrasia, mikutano ya AU haina tija

Na Gaudensia Mngumi

KIKAO cha kwanza cha Umoja wa Afrika (AU) kwa mwaka wa 2019 kimemalizika hivi karibuni jijini Addis Ababa, Ethiopia kikiwashirikisha wakuu wa nchi na viongozi wa serikali wa mataifa 55 ya bara hili yanayounda umoja huo.

Wakati wakuu wa Afrika wanafurahia kuliongoza bara hili linalopachikwa majina mengi yenye kejeli kama bara la giza 'dark continent', inavyoelekea mikutano ya AU huenda haina tija kwani hakuna utekelezaji wa maazimio, mikataba wala protokali inazojiwekea kujiletea maendeleo na kudumisha demokrasia.

Kwa mfano wapo wanaoendelea kuchezea katiba za mataifa yao kujiongezea muda wa kutawala, wakisababisha machafuko, chuki za kikabila na mauaji.

Mfano wa hivi karibuni ni wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambapo rais aliyekubali kuondoka madarakani Joseph Kabila, aliishi Ikulu tangu 2001. Mara kadhaa alikataa kung'atuka na safari

ENDELEA UK 16

Brexit inapofunikwa kwa uhasama wa Ufaransa, Italia kuhatarisha EU

Ukurasa 18

Rais Abdel Fattah el Sisi wa Misri, ambaye ni mwenyekiti mpya wa AU.

UKURASA 13



# Kifungo miaka 45 kwa mauaji tembo 430

UKURASA 2

TEMBO 430 WALIOUAWA WANA THAMANI YA SH. BILIONI 14

**TEMBO 430**

MENO YA TEMBO 860 WALIYOKUTWA NAYO YANA THAMANI YA DOLA ZA MAREKANI MILIONI 6.45

**MENO 860**






# Chadema yamjia juu Polepole



UKURASA 2

HABARI NEC YATOA MSIMAMO DAFTARI WAPIGAKURA UK. 3 | MAONI, KATUNI UK.6

# Kifungo miaka 45 mauaji tembo 430

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, imewahukumu raia wa China, Yang Feng Glan, maarufu Malkia wa Meno ya Tembo, na wenzake wawili kwenda jela miaka 45 au kulipa faini ya Sh. bilioni 27.864 baada ya kukutwa na hatia ya makosa matatu ya uhujumu uchumi.

Washtakiwa hao wamekutwa na hatia katika makosa yote matatu ya kuratibu makundi ya ujangili, kukutwa na meno ya tembo 860 (tembo 430) yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 6.45 (Sh. bilioni 13.932).

Hukumu hiyo ilitolewa jana na mahakama hiyo iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, aliyesikiliza kesi hiyo.

Hakimu huyo alisema shamba na nyumba vinavyomilikiwa na mshtakiwa Glan vinataifishwa na serikali.

Alisema mahakama yake baada ya kupitia ushahidi wa mashahidi 11 wa Jamhuri, bila kucha shaka, iliwatia hatiani washtakiwa.

Alisema ni jukumu la Jamhuri kuthibitisha mashtaka mahakamani na kwamba walijenga kesi yao na kuonekana kweli washtakiwa walihujumu uchumi.

Ushahidi unaeleza kuwa, mshtakiwa wa pili, Salvius Matembo, alikuwa anamiliki gari aina ya Noah na Glan alimiliki 'pikapu' ambazo walizitumia kubebea meno ya tembo.

"Mshtakiwa Glan alikuwa anamiliki ghala, ndani yake alipanda maua, lakini wakati mwingine aliyang'oa na kufukia meno ya tembo na baadaye waliyatoa kwenda kuyauza," Hakimu Shaidi alisema.

Akifafanua ushahidi huo, hakimu huyo alisema mlinzi wa ghala hilo alikabidhiwa kitabu maalum cha kuandika kumbukumbu za meno anayoyapokea, uzito wake na yaliyoondolewa kwenye eneo hilo.

"Mshtakiwa Glan alitumia malori mawili ya taasisi za serikali kusafirisha meno hayo kwenda bandarini, hii ni dharau kubwa sana kwa nchi yetu, nyara zetu uchukue na magari ya serikali utumie, si ulipitiliza mipaka," Hakimu Shaidi alisema.

Aliendelea kusoma hukumu hiyo akieleza kuwa, washtakiwa Matembo na Glan walikuwa wanafahamiana na kwamba kati ya Septemba 3 na 8, 2010, Glan alimhamishia Matembo Sh. milioni 22 kwenye akaunti yake.

Alisema katika utetezi wao, washtakiwa walikana kufahamiana, lakini walishindwa kuzungumzia sababu za kuhamishiana mamilioni ya shilingi kwenye akaunti zao.

Alisema mahakama hiyo ilihamishia shughuli zake Muheza mkoani Tanga kwenye shamba na nyumba ya Glan.

Alisema shamba limelimwa pilipili manga, lakini ilionekana mshtakiwa alitumia kufukia meno ya tembo na baadaye kuyasafirisha.

"Mahakama hii inawahukumu washtakiwa kwenda jela miaka 15 kwa kosa la kwanza, 15 kosa la pili kwa kila mshtakiwa na kosa la tatu kulipa faini mara mbili ya fedha wanazodaiwa kuhujumu Sh. bilioni 13.932 (Sh. bilioni 27.864) au kwenda jela miaka miwili," alisema hakimu wakati akisoma adhabu.

Kabla ya kutolewa adhabu hiyo, mahakama ilimwalika Ofisa Uhifadhi Wanyamapori, Idara ya Wanyamapori wa Wizara ya Maliasili na Utalii, Kizan Baraga (37), kuisaidia kujua athari na hasara iliyotokana na uhujumu uchumi wa

INAENDELEA UK 8

## Serikali yapewa siku 45 utetezi matokeo ya urais

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAHAKAMA ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu (AfCPHR), imetoa siku 45 kwa Serikali ya Tanzania, ikiitaka itoe utetezi kuhusu maombi yaliyofunguliwa mahakamani hapo kutaka matokeo ya uchaguzi ya Rais yapingwe mahakamani.

Kwa mujibu wa barua ya Msajili wa AfCPHR, Dk. Robert Eno, amri hiyo inafuatia ombi namba 018/2018 lililofunguliwa mahakamani hapo na mlalamikaji Jebra Kambole dhidi ya mlalamikiwa ambaye ni Serikali ya Tanzania.

Katika barua yake ya Februari 14, mwaka huu, yenye kumbukumbu namba AfCHPR/Reg./APPL/018/2018/008, Msajili Dk. Eno, amemtaka malalamikiwa kutoa utetezi wake ndani ya siku 45.

"Mlalamikiwa anajulishwa na mahakama hii, kwa mujibu wa maslahi ya haki, kuendelea na kutoa hukumu kwa mujibu wa maombi yaliyowasilishwa iwapo haitapokea utetezi wowote ndani ya siku 45 baada ya kupokea barua hii.

"Msajili anakutaarifu (mlalamikiwa) kwamba mlalamikaji ameomba kutolewa uamuzi kuhusu kushindwa kwako (mlalamikiwa), kutoa utetezi wa shauri alilofungua kwa mujibu wa kanuni 55(1) ya Kanuni za Mahakama hiyo.

"Pale ambao upande mmoja unashindwa kuonekana mahakamani au unashindwa kutetea kesi yake, mahakama inaweza kwa kuzingatia maombi yaliyowasilishwa na upande mwingine, kupitisha hukumu/uamuzi baada ya kujiridhisha kwamba upande ulioshindwa kufanya hivyo, ulipelekewa hati ya maombi ya shauri husika pamoja na nyaraka zake zote kwa ajili ya mwenendo wa shauri hilo," ilisema sehemu ya barua hiyo.



Mwendesha guta akiwa ameisheheni mzigo wa magodoro, katika Barabara ya Chang'ombe, eneo la Veta, jijini Dar es Salaam jana, na kumfanya ashindwe kuona nyuma kitendo ambacho ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

## Chadema yamjia juu Polepole

**Na Romana Mallya**

SIKU moja baada ya Katibu wa Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Humphrey Polepole, kudai hatua ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kufanya mikutano ya hadhara ni ukorofi na uvunjifu wa sheria, uongozi wa chama hicho cha upinzani umemjibu, ukidai kauli yake hiyo ni ya watu wasiopenda kufikiri.

Wiki iliyopita, Chadema kupitia Katibu Mkuu wake, Dk. Vicent Mashinji, ilitangaza kuwa inatarajia kuanza mikutano ya hadhara baada ya kukamilisha mambo yake ya ndani.

Chama hicho kilieleza kuwa kinatambua kuwapo kwa zuio la serikali kufanya maandamano na mikutano ya siasa nchini, lakini kitaendesha mikutano hiyo kwa kuwa iko kisheria na kwamba CCM wamekuwa wakiifanya bila kuchukuliwa hatua.

Baada ya Chadema kutangaza uamuzi huo huku wakiitaja CCM kukiuka agizo la Rais John Magufuli la Juni 23, 2016, ya kuzuia mikutano ya siasa na maandamano, Polepole alizungumza na Nipashe na kudai chama hicho cha upinzani kutangaza kufanya mikutano nchi nzima, ni ukorofi na uvunjifu wa sheria.

Akijibu kauli hiyo ya Polepole jana, Dk. Mashinji, alidai kauli ya Polepole ni ya mtu mvivu ambaye anapinga kitu bila ya kuwa na hoja.

"Hiyo ni kauli ya watu wavivu ambao hawapendi kuzihangaisha akili zao kupinga hoja zinazotolewa," Dk. Mashinji alisema, "kufanya mikutano ni uvunjifu wa sheria? Hebu atuambie ni sheria au kanuni ipi anayozungumzia hapo ambayo inakataza mikutano.

"Hawa ndiyo vijana wa CCM ambao wamepewa nafasi bila kuandaliwa, hawajui wazungumze nini. Sisi tutaendelea na programu zetu za mikutano kama tulivyoeleza awali.

"Polisi wetu hawana shida, tunawaandikia barua kuwataarifu kuhusu mikutano yetu, wanakuja wanatulinda, hawana shida na sisi. Sasa huyu Polepole anazungumzia sheria ipi au kuna kanuni ipi inayozuia mikutano?"

Juni 23, 2016, Rais John Magufuli alitangaza kupiga marufuku vyama kufanya mikutano ya siasa mpaka baada ya miaka mitano ili wananchi wahoji wanasiasa kama wametekeleza yale waliyoyaahidi katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Alitoa kauli hiyo Ikulu Dar es Salaam baada ya kukabidhiwa ripoti ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na aliyekuwa Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Jaji mstaafu Damian Lubuva.

"Niwaombe wanasiasa wenzangu, wafanye siasa za ushindani kwa nguvu zote baada ya miaka mitano ili wananchi watuhoji tuliyoyaahidi kama tumeyatekeleza au hatujayetekeleza.

"Kila nchi hata zile zilizobobea kwenye demokrasia, unapokwisha uchaguzi unakuwa ni wakati wa kazi. Haiwezekani mkawa kila siku ni siasa, watu watalima saa ngapi?

Kila siku ni siasa, ni vyema tukatimiza wajibu wetu tuliopewa na wananchi na watatupima kwenye hilo.

"Ni matumaini yangu kuwa Watanzania tunaowaongoza wanataka maendeleo. Iwe kwa bahati nzuri au mbaya, serikali inayoongoza ni ya Chama Cha Mapinduzi.

"Yako tuliyoyaahidi kuyatekeleza kwa wananchi katika kipindi cha miaka mitano, nisingependa kuona mtu yeyote ananichelewesha kutekeleza hayo niliyoahidi kwa kipindi cha miaka mitano," alisema.

Alisema ushindani ambao unatakiwa ufanywe kwa nguvu ni kwa wale wawakilishi waliopewa mamlaka na wananchi kupeleka hoja zao kwenye maeneo yao.

"Kama ni madiwani, wakapeleke hoja kwa nguvu zote kwenye maeneo yao, kama ni wabunge wakazungumze kwa nguvu sana bungeni, lakini hata kuziba midomo nayo ni demokrasia, hiyo ni demokrasia ya mwelekeo wa aina yake," Rais Magufuli alisema.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P 2888,
40470 DODOMA

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya **Ijumaa tarehe 22/02/2019** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yake yenye vipimo vikubwa kutoka Bandari ya **Mtwara** kuelekea **Mbeya**, magari hayo yana namba za usajili:

   **T221BYM/T887DJB**
   **T636DFA/T837DJB**
   **T133CCP/T574BZB**
   **T296CZS/T900BAZ**

2. Magari hayo yana vipimo vifuatavyo:
   Urefu - mita 27.0
   Upana - mita 5.50
   Kimo - mita 6.40

3. Njia itakayotumika: **Mtwara hadi Mbeya** Kupitia **Makambako,**
   Magari yatasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 06:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

**Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.**

215065902

## HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua ujenzi wa ofisi ya Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko mkoani Kigoma, baada ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi huo, jana. **PICHA: OWM**

# Babu ateketea kwa moto aliowasha shambani kwake

**Na Steven William,** MUHEZA

MKAZI wa kijiji cha Kilongo, Muheza mkoani Tanga, Saidi Sekizenge (72), amefariki dunia kwa kuteketea kwa moto akiwa shambani kwake.

Tukio hilo lilitokea juzi katika kijiji hicho ambako Sekizenge alikuwa anaishi na familia yake.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tanga, Edward Bukombe, alisema mzee huyo alifariki dunia kutokana na kuungua na kuteketea wakati akichoma moto majani yaliyokuwa yamekauka shambani mwake.

Alisema wakati akichoma majani hayo shambani, ghafla moto ulimzidi nguvu kutokana na upepo mkali, hivyo kuhamia katika mashamba ya watu ambayo wamepakana na shamba lake na moto

INAENDELEA UK 8

# NEC yatoa msimamo daftari la wapigakura

**Na Romana Mallya**

WAKATI wadau wakihoji ukimya wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) katika kuboresha daftari la kudumu la wapigakura, uongozi wa tume hiyo umesema muda wa uboreshaji wa daftari hilo bado haujafika.

Wadau wa siasa nchini wamekuwa wakipendekeza daftari hilo liboreshwe kwa mujibu wa sheria na litumike katika uchaguzi wa serikali za mitaa unaotarajiwa kufanyika Agosti mwaka huu.

Hata hivyo, Mkurugenzi wa NEC, Dk. Athumani Kihamia, aliiambia Nipashe jana kuwa hawajapokea maombi rasmi ya kutumika kwa daftari hilo katika uchaguzi huo na muda wa kuliboresha bado haujafika kwa mujibu wa kalenda yao.

"Sisi tuna kalenda yetu ya tume. Kwa hiyo, kila jambo lipo kwenye kalenda, muda wa uboreshaji wa daftari la mpigakura ukifika, tutawatangazia maana jambo hili siyo siri, kwa sasa muda haujafika," alisema.

Alipoulizwa kuhusu ombi la Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) na wadau kwamba daftari hilo litumike kwenye uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka huu, Dk. Kihamia alisema hawajapokea ombi hilo.

"Wakati Chadema wanazungumza, kulikuwa na watu wa tume? Si walikuwa wanaongea na waandishi wa habari? Siwezi kujibu kwa sababu hatukuwapo, wao waliwaambia waandishi wa habari, hatujalipokea ombi hilo," alisema.

Januari 31, Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge, Kazi na Ajira, Anthony Mavunde, aliliambia Bunge kuwa, serikali inakisia kuandikisha wapigakura wapya milioni nne kabla ya Uchaguzi Mkuu wa mwakani.

Waziri huyo alikuwa anajibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Cecilia Pareso (Chadema), ambaye alitaka kujua ni jinsi serikali itavyotumia kipindi kifupi kilichobaki kutoa haki kwa Watanzania wenye sifa kuandikishwa ili watumie haki yao kupiga kura mwakani.

Katika swali lake la msingi, mbunge huyo alihoji ni lini serikali itaanza mchakato wa kuboresha daftari hilo.

Wakati NEC ikieleza kuwa muda wa kuboresha daftari la kudumu la wapigakura haujafika, katika majibu yake kwa Pareso bungeni Januari 31, Mavunde alisema mchakato wa kuboresha daftari hilo ulianza Agosti mwaka jana kwa kuhuisha kanzidata ya daftari la kudumu la

INAENDELEA UK 8


## MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD

DEBT COLLECTOR AUCTIONEER
P.O. BOX 75087, DAR ES SALAAM, TANZANIA
Mobile: + 255 784 622 019, +255 715 622 019, +255 765 999 000
Tel: +255 2184653 Fax +255 0222181477
Web: www.masetodebtcollectors.co.tz
Email: masetodebtcollectors@yahoo.com or shabani.chuki@yahoo.com

20th February 2019

## NOTISI/TANGAZO LA MNADA

Kwa idhini tuliyopewa na **AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, MASETO AUCTIONEER & DEBT COLLECTOR LTD** tunatangaza kuuza dhamana za wadaiwa sugu walioshindwa kulipa mikopo yao katika Benki tajwa hapo juu kama watashindwa kulipa madeni yao ndani ya muda huu. Minada hii itafanyika kama inavyoonesha hapa chini;

| S/N | JINA LA MTEJA | UMILIKI WA DHAMANA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIKO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|---|
| 001 | ATHUMANI SAID BANDIKO | ATHUMANI SAID BANDIKO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA VIKUNAI WILAYA YA KIGAMBONI | 06/03/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 002 | KHADIJA HUSSEIN JAFARAH | JOSEPH JOACHIM MKWAVI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO, ILIYOKO MTA WA MBEZI MTONI (GOBA)- WILAYA YA KINONDONI | 08/03/2019 SAA 11:00 ASUBUHI |
| 003 | SAKINA JUMA HUSSEN | MOHAMED SALUM SAID | GARI SUZUKI CARRY T 984 DCB IKO TABATA CHANG'OMBE KITA'S PUB | 11/03/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 004 | ZITA FIDELIS MATEMBO | ZITA FIDELIS MATEMBO | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO TABATA KISUKURU MIGOMBANI – ILALA | 11/03/2019 SAA 06:00 MCHANA |
| 005 | ERASTO ALEX CHOGO | ERASTO ALEX CHOGO | NYUMBA YENYE YA MAUZIANO ILIYOKO BONYOKWA – ILALA | 11/03/2019 SAA 09:00 MCHANA |
| 006 | ABBAS HAMAD SHAGILE | ABBAS HAMAD SHAGILE | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MBONDOLE KWA MHAYA – ILALA | 13/03/0179 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 007 | FRANCIS DIWAN HUSSEN | FRANCIS DIWAN HUSSEN | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO ZINGIZIWA CHANIKA – ILALA | 13/03/2019 SAA 08:00 MCHANA |
| 008 | OMARY MOHAMED TWAHA | FOCUSI LUCA MUSHI | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO KIBAMBA CCM – UBUNGO | 15/03/2019 SAA 04:00 ASUBUHI |
| 009 | JORAM LAZARO SEMBWELA | JORAM LAZARO SEMBWELA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO KIBAHA MAILIMOJA – WILAYA YAKIBAHA | 15/03/2019 SAA 08:00 MCHANA |
| 010 | AUGUSTINO JOHN MASENYA | AUGUSTINO JOHN MASENYA | NYUMBA YENYE HATI YA MAUZIANO ILIYOKO MTAA WA BOMBAMBILI GONGO LA MBOTO – WILAYA YA ILALA | 18/03/2019 SAA 05:00 ASUBUHI |
| 011 | YASMIN SULTAN AWADH | YASMIN SULTAN AWADH | BOMA LA NYUMBA LENYE HATI YA MAUZIANO LILILOKO MTAA WA SARA KATA YA SOMANGILA-WILAYA YA KIGAMBONI | 20/03/2019 SAA 05:00 ASUBUHI |
| 012 | ABDALLAH GULAM MOHAMED | MARY ENEA ELIAMAN | NYUMBA YENYE LESENI YA MAKAZI LIYOKO KIBAHA MAILIMOJA-WILAYA YA TEMEKE | 22/03/2019 SAA 05:00 SUBUHI |

**Masharti ya mnada**

1. **Dhamana itauzwa kama ilivyo.**
2. **Mnunuzi atatakiwa kulipa siku hiyo hiyo ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.**
3. **Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14) kukamilisha malipo yote, ukishindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25% na mnada utarudiwa tena.**
4. **Gharama za kuona, kukaguwa, kuhamisha umiliki, na zingine zinazoambatana na hili ni juu ya mnunuzi.**

215071102

**KWA TAARIFA ZAID WASILIANA NA:**
**AKIBA COMMERCIAL BANK PLC,**
**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**P.O BOX 669,**
**DAR ES SALAAM**
**Tel+255 02221183403**

**AU**

**Maseto Auctioneer,**
**MKURUGENZI MTENDAJI,**
**P.O BOX 75087,**
**DAR ES SALAAM**
**+255 765 999 000 AU +255 787 288 442 AU +255 762 260 787**



FSSP

## CONSULTANCY POSITION

## PUBLIC FINANCIAL MANAGEMENT TECHNICAL SPECIALIST

## TO SUPPORT GLOBAL AFFAIRS CANADA

PricewaterhouseCoopers Limited (PwC) invites eligible candidates to indicate their interest to provide consultancy services as **Public Financial Management (PFM) Technical Specialist** to support Global Affairs Canada under the Field Support Services Project (FSSP) Tanzania.

The Public Financial Management Technical Specialist will provide PFM-related strategic advice and technical support related to Canada's policies, strategies and programming in Tanzania.

**Candidates will be evaluated based on the following key qualifications and experience:**

i. Master's degree in a relevant field such as public administration (including accounting or auditing), economics, business administration, accounting, development economics, macroeconomics or public finance
ii. Minimum of five (5) years of experience in public policy, economic policy, or public financial management, at least three (3) years of which should have been gained in Tanzania
iii. Minimum of five (5) years of experience in international development policy and programs, preferably in a bilateral or multilateral development institution
iv. Minimum of five (5) years of experience with public sector accounting, financial management, and budget reviews
v. Knowledge of public sector policy priorities and processes in Tanzania, including planning, management and budgeting of public sector resources

In addition to the key qualifications above, the incumbent should also demonstrate the following skills and competencies:

- Advanced professional proficiency in English;
- General professional proficiency in Kiswahili;

Training or experience in gender-responsive, gender-based, and/or gender-sensitive public financial management would be a strong asset.

Interested candidates should obtain a detailed description of these services by sending request email to procurement@fssptz.org specifying in the requests as follows: "**Consultancy position for Public Financial Management Technical Specialist.**"

Requests for further information will be received up to three working days prior to the **last submission date, 8 March, 2019.**

**Any request received later than that may not be responded to.**

**FSSP Manager**

215070802

# Majaliwa asimamisha kigogo kwa tuhuma za ubadhirifu

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemsimamisha kazi Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo mkoani Kigoma, Thomas Chogolo, ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili za ubadhirifu wa makusanyo ya mapato ya halmashauri hiyo.

Pia, Waziri Mkuu amewataka watendaji wa halmashauri huyo kumaliza haraka migogoro yao ya kiutendaji kabla ya serikali haijawachukulia hatua kwa kuwa wanachokifanya ni kinyume cha maelekezo yake. Waziri Mkuu alichukua hatua hiyo jana wakati akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kibondo, akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Kigoma.

"Katika serikali hii suala la ukusanyaji wa mapato ni jambo nyeti na limepewa kipaumbele, hivyo ni lazima fedha inayokusanywa itumike kama ilivyokusudiwa ikiwa ni pamoja na uboreshaji wa miradi ya maendeleo kwa wananchi."

Waziri Mkuu alisema wananchi wa halmashauri hiyo wanalipa kodi kupitia kwa watendaji wa kata katika maeneo yao, lakini mweka hazina haingizi kwenye mfumo wa serikali, jambo ambalo alisema halivumiliki.

Alisema mbali na fedha za makusanyo ya kodi, pia matumizi ya fedha zinazopelekwa na serikali katika halmashauri hiyo nayo hayaridhishi, huku akitolea mfano wa fedha za sekta ya afya ambapo zaidi ya shilingi bilioni mbili zimepelekwa, lakini hakuna kitu.

Waziri Mkuu amesema uaminifu na uadilifu ni jambo ambalo linapaswa kupewa kipaumbele na watumishi wa umma, hivyo amewataka watumishi hao wasijiingize kwenye mambo ambayo hayana tija katika utumishi wao.

Majaliwa alisema serikali imewapa dhamana watumishi hao kwa ajili ya kuwatumikia wananchi na si kutanguliza maslahi yao binafsi, hivyo kuwataka wajirekebishe kwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

"Serikali haitawapa nafasi ya kuendeleza migogoro yenu kila mmoja lazima atambue majukumu yake na kuyatekeleza. Serikali haihitaji mtumishi mvivu, asiyekuwa mwadilifu na wala anayejihusisha na vitendo vya rushwa."

**AFUNGA SOKO KISA WAKIMBIZI**

Wakati huo huo, Majaliwa amefunga soko la wakimbizi na wananchi lililoanzishwa nje ya kambi ya Nduta iliyoko wilayani Kibondo mkoani Kigoma.

Hatua hiyo imechukuliwa baada ya soko hilo kubainika kuwa chanzo cha wakimbizi kutoka nje ya kambi kiholela na kushiriki katika kufanya matukio ya kihalifu.

Waziri Mkuu alitangaza uamuzi huo jana wakati akizungumza na watumishi wa umma katika Halmashauri ya Kibondo.

"Vitendo vya uhalifu wilayani Kibondo vikiwamo vya utekaji wa watoto vimeongezeka na kusababisha hofu na taharuki miongoni mwa wananchi."

Waziri Mkuu alisema ni vema halmashauri hiyo ikaandaa utaratibu wa kutoa vibali vitakavyowaruhusu Watanzania kupeleka bidhaa ndani ya kambi hivyo.

Kadhalika, aliwataka wananchi waliopewa dhamana ya kufanya kazi kwenye kambi za wakimbizi wawe waadilifu na wasimamie sheria.

"Nafahamu tunao watendaji wetu ambao wapo kambini kusimamia shughuli mbalimbali za wakimbizi, tekelezeni wajibu wenu ipasavyo na si vinginevyo."

Baada ya kuzungumza na watumishi wa umma wa Halmashauri ya Kibondo, Waziri Mkuu alikwenda wilayani Kakonko na kukagua mradi wa maji Muhange.

Pia Waziri Mkuu ameweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa makao makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko unaotarajiwa kugharimu Sh. bilioni 4.5.



Mkurugenzi wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi (wa pili kulia), akikagua chumba cha maabara ya Shule ya Sekondari Dodoma, iliyoko jijini humo, jana. Kulia ni Mhandisi wa Ujenzi wa Jiji hilo, Ludigija Ndatwa. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

## IGP Sirro atoa kauli nzito mauaji ya watoto Simiyu

**Na Happy Severine,** BUSEGA

MKUU wa Jeshi la Polisi nchini, Simon Sirro, amesema jeshi lake halitawafumbia macho wale wote waliohusika na mauaji ya watoto kata ya Lamadi Wilaya ya Busega mkoani Simiyu, na kwamba hatua kali dhidi yao zitachukuliwa.

Kamanda Sirro alisema hayo jana wakati wa mkutano wake wa hadhara wa wananchi wa kata hiyo.

Sirro alisema hawatakaa kimya na kuwafumbia macho wale wote watakaobainika kuhusika na mauaji hayo, hivyo watambue wazi serikali haijalala na hatua kali dhidi yao zitachukuliwa.

Aliongeza kuwa mauaji mengi yanayotokea yanahusishwa na mambo ya kishirikina na wana ndugu au familia ndio wamekuwa wakishiriki katika matukio hayo.

IGP Sirro aliwahakikishia viongozi wa mkoa wa Simiyu kumaliza matukio ya mauaji yanayoendelea katika Kata ya Lamadi, huku akibainisha kuwa yanaonekana kusababishwa na imani potofu za kishirikina kutoka kwa wananchi.

Sirro alisema ameongeza nguvu kutoka makao makuu ya jeshi ili kushughulikia suala la matukio ya Lamadi na kuwa mauaji hayo yatakomeshwa.

Alibainisha kuwa njia pekee ya kukomesha vitendo vya mauaji mkoani Simiyu ni elimu zaidi itolewe kwa wananchi ili kuondokana na imani za kishirikina.

Aliwataka wananchi na viongozi wa mkoa kushirikiana na jeshi hilo, na kusema anaamini kuwa ushirikiano watakaotoa kwa polisi utasaidia wahusika wote kukamatwa.

"Kuna watu bado wanaamini kupata samaki wengi mpaka watumie hizo njia za kishirikina, mimi bado naikumbuka Lamadi hii tabia ilikuwapo zamani, na wahusika wakuu walikuwa wazazi wa watoto," alisema IGP Sirro.

"Sasa nimeagiza, watafutwe hata hao ambao walihusika katika matukio kama haya uko zamani, tuone kesi zao zilienda vipi na tujue wapi tunaanzia, lakini elimu inahitajika zaidi kwa wananchi," alisema IGP Sirro.

# Kanyasu awapa ahueni wadau misitu

**Na Lusungu Helela,** MOSHI

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, ameagiza Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuwaruhusu wadau wa misitu nchini wenye viwanda vya mbao waendelee kutumia mashine za zamani za kuchakata mbao walizo nazo, huku wakijipanga kununua za kisasa kulingana na mabadiliko ya teknolojia.

Hatua hiyo imechukuliwa kutokana na zuio la wamiliki wa viwanda hivyo kutumia mashine za zamani za kuchakata magogo ambazo zimekuwa zikizalisha taka nyingi, hivyo kusababisha upotevu mkubwa wa mbao.

Kanyasu alisema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wadau wa misitu na wenye viwanda vya mbao katika shamba la miti la Longuza, Rombo mkoani Kilimanjaro.

Mwenyekiti wa Wamiliki wa Viwanda vya Mbao kwa mikoa ya Kaskazini, Ibrahim Shoo, alilalamikia zuio hilo huku akimwomba Naibu Waziri awape muda wa kutosha kwa ajili ya kujipanga kununua mashine za kisasa.

Kutokana na malalamiko hayo, Kanyasu aliiagiza TFS iendelee kutoa leseni na mgawo wa vitalu vya miti kwa wamiliki wa viwanda wenye mashine za zamani, ili kutoa fursa kwao kujipanga kununua mashine ambazo zinazalisha taka chache wakati wa uchakataji wa mbao.

Hata hivyo, Kanyasu aliwaeleza wadau hao kuwa uamuzi wa kutumia mashine za kisasa za kupunguza hasara ya upotevu mkubwa wa mbao bado uko pale pale.

Aidha, Kanyasu alisema uamuzi wakuwataka wamiliki wa viwanda vya mbao kutumia mashine mpya unakwenda sambamba na zuio lililokuwa limetolewa awali la kuzuia kutumia misumeno ya Dingdong ambayo nayo ilikuwa ikisababisha upotevu mkubwa wa mbao.

Pia aliiagiza TFS itoe mikataba ya miaka miwili kwa wamiliki wa viwanda vya mbao hali itakayowasaidia kutoa uhakika kwa wamiliki hao kukopesheka katika taasisi za fedha.

Alisema benki nyingi zimekuwa zikitoa mkopo wa miezi 12 hali itakayowasaidia wafanyabiashara hao kuwa na uwezo wa kurudisha fedha walizokuwa wamekopa endapo watapewa mikataba ya miaka miwili.

Katika hatua nyingine, Kanyasu aliwataka wadau wa misitu nchini hasa wenye viwanda vya mbao wafungue mashamba makubwa ya miti ili badaye wavune miti katika mashamba yao hali itakayosaidia kupunguza utegemezi kutoka kwenye mashamba ya miti ya serikali.

Amesema nchi kama Finland uchumi wake unategemea kwa kiasi kikubwa misitu na wamiliki wakubwa wa mashamba ya miti ni wadau wa misitu wa nchi hiyo.

HABARI KITAIFA

# Sababu Lugola kumtumbua OCS

**Na Mwandishi Maalum,** KARATU

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amemwagiza Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa Arusha kumwondoa Mkuu wa Kituo cha Polisi Mang'ola wilayani Karatu kwa kushindwa kusimamia misingi ya kazi.

Lugola amesema amepokea malalamiko mengi kutoka vyanzo mbalimbali ikiwamo kupitia mkutano wa hadhara uliofanyika mjini Karatu.

Akizungumza na mamia ya wananchi wa Mji wa Karatu katika mkutano wa hadhara uliofanyika mjini humo jana, Lugola alisema malalamiko yaliyotolewa na wananchi wilayani humo yanaonyesha mkuu huyo wa kituo ameshindwa kusimamia nidhamu.

"RPC nakuagiza umwondoe haraka iwezekanavyo mkuu huyu wa kituo hiki, mlete mwingine atakayejenga nidhamu upya ya askari katika kuwahudumia wananchi wa Mang'ola, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko mengi yanayotolewa na wananchi juu ya askari kushindwa kusimamia misingi ya kazi yao," alisema Lugola.

Pia Lugola alimwelekeza Mkuu wa Wilaya ya Karatu aongozane na kamati yake ya ulinzi na usalama kwenda katika Gereza la Mang'ola wilayani humo, kuwaonyesha uongozi wa gereza hilo, eneo la kuchimba mtaro wa maji ili waachane na mtaro wanaoutumia wananchi ambao umekuwa ukileta mgogoro katika eneo hilo.

Pia Waziri Lugola alimwagiza Mkuu wa Magereza Mkoa wa Arusha, kuwaondoa askari watatu waliolalamikiwa kuwazuia wananchi kutumia maji na kuwapiga wananchi.

Lugola alisema mgogoro huo umeleta matatizo, hivyo alimtaka mkuu huyo wa Magereza kutuliza hali hiyo ili wananchi waweze kuyatumia maji hayo ambayo wanazuiwa na askari magereza.



"Nakuagiza kuzingatia yote niliyoyasema katika kikao yaliyohusiana na kumaliza mgogoro huo kati ya askari na wananchi wanaodaiwa kupigwa na endapo watashindwa kutekeleza maagizo hayo, nitaagiza hatua za kinidhamu zichukuliwe dhidi yao," alisema Lugola.

Wakizungumza katika mkutano huo wa hadhara, baadhi ya wananchi walitoa malalamiko jinsi askari magereza walivyowanyanyasa, kuwapiga, kuwatisha kwa kutumia bunduki, huku wakiwataja kwa majina yao.

"Askari wanakuja na bunduki wanakutishia mdomoni na kukusukuma wakidai hatutambuliki, lakini tulipeleka malalamiko yetu ngazi husika ikiwamo kwa katibu tarafa ambaye alionya mara nyingi bila mafanikio," alisema Jackson Qorou.



Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Benki ya Exim, Jaffari Matundu, akifafanua jambo kwa wateja wa benki hiyo, katika hafla iliyofanyika jijini Arusha hivi karibuni. **PICHA: EXIM**

# Mtaala wa pamoja vyuo afya waanzishwa

**Na Mary Geofrey**

KATIKA kuboresha sekta ya afya nchini, vyuo vikuu vitatu vinavyotoa mafunzo ya afya nchini, vimeungana kuanzisha mtaala utakaowezesha vyuo vyote kuzalisha wahitimu wenye viwango sawa.

Hatua hiyo imefikiwa kutokana na kutokuwapo kwa mwongozo maalum wa taaluma ya afya kutoka Tume ya Vyuo Vikuu (TCU), hali inayosababisha kila chuo kuwa na mtaala wake unaozalisha wahitimu wenye viwango tofauti.

Mkuu wa Mradi huo, Prof. Ephata Kaaya, aliyaeleza hayo wakati wa uzinduzi uliofanyika jijini Dar es Salaam jana na kutaja vyuo vilivyoanzisha ni Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi (Muhas),

INAENDELEA UK. 8

# Mawaziri watuliza wananchi kisa ardhi

**Na Happy Severine,** MEATU

TIMU ya mawaziri wanane wanaotembelea maeneo ya migogoro ya ardhi nchini imewataka wananchi kuwa watulivu wakati serikali ikiendelea kutatua migogoro hiyo inayowakabili katika maeneo yao.

Akizungumza na wananchi wa Kata ya Mwandoya wilayani Meatu mkoani Simiyu, Mwenyekiti wa timu hiyo, William Lukuvi ambaye ni Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, alisema Rais John Magufuli ameunda timu hiyo ili kupitia migogoro ya hifadhi na kero za ardhi zinazowakabili wananchi nchi nzima. Aliwataka wananchi kuwa wavumilivu wakati timu hiyo ikikusanya malalamiko ya wananchi na kuyafikisha kwa Rais na baadaye yatatolewa uamuzi.

Alisema kufuatia agizo la serikali la kurejesha vijiji 366 vilivyokuwa vimependekezwa kufutwa, Rais Magufuli amesimamisha zoezi la kuwahamisha wananchi katika maeneo yao, huku akiwataka waliowekewa alama ya kuhama waendelee kuishi bila hofu.

"Rais amesimamisha zoezi la kuhamisha wananchi kwenye vijiji 366 ambavyo vilisajiliwa na serikali hiyo hiyo inayotaka viondoke, tutapitia maeneo yaliyotajwa ili kubaini mpaka wa pori na vijiji," alisema na kuongeza:

"Maliasili walichukua maeneo bila kushirikisha wananchi, zoezi lolote litakaloendeshwa na Maliasili lazima liwe shirikishi kwa sasa."

Alisema awali maombi ya wananchi yalikuwa ni kupewa kilomita 10 kutoka kwenye mpaka wa hifadhi na pori la akiba la Maswa kwa ajili ya malisho ya mifugo yao.

Lukuvi alieleza kuwa hata mipaka ya mapori ya akiba iliwekwa bila kushirikisha wananchi wanaopakana na maeneo hayo, hali iliyochochea migogoro.

Kwa upande wao, wananchi walisema tangazo la serikali namba 482 limekuja kuharibu mipaka na uhusiano uliopo kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi.

Walisema tangu mwaka 1974 wananchi waliishi katika maeneo hayo, na makaburi ya ndugu zao yapo kwenye maeneo waliyotakiwa kuondoka.

"Sheria namba 5 ya mwaka 2009 ya wanyamapori ilileta mgogoro kwa sababu ilianzishwa bila kushirikisha na kuzingatia mahitaji ya wananchi waishio kando ya maeneo hayo...tangazo la serikali namba 235 la mwaka 1968 la kutenganisha pori la akiba linaanzia katika bikoni sahihi namba 49," alisema Peter Ndekeja, mkazi wa kijiji cha Sakasaka wilayani Meatu.

Akisoma taarifa kwa niaba ya wananchi, Martine Deusdedith, alisema awali wananchi walitakiwa wahame mita 500 kutoka kwenye maeneo ambayo waliishi kwa mipaka zaidi ya 30 wakifanya shughuli za kiuchumi ikiwamo kilimo na ufugaji.

Mbali na Lukuvi mawaziri wengine wanaounda timu hiyo ni Luhaga Mpina (Mifugo na Uvuvi); Seleman Jaffo (Tamisemi); Omary Mgumba (Naibu Waziri wa Kilimo); Prof. Makame Mbarawa (Maji na Umwagiliaji); Hussein Mwinyi (Ulinzi na JKT); Mussa Sima (Naibu Waziri Mazingira) na Dk. Khamis Kigwangalla (Maliasili na Utalii).


RADIO One

POPOTE ULIPO SIKILIZA RADIO ONE KATIKA MASAFA YAFUATAYO




www.radioone.co.tz

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Mawaziri waje na suluhu migogoro ya ardhi nchini

**KATIKA** jitihada za serikali kuhakikisha inatafuta ufumbuzi migogoro ya ardhi nchini kati ya wananchi na maeneo ya hifadhi, timu ya mawaziri wanane inafanya ziara ya kutembelea maeneo kadhaa kusikiliza malalamiko ya wananchi.

Kwa kuwa suala la ardhi ni mtambuka ndiyo maana Rais John Magufuli ametuma idadi kubwa ya mawaziri ambao wanaongozwa na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi.

Wengine wanaounda timu hiyo ni Luhaga Mpina (Mifugo na Uvuvi); Seleman Jafo (Tamisemi); Omary Mgumba (Naibu Waziri wa Kilimo); Prof. Makame Mbarawa (Maji na Umwagiliaji); Hussein Mwinyi (Ulinzi na JKT); Mussa Sima (Naibu Waziri Mazingira) na Dk. Hamis Kigwangalla (Maliasili na Utalii).

Mbali na kupitia maeneo ya wananchi yanayopakana na hifadhi za taifa na mapori ya akiba, mawaziri hao pia wameshatembelea baadhi ya maeneo ya wananchi yanapozungukwa na vyanzo vya maji likiwamo linalopakana na bwawa la Mindu katika Manispaa ya Morogoro, ambapo walisitisha uamuzi wa kuziondoa kaya 133 baada ya kukamilisha taratibu.

Aidha, wameshatembelea eneo lenye mgogoro wa ardhi katika Manispaa ya Ilemela mkoani Mwanza baina ya wananchi, Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) na Uwanja wa Ndege.

Akizungumza jana na wananchi wa Kata ya Mwandoya wilayani Meatu mkoani Simiyu, Lukuvi alisema Rais Magufuli ameunda timu hiyo ili kupitia migogoro ya hifadhi na kero za ardhi zinazowakabili wananchi nchi nzima.

Aliwataka wananchi kuwa wavumilivu wakati timu hiyo ikikusanya malalamiko ya wananchi na kuyafikisha kwa Rais na baadaye yatatolewa uamuzi.

Alisema kufuatia agizo la serikali la kurejesha vijiji 366 vilivyokuwa vimependekezwa kufutwa, Rais Magufuli amesimamisha zoezi la kuwahamisha wananchi katika maeneo yao, huku akiwataka waliowekewa alama ya kuhama waendelee kuishi bila hofu.

Migogoro ya ardhi nchini hususan inayohusisha wananchi na taasisi imekuwa ikiongezeka kila uchao, pengine kutokana na kutokuwapo usimamizi madhubuti wa mamlaka husika.

Kadhalika, sheria nyingi zilitungwa muda mrefu, hivyo zinaendelea kutumika bila kuzingatia mazingira halisi ya wakati uliopo likiwamo ongezeko la watu na mifugo.

Ongezeko la watu linaendana na mahitaji ya maeneo kwa ajili ya kilimo na matokeo yake wakulima wanalazimika kusogelea maeneo yenye maji ili kufanya shughuli za kilimo. Hivyo hivyo ongezeko la mifugo linawafanya wafugaji wasake maeneo ya kulisha.

Ndiyo maana serikali imeone ifike mahali isitishe matakwa ya kisheria ya kuwaondoa wananchi wanaoishi na kufanya shughuli za uchumi karibu na hifadhi pamoja na vyanzo vya maji, ili kufanya utafiti wa kina kwanza na kuona namna ya kulitafutia suala hilo ufumbuzi.

Inatia moyo kuona idadi kubwa ya mawaziri kutoka wizara mbalimbali wanashirikiana kwenda katika maeneo yenye migogoro hiyo na kuzungumza na wananchi ili waeleze historia, kero na mapendekezo yao.

Ni matarajio yetu kuwa timu ya mawaziri itawasikiliza wananchi hao kisha kuandaa taarifa yenye kuzingatia hali halisi kuhusiana na migogoro hiyo kisha kumshauri vizuri Rais Magufuli. Hayo yakizingatiwa, bila shaka migogoro hiyo itakuwa imepatiwa ufumbuzi kwa miaka mingi ijayo.

Tunampongeza Rais Magufuli kwa kulitafutia ufumbuzi tatizo hili kwa kutumia hekima, busara na uvumilivu kwa maslahi mapana ya nchi yetu.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com

BUSARA

**UKITAKA KUELEWEKA**

**UKITAKA UJUMBE WAKO UWAFIKIE WALENGWA UNAOWAKUSUDIA KWA MAFANIKIO MAKUBWA SHARTI UTUMIE LUGHA AMBAYO WALENGWA WAKO WANAIELEWA, UKITUMIA MSAMIATI RAHISI; KWA WAKATI MUAFAKA NDANI YA MAZINGIRA RAFIKI. KINYUME CHA HAPO UNAALIKA SINTOFAHAMU MIONGONI MWAO. NA BALOZI CHRISTOPHER LIUNDI**




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Raphael Kibiriti

## Wananchi 'kujiongeza' ni siri ya maendeleo si kuisubiri serikali

**MAENDELEO** ni moja ya mada inayovuta mijadala sehemu yoyote na katika kada mbalimbali za kimaisha.

Ukianzisha mada ya kwa nini kanda fulani ama mkoa umeendelea kwa mfano utakumbana na hoja zenye mitazamo tofauti juu ya mada hiyo. Na si ajabu kukumbana na mitizamo isiyokubaliana juu ya vigezo vya maendeleo ya nchi zilizoendelea, zinazoinukia na hata jamii au mtu aliyeendelea.

Aidha, kuna mitazamo tofauti juu ya nani anayeleta maendeleo ya mtu ama watu katika jamii au maeneo yao. Na ndiyo maana ya kusikia malalamiko dhidi ya serikali kwamba haijajenga daraja, haijachonga barabara, haijaleta karvati kwenye mtaro na wakati mwingine ikilalamikiwa kwa nini haijaikata miti inayohifadhi vibaka!

Kwamba kila changamoto ya maendeleo, hata iwe ndogo kiasi gani ambayo inaweza kutatuliwa na wananchi wenyewe, bado kuna watu katika baadhi ya maeneo watabaki wakisubiri serikali itatue changamoto hiyo.

Muungwana hakubaliani asilani na mtazamo akiongozwa na dhana kuwa, maendeleo ya watu huletwa na wao wenyewe kwa kushirikiana na serikali.

Inajulikana kwamba, serikali kama serikali ina wajibu na majukumu ya kufanya katika dhana nzima ya kuchangia maendeleo ya wananchi wake. Na baadhi ya majukumu na wajibu wa serikali ni pamoja na kudumisha amani kupitia sheria na amri mbalimbali zinazokusudia kulinda maisha na mali za watu wake.

Lakini pia kukuza demokrasia, haki za binadamu, kuzalisha ajira, kukuza uchumi na kutoa huduma za kijamii kwa wananchi.

Huduma kama zile za kujenga miundombinu, hospitali, mabomba ya maji, umeme, elimu na zingine zenye mchango katika kuboresha maisha ya wananchi.

Kwa mantiki hiyo ni kweli serikali ina wajibu na majukumu ya kufanya kwa ustawi wa watu wake katika hiyo dhana nzima ya kuleta maendeleo. Lakini, ambacho Muungwana hakubaliani nacho na ambacho anaona si haki kwa wananchi, ni kitendo chao cha kuiachia serikali kila kitu, hata kwa vitu ambavyo kimsingi viko chini ya uwezo wao.

Mara nyingi Muungwana amesikiliza, ametizama na kusoma malalamiko kwenye vyombo vya habari kutoka kwa wananchi wakiilalamikia serikali kwa sababu ya changamoto ambazo wangeweza kuzitatua wenyewe wakitumia raslimali zao.

Kwamba wananchi wameshindwa 'kujiongeza' hata katika suala la kununua koki ya maji ili bomba liendelee kuwahudumia kwa muda mrefu, na badala yake wanasubiri serikali ilete koki ya bomba, ili waendelee kupata huduma ya maji. Unakuta wananchi wanailalamikia serikali kutowajengea kivuko ama daraja dogo la mbao au miti kwenye bonde dogo linalopitisha maji wakati wa masika, na hivyo kusababisha watoto wao wasiende shule, wakati wangeweza 'kujiongeza' kidogo na kutatua changamoto hiyo.

Nimesikia malalamiko juu ya wananchi dhidi ya serikali kwamba imeshindwa kudhibiti utoro wa wanafunzi wanaozagaa katika mitaa yao wakati walipaswa kuwa shuleni, kana kwamba hilo hawezi kulidhibiti, yaani wakisubiri serikali ije isaidie kupiga doria.

Muungwana hakubaliani na hili la kuacha kutatua baadhi ya changamoto kwa kigezo cha kuisubiri serikali izitatue, wakati wananchi wenyewe wangeweza kuzitatua mapema iwapo 'wangejiongeza' Tuna maeneo hapa nchini ambayo yaliona umuhimu wa 'kujiongeza' muda mrefu kwa kutoitegemea serikali kwa kutoitegemea serikali na sasa yamepiga hatua kubwa za kimaendeleo.

Maeneo hayo hayakufungwa na upofu wa kuitegemea serikali kwa kila kitu na hata kwa changamoto zilizo chini ya uwezo wao.

Maeneo hayo yamepiga hatua kubwa za za kimaendeleo katika nyanja nyingi kama vile elimu, afya, maji na miundombinu kutokana na kulibaini hilo mapema.

Muungwana anatoa rai kwamba si muda tena kwa wananchi kusubiri kila kitu wafanyiwe na serikali, na badala yake wahamasishane wao wenyewe kutatua changamoto za maendeleo ziliko chini ya uwezo wao.

# BARUA & MJADALA

## Tunahitaji fedha zetu zitengeneze daraja

*Mhariri*

*MIMI ni mmoja kati ya wananchi wanaozikubali sana jitihada za Rais John Pombe Magufuli ya kuchapa kazi ili kujiletea maendeleo kama mtu mmoja mmoja, lakini na kwa ustawi wa taifa la Tanzania kwa ujumla wake.*

*Aidha, ni mmoja miongoni mwa Watanzania walio wengi ambao wanaikubali sana dhana ya wananchi kuchangia maendeleo ya eneo lao pale walipo, kwa kushiriki kwenye miradi mbalimbali ya kujitolea nguvu kazi ama kuchangia fedha.*

*Ninafanya hivyo kwa sababu michango kama hiyo huwa ina faida za moja kwa moja kwetu sisi wananchi au hata kama si ya moja kwa moja, ina faida zake kwa mgongo wa nyuma kwa maana ya ama watoto na wajukuu wetu, kama siyo kwa jirani zetu. Kunapokuwa na changamoto kwa mfano ya barabara ambayo wananchi wana uwezo wa kuilima au ya daraja ambalo wananchi wanaweza kubeba mawe au kuchangia kidogo fedha ili daraja la kuwasaidia liweze kujengwa, basi mimi huwa niko mstari wa mbele kushiriki.*

*Na ndiyo maana nimeshiriki kwa mapana sana katika kutoa michango mbalimbali iliyohusu kuchangia ujenzi wa zahanati katika kijiji chetu au ujenzi wa madarasa, nikielewa fika kuwa huo ni wajibu wa msingi kufanya.*

*Hata hivyo, Mhariri ninapokuja kupinga ua kutokubaliana na aina hii ya uchangiaji wa nguvu kazi ama fedha kutoka kwa mwananchi ni pale ambapo michango hiyo inapoishia hewani, bila kutekeleza kilichokusudiwa. Na ndicho kilichonifanya leo hii niandike barua hii kwako Mhariri, nikiwa mkazi wa Kinondo Mashariki, Kata ya Mabwepande, Wilaya ya Kinondoni, jijini Dar es Salaam.*

*Mimi pamoja na wakazi wenzangu wa wa Kinondo Mashariki, tulichangia shilingi 70,000 kila kaya kwa ajili ya ujenzi wa daraja litakalorahisisha usafiri katika eneo la Mji Mpya.*

*Sasa hadi miaka imepita, na daraja hatuoni likijengwa huku viongozi wetu, kwa maana ya Mwenyekiti wetu wa mtaa pamoja na diwani wetu wa Kata ya Mabwepande, wakiwa kimya kama vile hakuna kitu kilichofanyika.*

*Mhariri, hapa ndipo ninapokuja kupingana na aina hii ya uchangiaji kwa sababu tunapochanga kwa ajili ya maendeleo yetu, inapaswa tulichochangia kionekane na si vinginevyo. Ninaomba basi kupitia kwako wahusika watueleze fedha zetu zilipo kwa kuwa hatuoni daraja likijengwa na tatizo bado lipo.*

***Mwananchi Kinondo Mashariki, Dar***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**




## Serikali na jamii iwalinde watoto wanaoishi, kufanya kazi mitaani

**Na Raphael kibiriti**

**KUNA** maeneo ya msingi ambayo yameendelea kuwa ni ya kipaumbele kwa miongo sasa na hususani kutoka enzi ya serikali ya awamu ya kwanza hadi hii ya tano.

Kimsingi yanakuwa ni ya kipaumbele kutokana na umuhimu wake katika dhima nzima ya kuleta maendeleo na ustawi wa familia, jamii na taifa kwa ujumla wake.

Mojawapo ya maeneo hayo ni la kujenga na kurithisha malezi yenye maadili yanayokubalika kwa watoto na vijana ambao ni taifa la kesho.

Kwamba watoto na vijana ndiyo roho ama uti wa mgongo wa jamii yoyote ile, hivyo wanapaswa kupewa kipaumbele katika malezi tena yenye maadili kuwawezesha kuchukua majukumu yao wakati ukifika.

Mjadala unaangazia katika safu hii eneo hili la malezi ya watoto wa taifa hili sasa kama mchango wake kufuatia changamoto mbalimbali zinazozidi kuripotiwa kila siku zikilikabili kundi hili.

Changamoto zinazojumlisha ukatili ukiwamo wa mauaji kama ulioripotiwa mikoa ya Njombe na Simiyu hivi karibuni, lakini mateso mbalimbali yakiwamo ya vipigo, kubakwa, ulawiti, ukeketaji, ndoa na mimba za utotoni kwa kutaja baadhi.

Na kwa kuwa watoto wanaangukia kwenye makundi yaliyo pembezoni ama yenye mahitaji maalumu kama ilivyo kwa wanawake, wazee na watu wenye ulemavu, wanahitaji ulinzi wa jamii na taifa ili waweze kufikia ndoto zao za kimaisha.

**Takwimu za serikali kwa kushirikiana na RCI kutoka katika majiji sita nchini ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Iringa zinaonyesha kwamba kuna jumla ya watoto 10,595 wanaoishi na kufanya kazi mitaani.**

Watoto ni kundi lenye uhitaji kwa sababu bado hawajafikia umri wa kujitegemea kama unavyoelezwa na sheria.

Kwa mujibu wa Sheria ya Mtoto ya Tanzania ya mwaka 2009, Kifungu cha 4 (1), mtoto ni mtu yeyote aliye na umri wa chini ya miaka 18.

Hivyo basi, Mjadala unaposikia ukatili wa aina na aina ukifanywa dhidi ya watoto, unazidi kushawishika kwamba bado juhudi za serikali na jamii kwa ujumla wake zinahitaji kuchagizwa zaidi.

Bado juhudi zinahitajika kutoka kwa serikali, jamii, wadau na wazazi ama walezi wenyewe ambao kwa namna moja ama nyingine ni chanzo cha vitendo vyote vya kikatili vinavyofanywa dhidi ya kundi hili.

Mjadala unasema bado juhudi zinahitajika kuchukuliwa zaidi huku ukitambua hatua mbalimbali zilizofanikishwa hadi sasa na serikali, wadau na jamii katika dhima nzima ya ulinzi wa haki za kundi hili.

Baadhi ya juhudi hizo ni pamoja na kutungwa kwa sheria ya mtoto ya mwaka 2009, harakati za kupinga mimba za utotoni, ukeketaji na Sheria ya Makosa ya Kujamiiana ya mwaka 1998, iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Hata hivyo, wakati jamii ikiendelea kupigia kelele kuheshimiwa kwa haki za kundi hili la watoto, ndani yake kuna kundi dogo ambalo kwa maoni ya Mjadala ni kama limesahaulika.

Kwamba limesahaulika ama halijapewa kipaumbele cha kutosha kutoka kwa kada mbalimbali za watu katika kupigania ustawi wake.

Ninazungumzia kundi la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

Na ndiyo maana hata kama madhira yake yanazungumziwa ni katika mitazamo ama vionjo tofauti kutoka kwa jamii.

Hali hii kwa maoni ya Mjadala inachagizwa na kukosekana kwa ufahamu wa kutosha dhidi ya madhira yanayolikabili kundi hili. Mjadala unazungumzia kundi la watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani maarufu kwa jina la 'Watoto wa mitaani,' jina ambalo si sahihi kwa mujibu wa Rose Kagoro alipokuwa akitoa mada juu ya madhira ya kundi hili kwa waandishi wa habari jijini Dar es Salaam hivi karibuni.

Kagoro ni Meneja wa Uratibu Mikakati kutoka shirika la kimataifa lisilo la kiserikali la Railway Children Africa (RCA), linalopigania haki za watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani, akibainisha kwamba 'Mtaa hauzai mtoto!'

Takwimu za serikali kwa kushirikiana na RCI kutoka katika majiji sita nchini ya Dar es Salaam, Arusha, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Iringa zinaonyesha kwamba kuna jumla ya watoto 10,595 wanaoishi na kufanya kazi mitaani.

Watoto 6,393 miongoni mwao wakiwa chini ya umri wa miaka 18 na 4,202 wakiwa na zaidi ya miaka 18 hadi miaka 25.

Kimsingi idadi hii ni kubwa kwa sababu ni kama unaongelea shule za msingi 10 zenye wanafunzi takribani 1,000 kila moja.

Ni kwa mantiki hiyo, Mjadala unaona kwamba wakati umefika kwa jamii kwa maana ya wazazi, walezi, serikali na wadau kuelewa kuwa watoto wanaoishi na kufanya kazi mitaani ni kama watoto wengine.

Na kwa hali hiyo wana haki sawa na wanastahili fursa stahiki kama ilivyo kwa watoto wengine, hivyo hatua zichukuliwe kulinda ustawi wa watoto hawa.

**KABWELA** — Na Fadhili Mohammed



# Korti yapokea majumuisho kesi ya mauaji mwanafunzi

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MAHAKAMA Kuu Kanda ya Bukoba imepokea majumuisho kutoka kwa mawakili wa Upande ya Jamhuri na watetezi katika kesi ya mauaji dhidi ya Spelius Eradius, mwanafunzi wa Shule ya Msingi Kibeta, Manispaa ya Bukoba.

Kesi hiyo inawakabili walimu wawili wa wa shule hiyo, Respicius Mtazangira na Heriet Gerald, wanaoshtakiwa kwa mauaji dhidi ya mwanafunzi huyo Agosti 27, mwaka jana.

Katika kesi hiyo ya mauaji namba 156, Mtazangira ni mtuhumiwa namba moja na Heriet Gerald mtuhumiwa namba mbili wa mauaji dhidi ya mwanafunzi huyo.

Upande wa utetezi unaongozwa na Wakili Aaron Kabunga ambaye alidai sehemu ya ushahidi uliotolewa na Jamhuri ina shaka kwa kuwa maelezo ya awali yametofautiana na ya mahakamani.

Wakili wa Serikali Mkuu Hashimu Ngole aliyeongoza upande wa Jamhuri alidai ushahidi wa awali hauwezi kutosheleza vigezo vya kisheria kufanya Mahakama kutotia washtakiwa hatiani kutokana na maelezo yaliyotolewa mahakamani.

Waki Ngole alidai msingi wa mashtaka ni kile kilichosababisha mauaji dhidi ya mwanafunzi Spelius Eradius na kuwa ushahidi mwingine uliotolewa mahakamani kutoka upande wa utetezi haukujikita kwenye chanzo cha kifo.

Baada ya majumuisho hayo, Jaji wa Lameck Mlacha, alisema atasikiliza ushauri wa wazee Februari 22, mwaka huu na baada ya hapo, watapanga hukumu ya kesi hiyo.

## Babu ateketea kwa moto

INATOKA UK 3

kuanza kuyaunguza.

Kamanda Bukombe alisema baada ya moto huo kushika katika mashamba ya watu wengine, Shekizenge alijaribu kuuzima ili usiendelee kuunguza mashamba hayo lakini alizidiwa na moshi wa moto.

Bukombe alisema baada ya kuzidiwa na moshi akiwa anazima, alizingirwa na moto, hivyo kushindwa kukimbia kutokana na ulemavu aliokuwa nao na hatimaye kuungua mpaka kuteketea kabisa.

Diwani wa Songa wilayani Muheza, Leslie Nchimbi, alisema baada ya tukio hilo, viongozi walitoa taarifa katika kituo cha Polisi Wilaya ya Muheza.

Alisema polisi na daktari kutoka Hospitali Teule ya Wilaya ya Muheza, walifika eneo la tukio kwa ajili ya uchunguzi kisha kuruhusu mwili wake uzikwe baada ya uchunguzi.



Wakazi wa jiji wakiangalia ajali iliyolihusisha gari lenye namba za usajili T 198 DJB na bajaj, katika makutano ya Barabara ya Luthuli na Kivukoni, jijini Dar es Salaam jana. Hakuna aliyejeruhiwa katika ajali hiyo. **PICHA: JOHN BADI**

## Kifungo miaka 45 mauaji tembo 430

INATOKA UK 2

washtakiwa.

Baraga alidai kuwa Novemba 2015, aliagizwa na bosi wake kwenda kwenye Kituo cha Polisi Oysterbay kufanya tathmini ya meno ya tembo.

Baraga alitoa madai hayo alipoalikwa na mahakama kutoa ufafanuzi wa athari na hasara inayotokea kuhusu ujangili wa mauaji ya tembo wakati wa usikilizwaji na kuisaidia mahakama kutoa adhabu dhidi ya tuhuma za uhujumu uchumi na kukutwa na nyara za serikali.

Alidai kuwa alikwenda na alipofanya tathmini ya nyara za serikali wanazodaiwa kukutwa nazo washtakiwa, alikuta meno ya tembo 860.

Baraga alidai kuwa meno hayo ni sawa na tembo 430 waliouawa, kila tembo ana thamani ya Dola 15,000 (jumla kuu ni Dola za Marekani 6,450,000, sawa na Sh. bilioni 13.932).

Mbali na Glan na Matembo, mshtakiwa mwingine katika kesi hiyo ni Philemon Manase. Upande wa Jamhuri uliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Paul Kadushi, pamoja na Mawakili wa Serikali Simon Wankyo na Salim Msemo.

Msemo alidai kuwa, washtakiwa ni wakosaji wa mara ya kwanza, lakini mahakama itoe adhabu kali na amri nyingine inayoona inafaa.

Alidai kuwa uwapo wa genge na utendaji wa makosa ya uhujumu uchumi chini ya Kifungu cha 60 (2) cha Sheria ya Uhujumu Uchumi, adhabu yao ni miaka isiyozidi 15.

Alisema Kifungu cha 84(1) cha Sheria Na. 5 ya Usimamizi wa Wanyamapori, faini yake si chini ya mara mbili ya fedha za nyara wanazodaiwa kukutwa nazo.

Wakili wa Utetezi, Nehemia Nkoko, alidai washtakiwa ni wakosaji wa mara ya kwanza, hivyo mahakama iwaonee huruma na kwamba wameshakaa mahabusu miaka mitano.

Alidai washtakiwa wawili wanategemewa na familia zao na kukaa kwao jela kutaathiri maisha ya watoto wao kupata elimu bora.

Hakimu alisema pamoja na kwamba washtakiwa ni wakosaji wa mara ya kwanza, wameporomosha uchumi na kusababisha madhara makubwa kwa Watanzania. Alisema nyara za serikali walizohujumu washtakiwa, fedha zake zingetosha kujenga shule, hospitali na barabara za nyingi nchini.

"Mshtakiwa wa kwanza na wa pili, ninyi ni Watanzania lakini mmekubali kuisaliti nchi yetu, watoto wenu, ndugu zenu kwa kula keki ya taifa peke yenu. Mshtakiwa wa tatu ulikaribishwa nchini kwa ukarimu, lakini umejiingiza kwenye ujangili na kuliibia taifa letu," Hakimu Shaidi alisema wakati akitoa adhabu kwa washtakiwa hao.

Washtakiwa walikuwa wanakabiliwa na mashtaka ya kujihusisha na biashara haramu ya meno ya tembo yenye thamani ya Sh. bilioni 13.9 kinyume cha sheria.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao, wanadaiwa kutenda makosa hayo kati ya Januari Mosi, 2000 na Mei 22, 2014.

Washtakiwa wanadaiwa katika kipindi hicho, walifanya biashara ya meno ya tembo 860 yenye thamani hiyo.

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, aliwataka Watanzania kuiga mfano wa wasamaria wema waliowaibua Glan na wenzake katika mapambano dhidi ya kuhujumu taifa.

Alisema mahakama imetenda haki kutoa adhabu hiyo kwa mujibu wa sheria. Alisema Watanzania wawafichue watu wanaowatilia shaka ya kuhujumu uchumi kama washtakiwa waliohukumiwa kwenda jela jana.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Wanyamapori Tanzania (Tawa), Dk. James Wakibara, alisema hukumu hiyo ni faraja kwa wahifadhi nchini kwa kuwa inaonyesha jinsi gani serikali imedhamiria kupambana na ujangili na kuna ushirikiano baina ya taasisi zake katika kupambana na suala hilo.

Alisema kipindi cha nyuma ilikuwa ngumu sana kwa kuwa licha ya jitihada za taasisi za uhifadhi kupambana na ujangili, lakini kesi nyingi zilifutwa au watuhumiwa kuachiwa kwa kisingizio cha kukosa ushahidi.

"Hii inaonyesha kuwa ushirikiano wa kitaasisi utawezesha mafanikio makubwa katika vita dhidi ya ujangili nchini. Ujangili ni mtandao mkubwa sana na wenye watu wazito wenye nguvu zao, hivyo kupambana nao inahitaji nguvu ya pamoja," alisema.

Mkurugenzi wa Shirika la Hifadhi za Taifa (Tanapa), Dk. Allan Kijazi, alisema wamefurahia uamuzi huo kwa kuwa kuna watu wanaohujumu maliasili hiyo wamechukuliwa hatua.

"Tunatumia nguvu nyingi sana kuhifadhi maliasili hii na kupambana na mtandao wa ujangili. Hukumu hiyo iwe fundisho kwa wengine wenye mtandao wa ujangili, wajue serikali imedhamiria kutokomeza ujangili kuanzia ngazi ya chini hadi juu," alisema.

Dk. Kijazi aliongeza: "Kama mahakama imeunga mkono vita hii, ni wazi kuwa kutakuwa na mafanikio makubwa na ujangili nchini utakuwa historia kwa kuwa sasa serikali inafanya kazi kwa ushirikiano na taasisi zake."

## Mtaala wa pamoja

INATOKA UK 5

Chuo cha Sayansi ya Afya na Tiba cha Bugando (Cuhas) na Chuo Kikuu cha Afya (KCMC).

Alisema mradi huo wa miaka mitano umefadhiliwa na Serikali ya Marekani kupitia Shirika la JHIEPIGO kwa Dola za Marekani milioni tatu.

Alisema katika kuandaa mtaala huo, watawakutanisha wadau wote wa afya ili kujadili kwa pamoja upungufu, changamoto na namna ya kuandaa mtaala huo utakaotumiwa na vyuo vyote vya afya nchini.

"Lengo la kushirikiana na vyuo hivi vitatu kwa ajili ya kuandaa mtaala huu ni kuboresha ufundishaji kwa walimu, wahitimu na kuwaongezea ufanisi katika utendaji kazi wao," Prof. Kaaya alisema.

Alieleza zaidi kuwa, watawashirikisha TCU, wanafunzi, walimu, wahitimu, wizara zote zinazohudumia sekta ya afya ili kufahamu upungufu uliyoko kwa ajili ya kuufanyia kazi.

Mkurugenzi Mwendelezaji wa Mafunzo Endelevu na Weledi kutoka Muhas, Dk. Doreen Mroka, alisema mtaala huo utazalisha wahitimu wa sekta ya afya walio na viwango vya elimu na uelewa unaolingana.

"Tofauti na ilivyo sasa kila chuo kina mtaala wake unaowezesha kuzalisha wanafunzi wenye viwango tofauti kulingana na chuo alichosoma jambo ambalo tuliona si sawa kwa ustawi wa sekta ya afya," alisema.

Alieleza kuwa katika kipindi hicho cha miaka mitano ya utekelezaji wa mradi huo, wataanza kukusanya maoni, kuandaa rasimu, kuifanyia marekebisho na baadaye kupeleka kwenye mchakato wa kuwa mtaala.

"Kuna suala la utawala, wauguzi wengi wanapewa kazi ya kuwa viongozi, lakini hawana mafunzo ya uongozi ni mambo ambayo yanapaswa kuwapo katika mtaala huu, lakini kwanza tuwasikie wanasemaje na wanakwama wapi na kwa sababu gani. Pia tujue kwanini hawapendi kufanya kazi maeneo ya vijijini, yote haya tutajadili," alisema Dk. Doreen.

## NEC yatoa msimamo

INATOKA UK 3

mpigakura na kuboresha mifumo ya uandikishaji na utunzaji wa kumbukumbu za daftari.

Alisema kuwa, kwa mujibu wa Kifungu cha 15(5) cha Sheria ya Uchaguzi, Sura ya 343, NEC iko katika hatua za kufanya maandalizi ya uboreshaji wa daftari kwa majaribio katika baadhi ya mikoa.

Wiki iliyopita, Chadema kupitia kwa Katibu Mkuu wake, Dk. Vicent Mashinji, alisema moja ya mapendekezo ya Kamati Kuu ya chama hicho ni uchaguzi wa serikali za mitaa kusimamiwe na NEC na daftari la kudumu la wapigakura kutumika katika uchaguzi huo.

Watanzania 22,751,292 waliandikishwa na NEC kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015 na huku Tume ya Uchaguzi Zanzibar (ZEC) ikiandikisha wapigakura 505,193.

HABARI KITAIFA

# Hakimu alalamikia ushahidi wa kesi mimba za wanafunzi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

HAKIMU wa Mahakama ya Mwanzo Kata ya Chibe, Shinyanga Mjini, Eva Kassa, amelalamikia kitendo cha wanafunzi kushindwa kutoa ushahidi mahakamani, kwa kugoma kuwataja watuhumiwa ambao wamekuwa wakiwapatia ujauzito na kukatisha ndoto zao.

Alisema kwenye mahakama hiyo amekuwa akipokea kesi nyingi zinazohusu wanaume kuwapatia ujauzito wanafunzi, lakini hakuna ushirikiano kutoka kwa wanafunzi kutokana na kutowataja wahusika ambao wamekuwa wakiwapatia ujauzito huo.

Kassa alibainisha hayo juzi kwenye kikao cha Shirika la WEADO la mjini Shinyanga, lilipokuwa likitambulisha mradi wa kutokomeza mimba na ndoa za utotoni kwenye Kata ya Chibe mjini hapa.

Alisema kumekuwapo na kesi nyingi zinazohusu wanafunzi kupewa ujauzito, lakini zimekuwa zikiishia hewani kutokana na ushahidi kukosekana, na kuwa sababu ni wahusika kushindwa kutoa ushirikiano, kwa kugoma kuwataja wanaume ambao wamewapatia ujauzito huo.

"Ili kukomesha janga hili la wanafunzi kupewa ujauzito shuleni, inatakiwa kuwapo na umoja wa vyombo vya sheria, wazazi, pamoja na wanafunzi wenyewe kwa kutowaficha wahusika ambao wanawapatia ujauzito huo ili tupate kuwafunga jela, ndipo vitendo hivi vitakwisha tofauti na hapo mimba zitaendelea kuwapo," alisema Kassa.

Naye Mratibu wa Elimu wa Kata ya Chibe, Thadey Ottaru, alitaja takwimu za mwaka jana kuwa wanafunzi wawili wa shule ya msingi walikatishwa masomo kutokana na kupewa ujauzito, lakini hakuna hata mtuhumiwa aliyefungwa jela, kutokana na wanafunzi kugoma kuwataja mahakamani.

Ofisa mradi wa kutokomeza mimba na ndoa za utotoni kutoka shirika hilo la WEADO, Nkinda Joseph, alisema kwenye mradi huo watakuwa wakitoa elimu ya afya ya uzazi kwa wanafunzi, pamoja na wazazi kutambua umuhimu wa elimu na kupenda kuwasomesha watoto wa kike ili kumaliza tatizo la mimba shuleni.

# Waziweka kando itikadi, waomba miradi barabara

**Na George Tarimo,** IRINGA

WAJUMBE wa kikao cha Bodi ya Barabara Mkoa wa Iringa wameungana bila kujali itikadi za vyama na kuiomba serikali kutekeleza ujenzi wa miradi ya barabara ikiwamo barabara ya Iringa-Msembe katika Hifadhi ya Taifa ya Ruaha.

Wajumbe hao kutoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema), akiwamo mwenyekiti wa CCM Mkoa wa Iringa, Abel Nyamahanga na Mbunge wa Iringa Mjini, Mchungaji Peter Msigwa, kwa pamoja wameitaka serikali itekeleze ahadi ya ujenzi wa barabara hiyo yenye urefu wa zaidi ya kilometa 100.

**Wanapaswa kuungana na kushikamana na wasisubiri sana fedha ya Benki ya Dunia (WB) kwa sababu ina masharti.**

Nyamahanga alisema: "Jukumu hili la ujenzi wa barabara tunatakiwa sote tupambane tuwe kitu kimoja, lakini tukikaa kimya kwamba tuliiambia serikali kwamba ipo kwenye ilani ya uchaguzi, tutashangaa vipindi vya uchaguzi vyote vinapita."

Msigwa alisema wanapaswa kuungana na kushikamana na wasisubiri sana fedha ya Benki ya Dunia (WB) kwa sababu ina masharti.

Alisema ni vizuri viongozi wa mkoa na wabunge kushikamana kujenga barabara hiyo ili kuondoa changamoto za usafiri kwenye Hifadhi ya Ruaha.

Meneja wa Wakala wa Barabara Tanzania (Tanroads) Mkoa wa Iringa, Mhandisi Daniel Kindole, alisema wakala huo ulishaanza kujenga barabara hiyo kwa kilomita chache, huku wakisubiri serikali kuu kutoa fedha za kuijenga barabara pamoja na barabara ya Ipogolo (Iringa mjini)-Kilolo.

Mwenyekiti wa kikao hicho ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, aliwataka wajumbe na Tanroads mkoani Iringa, kutafuta wadau wa kusaidia ujenzi wa miradi hiyo, huku akiwatahadharisha kutotegemea mradi wa Regrow.



Mkurugenzi wa Huduma kwa Wateja wa Vodacom Tanzania, Harriet Lwakatare, akizungumza na wanahabari (hawako pichani) wakati wa uzinduzi wa kampeni ya 'Naweza na Vodacom' uliofanyika jana, makao makuu ya kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam. Kulia ni Mkurugenzi wa Uhusiano na Mawasiliano wa kampuni hiyo, Rosalynn Mworia na Mkuu wa Idara ya Ufanisi kwa Wateja, Najenjwa Mbagga. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Vodacom yawezesha wateja kujihudumia

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya simu ya Vodacom Tanzania PLC, imezindua kampeni iitwayo "Naweza na Vodacom" kwa lengo la kuelimisha wateja wake njia mbalimbali za kidijitali za kujihudumia na kutatua matatizo yao kwa urahisi na unafuu zaidi.

Uzinduzi huo umefanyika jana makao makuu ya kampuni hiyo jijini Dar es Salaam, zikiwa jitihada zake za kuhakikisha wateja wake wanapata huduma za haraka na kwa ufanisi zaidi hasa wakati huu ambao ulimwengu umekuwa kidijitali,

kampeni hiyo inalenga zaidi kuwaelimisha wateja wa Vodacom kuhusu njia mpya za kidijitali za kujihudumia na kupata taarifa mbalimbali pale wanapohitaji msaada.

Mkurugenzi wa Idara ya Huduma kwa Wateja, Harriet Lwakatare, amesema njia hizo ni kama kutumia mitandao ya jamii, wavuti, applikesheni kama my Vodacom na M-Pesa, kutumia taarifa zilizorekodiwa kupitia namba ya huduma kwa wateja (IVR). Pamoja na njia mbalimbali za kurudisha muamala endapo utakosea na kujua jinsi ya kujihudumia pale ambapo utakuwa umesahau namba ya siri ya M-Pesa.

"Tunajali muda na kazi za wateja wetu, hivyo tumeona ni wakati mwafaka wa kuwajulisha na kuwaelimisha kuwa tumeongeza ubunifu katika kuwahudumia. Lengo letu ni kuhakikisha mnapata msaada wa haraka zaidi na kuendelea na majukumu mengine ya kujenga taifa. Sisi kama kampuni ya kidijitali, tumejikita zaidi katika kutumia teknolojia kutatua changamoto za wateja wetu," alisema Lwakatare.

"Takwimu kutoka Mamlaka ya Mawasiliano (TCRA), zinaonyesha kwamba, Tanzania ina watumiaji wa huduma za simu takribani milioni 42, hivyo kampuni za mitandao ya simu hazinabudi kuwapa kipaumbele watumiaji hawa wote na kuhakikisha wanapata huduma zenye ubora wa hali ya juu. Vodacom Tanzania ikiwa ni kampuni inayoongoza katika soko kwa kuwa na wateja millioni 13 inahakikisha kwamba wateja wote wanapata huduma bora kupitia watoa huduma (call center), maduka, madawati ya kutoa huduma na mitandao ya kijamii."

"Napenda kuwahimiza wateja wetu kuungana na sisi katika mageuzi haya ya kidijitali kwa kuwa ulimwengu umebadilika, ili kuendana na wakati basi yatupasa hata sisi kwa pamoja tukubaliane na mabadiliko haya," aliongeza Lwakatare.

# Jafo ataka wadau kuchangia ujenzi madarasa, madawati

**Na Rose Jacob,** MWANZA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amewataka wadau mkoani Mwanza kujitokeza na kuchangia suala zima la ujenzi wa madarasa na madawati ili kuhakikisha wanafunzi wanasoma katika mazingira bora ambayo yatawasaidia kujifunza vyema.

Jafo aliyasema hayo wakati wa makabidhiano ya vyumba vya madarasa saba ya Shule ya Msingi Igelegele iliyopo Kata ya Mahina Wilaya ya Nyamagana mkoani Mwanza, ambayo yamejengwa na mdau wa Shirika la SOS Children's Villages lengo la kuhakikisha changamoto ya ukosefu wa madarasa na madawati unamalizika ndani ya jamii ya wanafunzi.

**Magari hayo yatasaidia kukuza utalii hata kwa watoto wenye umri chini ya miaka 18 kufika katika kilele cha mlima huo.**

"Juhudi na jitihada zinazoendelezwa na serikali pamoja na wadau ya kuhakikisha uchache wa madarasa unaoendelea kusababisha msongamano kwa wanafunzi, kikwazo katika kuongeza ubora wa elimu unapungua au kuisha, leo tumeona mfano mzuri kwa watu wa Shirika la SOS Children's Villages wametambua umuhimu wa elimu kwa kujenga madarasa saba," alisema Jafo.

Aidha, Jafo akiwataka wanafunzi kuhakikisha wanaachana na tabia za kuweka masuala ya mpira, miziki na mambo ambayo yanahatarisha masomo yao na kujikuta wanakuwa ni vijana wa kufanya vibaya katika mitihani, jambo ambalo linaharibu ndoto zao.

Naye Mkurugenzi wa Shirika la SOS Children's Villages, David Mulongo, akitoa taarifa mbele ya Jafo, alisema ujenzi wa madarasa saba na ukarabati wa vyumba vya madarasa nane katika shule za msingi na sekondari Igelegele ulianza mwaka 2017 na kukamilika Novemba mwaka 2018.




Naibu Mkurugenzi Mtendaji wa Halotel, Nguyen Van Tung, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati wa uzinduzi wa bando lijulikanalo kama Royal na Tomato Bando ambalo litawawezesha watumiaji kupiga simu za nje kwa gharama nafuu. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Virutubisho kinga kwa magonjwa vyaja

**Na Mwandishi Wetu**

WATANZANIA wameshauriwa kutumia virutubisho vya Stemregen vilivyofanyiwa utafiti wa kiafya na kukubalika matumizi yake katika nchi mbalimbali duniani ili kujikinga na magonjwa yanayoweza kuepukika kwa kuwa virutubisho hivyo hutengeneza chembe hai ziitwazo 'Stem Cells' ambazo huukinga mwili na maradhi.

Virutubisho hivyo ambavyo vimefanyiwa utafiti Marekani na kuthibitishwa na Mamlaka ya Chakula na Dawa (TFDA) vimeweza kuwa msaada mkubwa kwa watu wanaokumbwa na magonjwa mbalimbali ikiwamo kisukari, shinikizo la damu na magonjwa sugu.

Akizungumza wakati wa hafla ya uzinduzi wa matumizi ya virutubisho hivyo jijini Dar es Salaam, Daktari Bingwa, Dk. Walter Kweka, alisema virutubisho hivyo vina faida kubwa sana katika mwili wa binadamu.

"Virutubisho hivi vimeanza kuingia nchini baada ya kuonyesha mafanikio makubwa katika mataifa ya Marekani na Malaysia na sisi kama wadau tumeona ni vyema Watanzania wakaanza kuvitumia ili kuondokana na matatizo mbalimbali ya kiafya," alisema Dk. Kweka.

"Faida kubwa ya kutumia virutubisho vya Stemregen ni pamoja na kuongeza nguvu za kiume, kuleta nafuu kubwa kwenye magonjwa ya migongo, mifupa na viungo mwilini, lakini ikitumika na matibabu ya dawa za saratani inapunguza madhara yaletwayo na dawa za saratani na pia kupunguza ukuaji na kasi ya saratani," alifafanua.

Kwa upande wake Dk. Hawa Kawawa alisema: "Faida za virutubisho vya Stemregen ni kubwa kwa kuwa huwakinga watu na maradhi mbalimbali, lakini huweza kutibu iwapo mtu hakuligundua tatizo lake mapema. Kwa hiyo nawasihi Watanzania kuanza kutumia virutubisho hivi mapema kwa kuwa kinga ni bora kuliko tiba."

"Kumekuwa na changamoto kubwa juu ya gharama za upatikanaji wa virutubisho, lakini tutakapoanza kuviingiza rasmi hapa nchini tutahakikisha vinapatikana kwa bei ambayo inaweza kufikiwa na

Watanzania wengi hususani wa kipato cha chini na muhimu zaidi, mamlaka ya chakula na dawa kuthibitisha virutubisho hivi," alifafanua Dk. Kawawa.

# Wateja wa Halotel kupiga simu, kutumia intaneti bila kikomo

**Na Jumbe Ismailly,** SINGIDA

KAMPUNI ya mawasiliano ya simu ya Halotel imeanzisha huduma ya 'Royal Bundle' ambayo itawawezesha wateja wake kupata huduma zisizo na kikomo.

Huduma hizo ni kama vile kupiga bila kikomo simu za ndani na kimataifa, kutumia intaneti bila kikomo pamoja na kuunganishwa moja kwa moja pindi vifurushi vitakapokwisha.

Akizungumza wakati wa uzinduzi wa huduma hiyo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mkuu wa Halotel Tanzania, Nguyen Van Trung, alisema mbali na kuzingatia ubora na unafuu wa huduma zao, ubunifu ni silaha kubwa ambayo wanaitegemea katika kuwafikia wateja wa makundi yote katika kila kona ya nchi.

"Royal Bundle' imekuja kukata kiu ya wateja ambao walikuwa wanatamani kutumia huduma zetu bila ya kupata bugudha ya aina yoyote zikiwamo salio kuisha au intaneti kukata.

Tunatambua umuhimu wa sekta ya mawasiliano katika shughuli za kiuchumi, hivyo tusingependa kampuni yetu kuwa kikwazo katika kulifanikisha hilo. Ndiyo maana leo tunawatangazia Watanzania wote kuwa kwa shilingi 10,000 tu unaweza kupiga simu za ndani na kimataifa kama vile kwenda nchi za India, China, Canada na Marekani bila ya kikomo, kutumia intaneti bila ya kikomo, kutuma SMS bila ya kikomo, na kama haitoshi, mara tu muda wa kifurushi utakapokwisha tutakuunganisha mara kwa mara," alisema Van.

Alisema faida ni nyingi za kujiunga na huduma hii. Kwa mfano, kwa shilingi hiyo hiyo 10,000 kwa mwezi mteja atajipatia muda wa maongezi wa dakika 520 kupiga simu mitandao yote, kifurushi cha intaneti yenye kasi cha GB 2, pamoja na kuwezeshwa SMS 500. Endapo kifurushi hiki kitafikia ukomo, mteja ataweza kuwasiliana kwa gharama nafuu kabisa. Ataweza kupiga simu kwenda mitandao yote kwa shilingi 1 tu, atatumia shilingi 2 tu kwa sekunde kupiga simu kimataifa, atajipatia MB 1 kwa shilingi 5 tu, na kutuma SMS kwa shilingi 2 tu. Kiufupi ukiwa na 'Royal Bundle' hakuna huduma yenye ukomo," alisisitiza Mkurugenzi wa Halotel nchini.

Aidha, mkurugenzi huyo alitumia fursa hiyo kuzindua huduma nyingine ya "Tomato Bundle" ambayo ni maalum kwa wateja wa Halotel nchi nzima, itakayowawezesha kupiga simu bure kwenda namba yoyote ya Halotel kwa dk 5 za mwanzo kwa kila simu pamoja na kupata salio la ziada la bure la Sh. 4,000 ambalo mteja atalitumia kwenye huduma nyingine za Halotel (kwa mwezi mzima).

# Waziri awajia juu wanaotorosha mifugo

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdalla Ulega, amewataka wafanyabiashara wa mifugo kuacha kupeleka mifugo Kenya kwa njia za magendo na badala yake waipeleke soko la mifugo lililoko Kijiji cha Eworendeke, wilayani Longido.

"Msipeleke mifugo Kenya, acheni Wakenya waje wenyewe sokoni kununua, pia wakati tukiendelea kutatua changamoto zinazowakabili, epukeni tabia ya kutorosha mifugo kwa njia za magendo," aliwataka.

Alisema hayo wakati akizungumza na wafanyabiashara wa mifugo sokoni hapo juzi, ambapo pia alisikiliza kero zao.

Asilimia 95 ya ujenzi wa soko hilo umetekelezwa kupitia Programu ya Miundombinu ya Masoko, Uongezaji wa Thamani na Huduma za Kifedha Vijijini- (MIVARF), huku Halmashauri ya Wilaya ya Longido ikichangia asilimia tano.

Naibu Waziri Ulenga, alisema soko hilo limejengwa kwa ajili ya wafanyabiashara kupeleka mifugo na kisha kuuza ili wajikwamue kiuchumi na kuhakikisha Serikali Kuu na Halmashauri zinapata ushuru wa kuiendesha sekta ya mifugo.

**Msipeleke mifugo Kenya, acheni Wakenya waje wenyewe sokoni kununua, pia wakati tukiendelea kutatua changamoto zinazowakabili, epukeni tabia ya kutorosha mifugo kwa njia za magendo.**

"Mkileta mifugo hapa ni lazima Wakenya watakuja kununua, na anayetakiwa kulipa tozo ya mifugo hiyo ni mnunuzi (Mkenya) na si ninyi, ninyi bakini hapa sokoni kama madalali tu, waacheni waje wenyewe," alisema.

Kuhusu kero ya tozo, alisema ataziwasilisha kwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, ili kujadiliana namna watakavyoweza kutengeneza tozo rafiki kati ya serikali na wafanyabiashara hao.

"Sheria hii mpya ya mifugo inayosafirishwa kwenda nje ya nchi mbuzi mmoja Sh. 7,500 na ng'ombe mmoja Sh. 30,000 ilianza kutumika Oktoba 1, mwaka jana, na kwa kuwa ilishapitishwa, hivyo, utaratibu utaanza upya kuangalia namna utakavyofanyiwa marekebisho ili iwe rafiki kwenu.

"Awali tozo hii ilikuwa Sh. 5000 kwa mbuzi mmoja na Sh. 20,000 kwa ng'ombe mmoja, lakini bado mlikuwa mkikwepa kulipa tozo hii, serikali inawapenda wananchi wake haina nia mbaya kwenu, miradi ya maendeleo mnayoipata katika wilaya yenu ni kwa sababu ya mapato, sasa mkikwepa kulipa nchi itajiendesha na nini," alisema.

Alisema kero kubwa ya malalamiko yao ni tozo hii ya wizara kuwa kubwa, hali ambayo huwafanya baadhi ya wafanyabiashara hao kutorosha mifugo na wakati mwingine mifugo kutaifishwa.

Alisema sheria iko wazi kwa mtu anayekamatwa akitorosha mifugo ambapo kitu cha kwanza atalipa tozo ya mifugo aliyokuwa akikwepa pamoja na faini na akiweza kufanya hivyo atarudishiwa mifugo yake, lakini kama atashindwa kulipa kodi na fani mifugo itataifishwa na kuwa mali ya umma na kisha kupandishwa mahakamani.

"Msikubali Tanzania kuwa eneo la ufugaji na malisho, halafu malighafi yote wanafaidi Wakenya tena kwa kuwapelekea ninyi wenyewe kwa njia za magendo, wanafaidi nyama, ngozi, pembe, kwato na baadaye wanazalisha nakuja kutuuzia Watanzania, badilikeni sasa," alieleza.

Mwenyekiti wa wafanyabiashara wa mifugo soko la MIVRAF, Saruni Laizer, alisema sababu kubwa ya wao kupitisha mifugo njia za panya ni kutokana na tozo hiyo ya mifugo inayoenda nje ya nchi kuwa kubwa.

"Tunalipishwa kichwa cha mbuzi Sh. 7,500 na ng'ombe Sh. 30,000 kwa kweli ni kubwa sana, tunaomba serikali itufanyie kichwa cha mbuzi Sh. 4,500 na cha ng'ombe Sh. 15,000 wakifanya hivyo hatutatorosha tena," alidai.

Alieleza hadi sasa ni zaidi ya mifugo 800 imetaifishwa baada ya kukamatwa zikivushwa kwa njia za panya na kudai kuwa hata sasa idadi ya wafanyabiashara hao imepungua kutokana na wengine kukosa mitaji ya kujiendeleza.

"Tozo hii imetuletea umaskini, watu wengine wamechukua hela kwenye vikoba na kukopa benki, sasa hivi wamefilisika na hii opereshini Zagamba ya kukamata kamata mifugo inayotoroshwa nje ya nchi bila kufuata taratibu," alisema.

Alieleza hapo awali magari yalikuwa yakija zaidi ya magari 50 kwa siku moja, lakini kwa sasa ni magari mawili hadi moja na hii yote ni watu kukwepa hiyo tozo hivyo hulazimika kupiga njia za panya, tozo hiyo ni kubwa hata tukienda kuuza hiyo mifugo kwenye mbuzi tunapata faida Sh. 3,000 hadi Sh. 5, 000 na ng'ombe Sh. 10,000 hadi Sh. 15,000.

Mbunge wa Longido, Dk. Steven Kiruswa, aliiomba serikali kuacha kutaifisha, mifugo inayokiuka taratibu za kisheria na badala yake walipe faini punde wanapokamatwa.

Alisema wafanyabiashara hawa hawajapata elimu juu ya tozo na hawajashirikishwa, hivyo kuna umuhimu wakutoa elimu ili kuepusha msuguano kati ya serikali na wafanyabiashara wa mifugo.

Alisema wapo tayari kulipa tozo hiyo ya mifugo endapo itakuwa rafiki kwao na watakuwa mabalozi wakukemea watakaojitokeza kuvusha kwa njia za magendo.

## Watendaji wa kata wafundwa migogoro

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

MAOFISA watendaji wa kata na watendaji wa mitaa kutoka kata 25 jijini hapa, wamepata mafunzo juu ya sheria za mipango miji ili waweze kuondokana na migogoro mbalimbali inayosababishwa na ukosefu wa elimu hiyo.

Mratibu kutoka Mradi wa Miji, Mikakati Tanzania, (TSCP), Felista Shayo, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuhakikisha watendaji hao wanapata elimu juu ya mipango miji sambamba na kuzitambua sheria zake ili waweze kutenda haki kwa wananchi wanaowazunguka katika kata zao.

Alisema Jiji la Arusha linakabiliwa changamoto ya makazi mengi holela hali ambayo inahitaji kupangwa, hivyo uwepo wa mafunzo hayo utasaidia kuondokana na changamoto ya miji isiyopimwa.

Alisema watendaji wengi hawana elimu ya kutosha juu ya sheria na utoaji wa vibali vya mipango miji hali ambayo mwisho wa siku huchangia kuwepo kwa makazi holela kutokana na kutofuatwa kwa sheria za mipango miji.

Kwa upande wa Ofisa Mipango Miji kutoka kampuni inayojihusisha na masuala ya mipango miji ya Spatial Planning Vision Co Ltd, ambao ndio wawezeshaji, Alpha Mangula, alisema kumekuwapo na migogoro mbalimbali ya ardhi pamoja na ujenzi holela katika maeneo mengi hali inayosababishwa na watendaji kutokana na ukosefu wa elimu juu ya mipango miji.




Mkuu wa Mkoa Arusha, Mrisho Gambo (wa pili kushoto), akimpongeza Mwakilishi wa Ubalozi wa China nchini Tanzania, Gac Wei, baada ya ubalozi huo, kukabidhi vifaa tiba vyenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 61 katika Kituo cha Afya Muriet, kilichopo Halmashauri la Jiji la Arusha juzi. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

## Wakurugenzi kuchongewa kwa JPM

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MWENYEKITI wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika nchini, Dk. Titus Kamani, ametishia kuwashtaki kwa Rais John Magufuli, wakurugenzi wanaoshindwa kuwalipa watumishi ambao wanakatwa fedha zao kwenye Saccos walizoanzisha watumishi hao.

Dk. Kamani alitoa tishio hilo kwa wakurugenzi wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji mwishoni mwa wiki iliyopita wakati akizungumza na viongozi mbalimbali wa vyama vya ushirika zikiwamo Saccos ambazo zilianzishwa na vyama vya wafanyakazi wa kada tofauti tofauti, alipokuwa kwenye ziara yake mkoani Manyara.

"Na wakurugenzi wanaoshindwa kuwalipa watumishi kwenye Saccos nitawachongea kwa aliyewateua ili atengue uteuzi wenu maana hii ni dhuluma wanayofanya hawa watumishi, hili ni jasho lao wanatakiwa kulipwa," alisema.

Aidha, alisema kama kuna wakurugenzi wanaendelea kujizungusha katika suala hili la kuwalipa watumishi wanaodai fedha zao dawa yao iko jikoni inachemka ili watumishi hao waweze kupata haki yao.

"Wakurugenzi wanaoshindwa kuwalipa watumishi hawa ambao wamekatwa kwenye Saccos zao ni kuwafanya wakose jasho lao ambalo lingeenda kuzinufaisha familia zao na kuwasaidia kukidhi mahitaji yao ili wafanye kazi vizuri," alisisitiza.

Mapema akichangia kwenye mkutano huo, Fortunatus Kalewa, kutoka Mbulu alisema wakurugenzi ambao wanakula fedha za mapato yanayotokana na makato ya Saccos ya mishahara yao aliomba wapewe ili wasiwe na madeni katika Saccos zao.

Hoja ya mjumbe huyo iliungwa mkono na wajumbe wengine kutoka halmashauri karibu zote za mkoa hapa ambazo watumishi wenye Saccos walilia kilio cha kutokulipwa fedha zao kwa muda mrefu sana wakati wanakatwa kila mwezi.

# Rombo waomba fidia ya kujeruhiwa na nyani

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

WANANCHI kutoka kaya 15 za Wilaya ya Rombo, wameiangukia serikali wakitaka kulipwa fidia ya fedha kutokana na kujeruhiwa na nyani waliovamia makazi yao pamoja na kuharibu mazao yao mashambani.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Agness Hokororo, amesema amewasilisha rasmi ombi la wananchi hao kwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu.

"Kwa siku kadhaa nimepokea malalamiko ya wananchi hasa wanaoishi katika maeneo yaliyo karibu na hifadhi kwamba wanyama mbalimbali na hasa nyani wamevamia makazi yao na wanagombea chakula na watoto katika familia za watu.

**Kwa siku kadhaa nimepokea malalamiko ya wananchi hasa wanaoishi katika maeneo yaliyo karibu na hifadhi wanyama mbalimbali na hasa nyani wamevamia makazi yao na wanagombea chakula na watoto.**

Hokororo aliongeza: "Mpaka sasa nimeshapokea malalamiko ya wananchi zaidi ya 15 ambao wanaomba serikali ifikirie walao kuwalipa kifuta jasho kutokana na hasara waliyoipata, na mimi hivi ninavyoongea nimewasilisha kwa Naibu Waziri Kanyasu, ili wakalijadili hilo na waziri mwenye dhamana, Dk. Hamis Kigwangalla na ikiwezekana wachukue hatua."

Wanyama wengine ambao wamekuwa wakifanya uharibifu kama huo katika Wilaya ya Rombo ni pamoja na tembo na nyati ambao wamekuwa wakifanya uharibifu mkubwa wa mazao na kujeruhi wananchi wa baadhi ya vijiji vya wilaya hiyo.

Maeneo ambayo yamekuwa yakisumbuliwa na wanyamapori hao ni kata za Ushiiri, Mrao-Keryo, Kirua-Kei, Katangera-Mrere, Kirongo-Somanga na Olele.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo, changamoto hiyo ya wanyama pia imeleta uharibifu mkubwa wa miti kwenye mashamba ya taifa ya miti ya serikali ya Rongai na West Kilimanjaro.

Pamoja na ombi hilo, Kanuni za 'Dangerous Animals Damage Consolation' (kifuta jasho cha uharibifu wa wanyama hatari) zinaelekeza wazi kwamba ulipaji wa kifuta jasho kwa mujibu wa kanuni hizo, nyani si miongoni mwa wanyama wanaotambulia kisheria katika ulipaji wa kifuta jasho.



Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mary Mwanjelwa (kulia), akizungumza na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe na Halmashauri ya Mji wa Korogwe, mkoani Tanga juzi, wakati wa kikao kazi na watumishi kuhimiza uwajibikaji. Wapili kushoto ni Katibu Tawala Mkoa wa Tanga, Zena Said. **PICHA: OFISI YA RAIS UTUMISHI**

# Kabaka kufuatilia utekelezaji wa ilani

**Na Paul William,** MOSHI

UWEKEZAJI mkubwa wa upanuzi wa vituo viwili vya afya vya Ndungu na Pasua ambavyo viko chini ya majimbo yanayoongozwa na wapinzani, umemsukuma Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama Cha Mapinduzi (CC), Gaudensia Kabaka, kwenda kuweka mkazo kwamba yanayofanyika huko ni utekelezaji wa ilani ya chama hicho.

Taarifa iliyopatikana na kuthibitishwa na Katibu wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, imesema kuwa pamoja na mambo mengine, Kabaka amekwenda kuimarisha chama na kukagua utekelezaji wa ilani ya CCM.

Kituo cha Afya Ndungu kipo katika Jimbo la Same Mashariki linaloongozwa na Naghenjwa Kaboyoka na Kituo cha Afya Pasua kipo Jimbo la Moshi Mjini linaloongozwa na Jaffary Michael (wote Chadema).

Kabaka ambaye aliwahi kuwa Waziri wa Kazi katika serikali ya awamu ya nne, anawasili kesho mkoani Kilimanjaro na kupokelewa katika Wilaya ya Same kwa ajili ya kwenda kukagua maendeleo ya ujenzi wa Kituo cha Afya Ndungu ambacho kilitengewa Sh. milioni 400.

Fedha hizo zilitolewa na serikali kwa ajili ya mradi huo unaohusisha ujenzi maabara, chumba cha upasuaji, jengo la kufulia na wodi ya kinamama. Kabaka ndiye mlezi wa CCM mkoa wa Kilimanjaro kwa sasa.

Aidha, Kabaka atajadiliana na wana CCM Mkoa wa Kilimanjaro kuhusu kupanda kwa fukuto la uchaguzi wa serikali za mitaa na kuweka mkakati mzito wa kushinda viti vyote katika majimbo yanayoshikiliwa na upinzani.

Kutokana na mkakati huo, Mabihya ameeleza: "Mwenyekiti huyu wa UWT Taifa, anataka wanachama wa CCM Mkoa wa Kilimanjaro wahakikishe kwamba katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, wagombea wa chama tawala wanashinda ubunge wa Moshi Mjini, Hai, Rombo, Vunjo na Moshi Vijijini maeneo ambayo wapinzania wanatamba."

# CCM yatoa tamko mfumuko wa wamachinga

**Na Paul William,** MOSHI

UTITIRI wa wafanyabiashara wadogo wanaopanga bidhaa zao pembezoni mwa barabara na nje ya Soko kuu la Mbuyuni katika Manispaa ya Moshi, umeanza kuibua malalamiko ambayo yamekilazimisha Chama Cha Mapinduzi (CCM) kutoa tamko.

Katibu wa CCM, Mkoa wa Kilimanjaro, Jonathan Mabihya, ameeleza kuwa chama hicho hakiridhishwi na hali hiyo, na amemtaka Mkurugenzi wa Manispaa ya Moshi, Michael Mwandezi, kuhakikisha waliopo kando ya barabara wanahamishiwa ndani ya soko hilo haraka.

Mabihya alitoa tamko hilo jana, baada ya kusikiliza kero za wafanyabiashara wa soko hilo na wana CCM kumaliza kufanya usafi wa mazingira.

"Kufanya biashara pembezoni mwa barabara ni hatari kwa maisha yao, endapo gari likikosea njia linaweza kusababisha vifo, lakini pia sioni sababu ya wananchi hawa kuendelea kufanya shughuli zao barabarani, wakati katika soko yapo maeneo ambayo wanaweza kukaa na kufanya shughuli zao bila bughudha. Nakuagiza Mkurugenzi (Mwandezi) waondoe wafanyabiashara wote waliopo barabarani," alisema.

Mabihya alieleza kwamba kitendo hicho cha baadhi ya wafanyabiashara kupanga bidhaa zao pembezoni mwa barabara katika Soko la Mbuyuni kinasababisha wafanyabiashara waofanya shughuli zao ndani ya soko hilo kuwa ngumu kutokana na wateja kuishia barabarani.

Alieleza: "Watanzania tumekuwa wepesi mno kulalamika na kutaka maendeleo, wakati huo huo tunashiriki kwa kiasi kikubwa katika kukwamisha juhudi hizo za maendeleo. Kila siku kumekuwapo kelele za matatizo na kero mbalimbali ambazo tumekuwa tukiinyooshea kidole serikali bila kujua kuwa sehemu kubwa ya matatizo hayo inasababishwa na sisi wenyewe."

Awali, mmoja wa wafanyabiashara katika soko hilo, Samuel Kiwele, akiwasilisha kero hiyo alisema jambo hilo linaweza kuonekana la kawaida, lakini kwa kiasi kikubwa linaweza kusababisha madhara makubwa kiuchumi na hata kupoteza nguvu kazi ya taifa kutokana na ajali ambazo zinaweza kusababishwa na biashara hizo.

Ukurasa 18



NJELU KASAKA MWANASIASA MKONGWE ALIYEIBUKA KIVINGINE

**MAKALA:**

EAC itatue changamoto kabla ya kufikia ngazi ya shirikisho



Ukurasa 14

**KIMATAIFA:**



Mabilioni ya Qatar yatuliza munkari Gaza, lakini

Ukurasa 15

siasa

JUMATANO FEBRUARI 20, 2019

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe



Brexit inapofunikwa kwa uhasama wa Ufaransa, Italia kuhatarisha EU

Ukurasa 18

# Bila ya kuwa na demokrasia, mikutano ya AU haina tija

**Na Gaudensia Mngumi**

KIKAO cha kwanza cha Umoja wa Afrika (AU) kwa mwaka wa 2019 kimemalizika hivi karibuni jijini Addis Ababa, Ethiopia kikiwashirikisha wakuu wa nchi na viongozi wa serikali wa mataifa 55 ya bara hili yanayounda umoja huo.

Wakati wakuu wa Afrika wanafurahia kuliongoza bara hili linalopachikwa majina mengi yenye kejeli kama bara la giza 'dark continent', inavyoelekea mikutano ya AU huenda haina tija kwani hakuna utekelezaji wa maazimio, mikataba wala protokali inazojiwekea kujiletea maendeleo na kudumisha demokrasia.

Kwa mfano wapo wanaoendelea kuchezea katiba za mataifa yao kujiongezea muda wa kutawala, wakisababisha machafuko, chuki za kikabila na mauaji.

Mfano wa hivi karibuni ni wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) ambapo rais aliyekubali kuondoka madarakani Joseph Kabila, aliishi Ikulu tangu 2001.

Mara kadhaa alikataa kung'atuka na safari

ENDELEA UK 16



Rais Abdel Fattah el Sisi wa Misri, ambaye ni mwenyekiti mpya wa AU.

UCHAMBUZI

# EAC itatue changamoto kabla ya kufikia ngazi ya shirikisho

**Na Mashaka Mgeta**

MKUTANO wa wakuu wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) uliofanyika jijini Arusha Februari Mosi, mwaka huu, ulimalizika kwa kuweka maazimio kadhaa.

Miongoni mwa hayo ni lile lililoelekezwa kwa Baraza la Mawaziri wa EAC, kusimamia mchakato wa kuandikwa rasimu ya Katiba ya shirikisho la kisiasa la jumuiya hiyo, na taarifa yake kuwasilishwa kwenye mkutano wa 21 wa wakuu hao.

Kuwapo shirikisho la kisiasa la EAC ni moja katika nguzo nne zinazoijenga jumuiya hiyo, zikiwamo soko la pamoja, forodha na fedha (sarafu moja).

Marais John Magufuli (Tanzania), Uhuru Kenyatta (Kenya), Yoweri Museveni (Uganda) na Paul Kagame (Rwanda) walihudhuria huku Pierre Nkurunziza wa Burundi akiwakilishwa na Makamu wa Kwanza wa Rais, Gaston Sindimwo na Salva Kiir wa Sudan Kusini, aliwakilishwa na Waziri wa Mambo ya Nje, Nhial Deng Nhial.

Taarifa ya Katibu Mkuu wa EAC, Dk. Libérat Mfumukeko ikaeleza kuwa viongozi hao walimteua mshauri mwelekezi wa Katiba hiyo na kumtaka atoe taarifa yake ndani ya miezi saba.

Wakati hayo yakijiri, mwaka 2013 nchi za Kenya Uganda na Rwanda zilijaribu kuingia makubaliano ya kuharakisha mchakato wa kuundwa shirikisho la kisiasa pasipo kuihusisha Tanzania na Burundi. Baadaye Burundi ilitangaza kuwaunga mkono.

Kufikia hatua ya shirikisho ni jambo lenye maana pana kwa 'chombo' hicho cha ushirikiano wa kikanda, lakini inahitajika kuchukuliwa tahadhari kubwa ili kuepuka madhira kama yaliyotokea mwaka 1977.

Ikumbukwe kwamba EAC ya awali iliundwa mwaka 1967, lakini ilipofika 1977 yaani miaka 10 baadaye, jumuiya hiyo ilivunjika na kila nchi mwanachama ikabaki kivyake.

Mpango wa kuifufua EAC ulianza kwa mara nyingine na mkataba wa kwanza ukasainiwa Novemba 30, 1999, wakati huo nchi wanachama zikiwa tatu, yaani Tanzania, Kenya na Uganda.

Mkataba huo ulianza kutekelezwa rasmi Julai 7, 2000 ukijikita katika maeneo manne makuu ambayo ni soko la pamoja, forodha, fedha na shirikisho la kisiasa. Miaka saba baadaye (2007), nchi za Rwanda na Burundi zilijiunga katika jumuiya hiyo, kisha zikafuatiwa na Sudan Kusini iliyojiunga 2016.

Inapotazamwa EAC katika ujumla wake tangu kuundwa kwake na kuanza kutekelezwa kwa mkataba wa makubaliano, yapo mafanikio yanayotoa taswira chanya ya kuendelea kuwapo, kukomaa na kutimiza wajibu wao kwa umma.

Mathalani, kumeundwa Bunge la Afrika Mashariki (EALA), Mahakama ya Afrika Mashariki, umoja wa forodha na sasa hatua za kuwa na sarafu moja na shirikisho yapo katika hatua nzuri ya kujadiliwa. Hayo ni mafanikio ya kujivunia.

Pamoja na mafanikio hayo, nchi hizo zinapoelekea katika kuwa na shirikisho la kisiasa, ni vizuri zikabaini changamoto kadhaa zinazowakabili, iwe ni miongoni mwao ama nchi zote kwa ujumla wake.

**MIZOZO YA KIDIPLOMASIA**

Mizozo ya kidiplomasia inaonekana kuwa mfano wa 'bundi anayetua na kuruka kwenye EAC' kila baada ya muda, hali inayokwamisha maendeleo yake ikiwamo azma na dhamira ya kufikia katika shirikisho la kisiasa.

Kwa mfano, mgogoro uliopo sasa kati ya Rwanda na Burundi, unatajwa kuwa miongoni mwa vyanzo vya kuahirishwa kwa mikutano miwili ya wakuu wa nchi hizo iliyopangwa kufanyika mwishoni mwa mwaka jana.

Burundi inaishutumu Rwanda kwa kushirikiana na vikundi vya waasi vinavyofanya matendo yasiyo ya kibinadamu kama vile mauaji ya watu wasiokuwa na hatia ndani ya ardhi yake (Burundi).

Hata jaribio lililoshindikana mwaka 2015 la kuipindua serikali ya Rais Pierre Nkurunziza, bado Burundi inainyooshea kidole serikali ya Rais Paul Kagame wa Rwanda, kuwa inahusika.

Rwanda imekuwa ikiyakanusha madai hayo.

Miongoni mwa madhara ya uhusiano mbovu kati ya nchi wanachama ni taarifa kuwa mkutano wa marais wa nchi za EAC uliopangwa kufanyika Desemba 27, mwaka jana uliahirishwa, wiki tatu baada ya ule wa kwanza uliokuwa umepangwa kufanyika Novemba 30 kufutwa.

Sababu kubwa ikatajwa kuwa ni baada ya Burundi kusema kuwa haitashiriki kwa vile upo uhasama wa nchi hiyo na Rwanda.

Nchi mbili hizo zimekuwa katika mzozo lakini zaidi ukikolezwa na jaribio la mapinduzi ya kijeshi dhidi ya Rais Nkurunziza, Mei 13, 2015.

EAC haina budi kutambua kuwa, pamoja na kwamba tukio la nchi moja moja haliwezi kutafsiriwa kama sehemu ya mataifa yote, lakini uhusiano na ushirikiano kati ya nchi wanachama unapokosekana, si rahisi ikafikiwa hatua bora ya kuwa na shirikisho lililoimarika.

Kwa maana mgogoro si huo pekee unaoikabili EAC, ikumbukwe pia Rwanda bado ipo katika hali ya sintofahamu ya kidiplomasia na Uganda. Sasa hivi Rwanda imepokea uenyekiti wa EAC kutoka kwa Rais Yoweri Museveni.

Ipo haja kwa migogoro hii kupewa fursa inayowaleta pamoja wasuluhishi na pande zinazohusika, lakini zaidi wasuluhishi hao wakiwa wanakubalika kwa walengwa wote wa migogoro husika.

**UKATA WA EAC**

Zipo taarifa zinazoelezea kuhusu hali ya upungufu wa fedha na raslimali nyingine unaoikabili EAC.

Sehemu kubwa ya nchi wanachama inaelezwa hazijawasilisha michango yao kwa sekretarieti ya EAC, hali inayorudisha maendeleo ya jumuiya hiyo.

Kuwasilishwa kwa michango mapema si tu kwamba kunaiwezesha sekretarieti kufanya kazi zake ipasavyo, lakini kunajenga uimara wa kiuchumi wa jumuiya, hivyo kuipa uwezo endelevu wa kubuni, kutekeleza na kusimamia miradi yake ya maendeleo.

Sasa kama utoaji michango kwa nchi wanachama utakuwa wa kusuasua kiasi cha nchi nyingine kulimbikiza madeni yao, haiwezekani kutarajia kuwapo shirikisho bora la kisiasa kwa jumuiya hiyo. Huenda likawepo lakini lililo legelege na tegemezi.

Ndio maana, taarifa za hivi karibuni zinaeleza kushindwa kufanyika kwa mkutano wa Bunge la Afrika Mashariki (EALA) kwa sababu ya upungufu wa fedha unaoikabili jumuiya hiyo. Hiyo si ishara njema kuelekea katika shirikisho la kisiasa.

**Makala haya yameandikwa kwa msaada wa vyanzo mbalimbali. Mwandishi anapatikana kupitia simu namba +255 754 691540 ama barua pepe:mgeta2000@yahoo.com.**



Rais Paul Kagame wa Rwanda (kushoto) na Rais Pierre Nkurunziza wa Burundi. Ni viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC). **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> "Sasa kama utoaji michango kwa nchi wanachama utakuwa wa kusuasua kiasi cha nchi nyingine kulimbikiza madeni yao, haiwezekani kutarajia kuwapo shirikisho bora la kisiasa kwa jumuiya hiyo. Huenda likawepo lakini lililo legelege na tegemezi.



Rais John Magufuli wa Tanzania (kulia), Rais Yoweri Museveni wa Uganda (katikati) na Uhuru Kenyatta wa Kenya.



Rais Mahmoud Abbas wa Palestina (kulia), akiwa na Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu.. **PICHA: MTANDAO**

# Mabilioni ya Qatar yatuliza munkari Gaza, lakini Israel yajiandaa kwa vita

**Na Ani Jozeni**

WAKUU wa jeshi la Israel, waliozoea hali ya vita ya hapa na pale na kundi la kijihadi la Hamas linaloidhibiti Gaza, wanaangalia pande tofauti kama nchi tajiri kwa mafuta ya Qatar, ambayo sasa imetengwa na nchi nyingine za Ghuba ya Uarabuni kidiplomasia, itafaulu kuzuia kundi hilo lisianzishe vita nyingine dhidi ya Israel hivi punde.

Taarifa hizo zinakuja wakati ndani ya utawala wa Palestina Rais Mahmoud Abbas wiki iliyopita alitangaza kusimamisha malipo ya watumishi 5,000 wanaofanyakazi chini ya Hamas katika ukanda wa Gaza, hatua inayotokana, kwa upande mwingine, na kibano cha fedha baada ya Marekani kukata nusu ya pesa inazotoa kwa shirika la Umoja wa Mataifa kusaidia wakimbizi Palestina (UNRWA).

Ni kwa vile Abbas haongei na Marekani.

Mawasiliano kati ya utawala wa Marekani wa Rais Donald Trump na uongozi wa Palestina uliharibika baada ya Rais Trump kutangaza Desemba 2017 kuitambua Yerusalemu kuwa ndiyo mji mkuu wa Israel, wakati madai ya kufikia amani Palestina yanataka Yerusalemu iwe ndiyo mji wao mkuu.

Moja ya sababu za msingi ni kuwa kuna msikiti maarufu sana huko unaoitwa Al Aqsa, wakati Wayahudi hawana hekalu la maana mjini hapo, bali kuna masinagogi maridhawa.

Wanaharakati wa Palestina wanaona uwepo wa Israel ni uvamizi tu, inataka wafunge virago warudi kwao Ulaya, na unatazamia kuwa mzingiro wa Israel na kutumia makombora ya masafa mafupi na kati kutokea Gaza, mpaka wa Syria na wa Lebanon, ugaidi ndani ya Yerusalemu vitatosha kuichosha Israel.

Ni katika mazingira hayo ambako nchi ya Qatar inafanya diplomasia ngumu ya pembe tatu bila nchi nyingine kuelewa mshirika wake hasa ni nani, na inatazamia nini katika juhudi hizo.

Vyombo vya habari vya Israel vinasema kuwa kwa kukubaliwa na Israel kupitisha fedha kuingia Gaza, nchi hiyo ndogo ya Ghuba imetoa dola bilioni moja kwa utawala huo wa Hamas tangu 2012.

Zinasema kuwa mwaka jana Qatar iliipa Gaza dola milioni 200 kwa misaada, nishati na kulipa mishahara serikalini, na kuwa inatazamiwa kutoa mamia ya mamilioni ya dola mwaka huu.

Taarifa hazikutolewa rasmi na serikali mojawapo kati ya Israel, Qatar au utawala wa Hamas eneo la Gaza ila zilikusanywa na mojawapo ya mashirika ya misaada yanayofanya kazi eneo la Gaza kwa muda.

Baadhi ya wachunguzi wa habari wanasema kuwa fedha zinazotolewa na Qatar sana sana zinasaidia watu wa Gaza kupata mlo mmoja kwa siku ikiwezekana au na ziada kidogo, na kuwa Israel inaruhusu Qatar ipeleke fedha hizo kwa sababu imezingira mipaka ya Gaza hivyo inahusika na mahitaji ya msingi ya wakazi wa eneo hilo.

Israel inajivua jukumu hilo ikisema kuwa sera ya vita ya kundi la Hamas linalodhibiti eneo hilo linafanya Israel muda wote iwe katika mazingira ya kujilinda, jukumu ambalo haliwezi kuoanishwa na kusimamia ustawi wa Gaza wakati kundi la Hamas halikubali usimamizi wa shughuli za Gaza na utawala wa Rais Abbas.

Isitoshe, njaa na ukali wa maisha ni mtaji katika sera ya vita ya Hamas, kwani inawasukuma wengi kujitolea kupigana.

Wakati Qatar inajitahidi kuhakikisha kuwa Gaza inakalika na wananchi wake wanakuwa na uwezo wa kupata mahitaji ya lazima kama chakula na tiba, uhusiano wake na Hamas unaonekana kama ni kuiwezesha Hamas kufuatilia ajenda yake ya vita isiyoisha na Israel.

> Ndiyo maana kinachosimamia mikakati ya Hamas siyo misaada na hisia za Qatar bali kuunganisha nguvu za kijeshi na hata katika ugaidi kufikia malengo yaliyopo.

Wakati Marekani haina ugomvi na Qatar kwa suala hilo, ni nchi za Kiarabu eneo la Ghuba na kwingineko zilizovunja uhusiano na Qatar mwaka 2017 kwa madai ya kuunga mkono ugaidi, kwani nchi hiyo pia inaruhusu kundi la Islamic State kutoa maelezo yake katika kituo cha Al Jazeera kinachoangaliwa dunia nzima.

Isitoshe, wapinzani katika nchi tofauti za Kiarabu kama mwandishi nguli wa Saudia aliyeuawa katika ubalozi mdogo Istanbul, Uturuki, wanapata jukwaa katika kituo hicho, n.k.

Kundi la Hamas linaorodheshwa kama la kigaidi na nchi za Marekani, Israel, Misri, Falme za Kiarabu (Ghuba), Saudia na Canada wakati hatua hiyo ya kuitenga Qatar iliendana na matukio nchini Uturuki ya kusafisha jeshi dhidi ya waliodaiwa kutaka kumpindua Rais Recep Tayyip Erdogan, 2017.

Cha msingi ni kuwa kiongozi huyo alihitaji kusafisha jeshi kuondoa wakereketwa wanaounga mkono kundi la Islamic State ambalo lilisaidia kuinuliwa huko Syria na Iraq na majasusi wa Marekani, Uturuki na baadhi wanadai, hata Israel kwani kundi hilo ni adui wa Iran, adui namba moja wa Israel katika ukanda wa Mashariki ya Kati.

Lilipofikia hatua ya kutishia nchi zote katika ukanda huo, kumeza majeshi kujiunga 'siasa kali,' ikabidi njia zitafutwe kupigana nalo.

Wachunguzi wa habari wanasema Israel inashindwa kuelewa kwa kina dhamira ya utawala wa Qatar hasa ni nini, kwani umesimama katikati ya makundi ya mahusiano kimkakati au mifungamano ya kijeshi katika eneo hilo.

Uhusiano wake wa karibu na Hamas unatafsiriwa kuwa ni wa kuisaidia Iran ambayo ni mfadhili wa Hamas hasa katika masuala ya kijeshi au kiusalama, na fedha pale inapowezekana, lakini uwezo wake wa kuituliza Gaza na kusikilizana na Hamas kiasi fulani unaisaidia Israel ambayo haitaki ilazimike kupigana kila mara ukanda wa Gaza, kwani inaweza kuchochea vita kubwa zaidi licha ya kuwa nchi za Kiarabu zina tatizo kwa kiasi fulani na uongozi wa Hamas.

Wachunguzi wanasema Qatar, Uturuki, utawala wa Palestina na Hamas wana mahusiano ya hapa na pale, huku uhusiano wa Qatar na China ukiwa unaimarika zaidi, kama ambavyo Marekani, Israel na Misri wana uhusiano wa karibu kidiplomasia na kijeshi ambao kwa kawaida hautetereki.

Jambo la kushangaza ni kuwa Rais Abbas mara kadhaa amekuwa akipinga kutolewa fedha na Qatar kwa ajili ya kutuliza hali eneo la Gaza, wakati Qatar inaaminika kuwa inaisukuma Hamas kufikia makubaliano ya msingi na Israel.

Hata hivyo, wachunguzi wa habari hawatazamii kuwa Qatar itafaulu katika juhudi hizo, zinazoendana na sera za China za 'ukanda wa hariri na barabara,' kutaka dunia ya utandawazi ambako nchi zote zinaelewana bila kujali historia zao, mifumo ya uchumi, siasa au itikadi.

Lengo la Hamas, kama ilivyo Iran, ni kuiondoa Israel katika ramani na kuleta ushindi wa kihistoria dhidi ya wavamizi wa Kiyahudi kutoka Ulaya.

Ndiyo maana kinachosimamia mikakati ya Hamas siyo misaada na hisia za Qatar bali kuunganisha nguvu za kijeshi na hata katika ugaidi kufikia malengo yaliyopo.

Kwa vile Israel inaingia katika uchaguzi mkuu ikiwa tayari imegawanyika kwa kina na kutengwa kimataifa kupitia wimbi la kuitenga serikali ya Waziri Mkuu Benjamin Netanyahu linaloendeshwa na Wayahudi nchini Marekani kwa sehemu kubwa, inakuwa ni wakati muafaka wa kuitikisa.

Isitoshe Hamas imekuwa ikijaribisha makombora na kupiga viunga vya miji Kusini ya Israel, na Iran inatafuta kisingizio cha kushambulia Israel kwa nguvu ili kuilazimisha Marekani kutafuta suluhu na siyo vikwazo vya uchumi na mzingiro wa kijeshi.

Mkuu mpya wa jeshi la Israel, Jenerali Aviv Kochavi, alifanya ziara yake ya kwanza ya makambi ya jeshi kwa divisheni iliyoko kando ya Gaza, akapitisha kwa haraka mpango wa kuboresha uwezo wa jeshi la Israel kuingia katika mapambano ya aina yoyote ile huko Gaza, iliyohitaji bajeti mpya kamilifu.

MAKALA

Inatoka Uk.13

# Bila ya kuwa na demokrasia, mikutano ya AU haina tija

ya mwisho ilikuwa aondoke Desemba 2016.

Japo amemkabidhi uongozi Rais mpya Felix Tshisekedi, ukweli ni kwamba ameacha makovu mengi kuanzia vifo vya raia, mateso na machafuko kutoka kwa makundi ya waasi.

Kadhalika nchini Uganda, uongozi ulio madarakani ulichukua nchi tangu 1986 na sasa unatimiza miaka 33.

Na ndivyo ilivyo huko Congo-Brazaville, ambako Rais Denis Sassou Nguesso, ameongoza taifa hilo kwa takribani miaka 30 sasa.

Kunga'ng'ania madarakani na kuchezea demokrasia ndiyo mambo yanayoilazimisha AU kuibua mikataba na protokali mbalimbali kwa ajili ya wanachama wake.

Kwa mujibu wa ripoti za Idara ya Siasa ya Umoja huo, AU ya leo imebadilisha majukumu yake na kujipa mwelekeo mpya tofauti na OAU za zamani. Umoja huo ulipoanzishwa ulikuwa na jukumu la kupigania uhuru na kuleta ukombozi wa Afrika.

AU ya sasa imejipa sura mpya ikijikita zaidi kwenye harakati za kujiimarisha kidemokrasia, kujiletea maendeleo na kudumisha utawala bora, hatua zilizochukuliwa tangu mwanzoni mwa miaka ya 2000.

Ripoti za Idara ya Siasa ya Kamisheni ya AU zinasema ili kujiimarisha Afrika ilianzisha mpango wa kujitathimini yenyewe 'Africa Peer Review Mechanism-APRM.'

Ni mkakati ulioasisiwa na Marais wa zamani wa Nigeria, Olusegun Obasanjo na Thabo Mbeki wa Afrika Kusini, kama kioo cha kujitathmini kila mmoja akijichunguza na kujipima kupitia kwa mwenzake na kuiga pale penye mafanikio.

Ili kuwa na Afrika yenye demokrasia na utawala bora, AU imeanzisha Mkataba wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala (ACDEG) ulioanza kutekelezwa rasmi mwaka 2012.

Unatarajiwa kuwa dira ya kuhakikisha utawala bora, uongozi wa sheria na haki, kuheshimu haki za binadamu, kufanya chaguzi huru na haki.

Aidha, unatumika kwenye masuala ya kuheshimu katiba na kudumisha demokrasia.

APRM na ACDEG zinatazamwa kama kifutio cha kufuta sifa mbaya za Afrika kama bara lililojaa giza, lenye watu wajinga, fukara, wagonjwa, madikteta na wala rushwa.

**HALI HALISI**

Hadi leo viongozi wa Afrika wanafanya wanavyotaka na si wote wana nia ya kujiingiza kwenye mkataba wa ACDEG, dira inayowaelekeza kufanya mageuzi ya kidemokrasia na kiuongozi.

Wengi ni 'mateja' wa urais wala hawako tayari kuondoka Ikulu, hawako tayari kusaini mkataba huo unaotaka kuipa Afrika sura mpya kiuchumi, kisiasa na kimaendeleo.

Kabla ya mkutano wa AU uliomalizika hivi karibuni, Azaki za Afrika pamoja na wadau na wanaharakati wa kufanikisha ajenda ya kuwa na Afrika Mpya, walikutana jijini Addis Ababa.

Walikutana kwa lengo la kuziwajibisha serikali za Afrika kutekeleza mkataba wa ACDEG ambao unalenga kuboresha demokrasia, kuhakikisha utawala bora, uongozi kwa misingi ya sheria, kuheshimu katiba na kuleta maendeleo barani humo.

> Hammad anasema wakati mkataba wa ACDEG unasuasua kusainiwa na kutekelezwa, viongozi wa Afrika wamekubaliana kumaliza migogoro ya kivita na kuanza kutekeleza mkataba wa kutokomeza matumizi ya bunduki Afrika mwaka 2020.



Rais Paul Kagame wa Rwanda (wa tatu kushoto), akikabidhi uenyekiti wa Umoja wa Afrika (AU), kwa Rais Abdel Fattah el Sisi wa Misri. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



Rais aliyemaliza muda wake DRC, Joseph Kabila (kushoto), akikabidhi kijiti kwa Rais wa sasa wa DRC, Felix Tshisekedi.

Tamko la pamoja la Azaki za Afrika linasema viongozi wanachelewa kusaini, kuridhia na kutekeleza mkataba huo wa Afrika wa Demokrasia, Uchaguzi na Uongozi Bora na kuzidi kuzorotesha amani na maendeleo barani hapa.

Asasi za kiraia zinaamini kuwa kama mkataba ungetekelezwa na mataifa yote 55 kusingekuwa na vurumai ambazo zinasababisha vifo vya Waafrika wanaodai haki zao na kupinga uongozi wa serikali zao.

Mkutano huo ulizishirikisha asasi zaidi ya 30 za Afrika zinazofanyakazi na Shirika la Kimataifa la Action Aid International na Action Aid Denmark kuhamasisha utekelezaji wa mkataba huo na kufuatilia matokeo yake.

Una wajumbe kutoka Zambia, Botswana, Zimbabwe, Sierra Leone, Ghana, Tanzania, Uganda na Nigeria.

"AA Denmark inafanyakazi na Azaki kuhamasisha serikali kutekeleza mkataba huo," anasema Mshauri wa Action Aid kuhusu masuala ya uhamasishaji barani Afrika, Buba Khan.

Khan anawaeleza wajumbe wa mkutano huo kuwa suala la kuwa na uongozi bora na utawala wa kisheria, kufanya uchaguzi kwa amani, uhuru na haki, lakini pia kuheshimu katiba ni mambo ambayo Azaki za Afrika zinataka yafanyike.

Asasi hizo ni Jukwaa la Azaki la Afrika Magharibi (West African Civil Society Forum (WACSOF), Jukwaa la Azaki za Afrika Mashariki (EACSOF) na za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC NGOs).

Lakini pia wadau wengine wa mataifa ya Afrika yanayoshirikiana na Action Aid yanahimiza utekelezaji wa mkataba huo na kuripoti mafanikio na changamoto zake kwenye Kamisheni ya AU ili kuwe na mabadiliko na mafanikio ya kiongozi.

**AU INASEMAJE?**

Kwa mujibu wa Balozi Salah Hamad, Ofisa wa Idara ya Masuala ya Siasa ya Kamisheni ya Umoja wa Afrika, inayosimamia utekelezaji wa ACDEG anasema kuna haja ya Azaki kushiriki na kuongeza bidii kwenye uhamasishaji wa utekelezaji wa mkataba huo.

Hamad anasema Azaki zishirikiane na watunga sera, sheria, wanasiasa wakiwamo wabunge, wanataaluma na wadau mbalimbali kuzishinikiza serikali kusaini, kuridhia na kutekeleza mkataba huo unaolenga kuiboresha Afrika.

"Mkataba huu uliozinduliwa Januari 2007 na kuanza kutekelezwa rasmi mwaka 2012 unaotarajiwa kuiunganisha Afrika kimaadili mema, ni jukwaa la pamoja la kushirikiana na kuendeleza demokrasia, kudumisha utawala bora, haki, misingi ya sheria na kuheshimu haki za binadamu," anasema Hamad na kuongeza:

"ACDEG itafanikisha kujenga bara lenye ustawi, amani tena lililounganishwa ili kupata Afrika ambayo wengi wanaitamani."

Balozi Hammad anakiri kuwa hali si ya kuridhisha Afrika kwamba kuna machafuko nchini Sudan, Togo, Zimbabwe na DRC ambako watu kadhaa walipoteza maisha kutokana na vurumai za kabla na baada ya uchaguzi.

Anaamini kuwa lilikuwa ni jukumu la ACDEG kurekebisha mambo hayo na kudhibiti ili yasitokee kama mkataba huo ungekuwa umeridhiwa na kutekelezwa.

Hammad anawaambia wajumbe wa mkutano wa Azaki za Afrika kuwa kukosekana kwa nia ya dhati na utayari wa wanasiasa wa kuusaini mkataba huo, kuuridhia na kutekeleza kumezidi kuitumbukiza Afrika kwenye majanga.

Majanga ya maandamano ya kupinga viongozi, ukiukaji wa haki za binadamu, vita dhidi ya uongozi na kama ambavyo imetokea nyumbani kwake nchini Sudan hivi karibuni na kusababisha waandamanaji zaidi ya 50 kuuawa na polisi.

Ni katika maandamano ya kupinga serikali kuongeza bei za bidhaa muhimu wakati wananchi hawana kazi, huduma muhimu za kijamii wala maisha bora.

"Mkataba huu wa Demokrasia, Uchaguzi na Utawala Bora umekuwa kitu kisichosainiwa, kisichoridhiwa wala kutumika, matokeo yake haujawahi kuwa na manufaa kwa wananchi wa Afrika," anasema na kuongeza:

"Na kwamba machafuko yanayotokea sasa yasingekuwapo iwapo wakuu wa Afrika wangekubali kufanyakazi pamoja na kutekeleza kile ambacho kwa kauli moja bara lao limekifanya na kuamua kuwa na mkataba ambao utaleta amani, ustawi na maendeleo kwa wananchi."

Hammad anasema wakati mkataba wa ACDEG unasuasua kusainiwa na kutekelezwa, viongozi wa Afrika wamekubaliana kumaliza migogoro ya kivita na kuanza kutekeleza mkataba wa kutokomeza matumizi ya bunduki Afrika mwaka 2020.

Lakini mwanadiplomasia huyo, anaonyesha wasiwasi kuwa imeshafika Februari 2019 na kwamba AU inabakiwa na miezi michache, hivyo huenda hilo halitawezekana.

Anasema Mpango huo utakuwa kwenye hatihati kutokana na uzoefu kuonyesha kuwa hata mikataba kama ACDEG inashindikana kutekelezwa na kuleta utimilifu wa kisiasa, sembuse huo wa kutokomeza silaha!

Ofisa wa Idara ya Siasa ya AU, Rizzan Nassuna, akitoa ufafanuzi zaidi anawaambia wadau wa mashirika ya kijamii kuwa hadi sasa ni mataifa 31 pekee kati ya 55 ambao ni wanachama wa AU yaliyoridhia mkataba huo.

"Nchi 18 zimeridhia na kusaini wakati mataifa sita ambayo ni Tanzania, Misri, Botswana, Eritrea, Libya na Morocco zimeupa kisogo, hazijausaini, kuuridhia wala kuutekeleza," anasema.



Rais wa Nigeria Muhammadu Buhari. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

## Uchaguzi Nigeria; Buhari awaonya wezi wa kura

RAIS wa Nigeria Muhammadu Buhari, anasema ameamuru Polisi na wanajeshi kutowahurumia watu watakaobainika kushiriki kwenye wizi wa kura katika kipindi hiki cha kuelekea siku ya upigaji wa kura kwa taifa hilo,

Hiyo ni kufuatia hatua ya kusogezwa mbele kwa wiki moja kwa uchaguzi huo.

Hata hivyo, Rais Buhari na upande upinzani kwa pamoja waliikosoa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ya nchi hiyo kwa kuahirisha shughuli ya upigaji kura na kudai kuwa tume ina mapungufu na kutaka uchunguzi ufanyike.

Pamoja na hayo, wakosoaji wa kisiasa nchini Nigeria wamepokea kwa hisia tofauti kauli hiyo ya Rais Buhari, wakidai kuwa yeye pia ni miongoni mwa wezi wa kura.

Tume ya Uchaguzi ya Nigeria pamoja kukosolewa, imejitetea kwamba hatua yao ya kusogeza mbele uchaguzi ilitokana na ugumu wa usambazaji wa vifaa kwa sababu ya ukubwa wa eneo la nchi hiyo.

Kauli hiyo ya Rais Buhari anayemaliza muda wake, imetolewa katika mkutano wa dharura wa chama chake uliofanyika jijini Abuja.

Akizungumza kwa msisitizo, Rais Buhari anasema kuwa yeyote atakayefanya jaribio la udanganyifu au fujo awe tayari kulipa gharama ikibidi ya uhai wake.

Chama kikuu cha upinzani nchini Nigeria cha PDP kinasema kauli ya Buhari ni sawa na kutoa kibali cha mauaji kwa raia wake.

**WASIWASI WA KUAHIRISHWA KWA UCHAGUZI WA NIGERIA**

Pamoja na kuwa, waangalizi wa uchaguzi hawakuwa na uhakika wa asilimia 100 kwamba uchaguzi huo utafanyika katika siku iliyopangwa awali kutokana na changamoto zilizokuwepo, lakini uamuzi wa tume umewatia wasiwasi.

Hata hivyo, kampeni zilisitishwa saa 24 kabla ya uchaguzi na baada ya kuahirishwa vyama vya siasa vilidhamiria kurudi kufanya kampeni tena.

Rais Buhari na mpinzani wake Atiku Abubakar walieleza kutoridhishwa kwao na hatua hiyo ya tume ya uchaguzi kusogeza mbele tarehe ya upigaji kura kwa madai ya kutokamilika kwa baadhi ya maandalizi muhimu.

Mwenyekiti wa tume ya uchaguzi Mahmood Yakubu, amedai kuwa kuchelewa kwa uchaguzi huo hakuhusiani na ushawishi wa kisiasa kwa namna yeyote.



Atiku Abubakar mpinzani mkubwa wa Rais Buhari

Waangalizi wa kimataifa katika uchaguzi mkuu huo uliosogezwa mbele wametoa wito kwa raia wa taifa hilo kuwa watulivu wakati maandalizi ya uchaguzi yakiendelea.

**BBC**



# NJELU KASAKA

## Mwanasiasa mkongwe aliyeibuka kivingine

■ **Aandika kitabu kinachohusu maisha yake, siasa na hoja ya Tanganyika**

**Na Mwandishi Wetu**

JINA la Njelu Kasaka si geni kwa watu wanaofuatilia masuala ya siasa za Tanzania. Hii ni kutokana na alivyopata umaarufu kutokana na kuwa mmoja wa wabunge walioibua hoja ya taifa kuwa na mfumo wa serikali tatu- kuundwa kwa serikali ya Tanganyika ndani ya Muungano.

Hoja hiyo ilipata mashiko na ushabiki mkubwa miongoni mwa Watanzania hasa ikizingatiwa kuwa katika kipindi hicho ndiyo kwanza Tanzania ilikuwa imeingia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa si zaidi ya mwaka mmoja.

Yako mambo mengi yaliyokuwa yakizungumzwa wakati huo wa kuibuka kwa wabunge waliojulikana kwa jina la G55 (kundi la wabunge 55) waliotia saini kutaka kuundwa kwa serikali ya Tanganyika.

Miongoni mwa mambo hayo ni wimbi la mabadiliko ya kisiasa lililoikumba dunia na kusababisha kusambaratika kwa Jamhuri ya Muungano wa Kisovieti wa Urusi (USSR), kumalizika kwa vita baridi kati ya nchi za kijamaa, zikiongozwa na Urusi na za kibepari, Marekani ikiwa kinara.

Mengine ni Zanzibar kujiunga na Jumuiya ya Kiislamu Duniani (OIC), kuibuka kwa wanasiasa kama Mchungaji Christopher Mtikila (marehemu), waliokuwa wakitaka kuwapo kwa Muungano wenye usawa kwa maana ya kuanzishwa kwa serikali ya Tanganyika, hivyo kuwa na serikali tatu.

Hayo ni baadhi ya mambo ambayo yalikuwa yakichagiza na kuwafanya baadhi ya Watanzania kuamini kuwa ndicho chanzo cha vuguvugu hilo ambalo lilimfanya mwasisi wa taifa la Tanzania na baadaye Tanzania, Mwalimu Julius Nyerere, kuingilia kati na hata kuwashambulia baadhi ya viongozi wa ngazi za juu serikalini kuwa wameshindwa kuizima hoja hiyo.

Kwa kuwa sababu zilizotajwa ndizo zilikuwa zikidhaniwa kuwa ni chanzo cha G55 kuibuka na kudai serikali ya Tanganyika, Njelu Kasaka aliyekuwa amesimama kidete katika suala hilo, ameibuka na kuweka mambo sawa juu ya chimbuko na mchakato wa jambo hilo.

**UKWELI WA MAMBO**

Mwanasiasa huyo, aliyekuwa mbunge wa Chunya kupitia CCM na baadaye Lupa baada ya majimbo kugawanywa na kuwa Lupa na Songwe, ameibuka na kuweka mambo sawa kupitia kitabu chake cha 'Njelu Kasaka- Maisha, Siasa na Hoja ya Tanganyika- G55".

Akizungumza na Nipashe hivi karibuni, mwanasiasa huyo ambaye ni msomi katika taaluma ya uchumi kilimo, alibainisha kuwa hadi kufikia kwa hatua ya kudai Tanganyika, yako mambo mengi yamewachisha na hata serikali ya wakati huo kupoteza mwelekeo.

Suala la kutaka kuundwa kwa serikali ya Tanganyika, mzizi wake ulikuwa Juni 29, 1999 alipokuwa akichangia bungeni hotuba ya Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais (wakati huo John Malecela).

"...suala la Muungano kama walivyosema wengine ni kubwa na tunapolijadili lazima tulijadili kwa kina, kwa uwazi na kuwa 'serious' (makini)na tusilete mzaha mzaha. Uhai wa taifa hili na hali yake baadaye unategemea sisi hapa tulipo (wabunge), hautegemei mtu mwingine na kwa hiyo ukileta mzaha mzaha wowote ni kwamba utawaharibia wale watakaokuja.

"Kwa hiyo, mimi nimesema ule mfumo wa serikali mbili katika Muungano wa nchi mbili umepitwa na wakati, haufai na tuondokane nao mapema iwezekanavyo. Kuna sababu zake za kimsingi ambazo zinaufanya huo mfumo uonekane haufai," alisema.

Katika kuweka misingi ya hoja yake hiyo, Kasaka alisema Muungano uliokuwapo wakati huo (hata sasa bado upo) ulikuwa unasababisha hali ya kutokutoa haki sawa kwa nchi shiriki katika Muungano.

> Pia anasema kitabu hicho kitakuwa rejea muhimu kwa vijana wanaotaka kuingia katika uongozi wa kisiasa na wasomi wanaotaka kujua historia ya karibuni ya siasa za Tanzania.

"Upande wa Zanzibar wamepewa uhuru wa kufanya mambo kama wanavyopenda katika nchi yao na papo hapo wamepewa tena uhuru wote kushiriki mambo ya (Tanzania) Bara. Sasa katika muundo wa nchi mbili ni kwamba nchi moja haijapewa haki inayostahili.

"...Sababu ya pili, kwa nini huu mfumo wa serikali mbili haufai... umefanya sehemu ya Tanganyika au Bara kama tunavyoiita ikose uongozi wa ndani...tunao uongozi wa Muungano tu lakini uongozi wa ndani hatuna kwa sabau viongozi tulio nao wamo katika Muungano hawana mahali ambapo wanakaa kama Bara au wanakaa kama Tanganyika," alisema.

Ili kuhakikisha haki inapatikana katika pande zote za Muungano, Kasaka katika mchango wake huo, alisema suluhisho ni kuwapo kwa serikali ya Tanganyika au Tanzania Bara. Pia alielezea kuwa hali ilikuwa imefikia pabaya baada ya Zanzibar kuanza kujiondoa kidogo kidogo katika masuala ya Muungano ikiwamo michezo.

Baada ya kueleza hayo, mijadala iliibuka katika duru za siasa za Tanzania vikiwamo vikao vya juu vya CCM ambavyo vilikuwa vikijaribu kulizima suala hilo kabla ya kupelekwa kwa hoja rasmi ya kuundwa kwa serikali ya Tanzania ndani ya Bunge.

Hatimaye Agosti 23, 1993 hoja ilifikishwa na kusomwa rasmi Bungeni? Nini kilitokea wakati wa kuwasilishwa kwa hoja hiyo?

Ni mambo gani hayo? Yote hayo yataelezewa katika mfululizo wa makala zitakazoendelea kwa lengo la kuwaelimisha Watanzania juu ya historia na matukio ya kisiasa kuhusu Muungano tangu kuasisiwa kwake.

**DIBAJI YA KITILA**

Waziri wa Maji, Profesa Kitila Mkumbo, ambaye ameandika dibaji ya kitabu hicho anaeleza kwa kinagaubaga kwamba hoja ya kuanzishwa kwa Tanganyika kiliweka historia katika siasa za Tanzania.

Profesa Kitila anaeleza kuwa ni hoja ambayo iliwafanya wabunge maarufu kama G55 kujitoa mhanga katika kudai serikali ya Tanganyika kwa kuwa wapo viongozi maarufu waliopata misukosuko kutokana na hoja kama hiyo.

Anawataja miongoni mwao kuwa ni aliyekuwa Makamu wa Rais wa Tanzania na Rais wa Zanzibar, Alhaj Aboud Jumbe Mwinyi, aliyelazimishwa kujiuzulu baada ya kuanza kuwa na mawazo ya serikali tatu. Mwingine ni aliyekuwa Mwanasheria Mkuu na Jaji Mkuu wa Zanzibar, Wolfgang Dourado, ambaye aliwekwa kizuizini kwa kuibua hoja ya serikali tatu.

"Kimsingi hoja hii haikuwa mpya miongoni mwa Watanzania. Kilichokuwa kipya ni ujasiri wa kuiwasilisha. Kabla ya hapo, kuzungumzia jambo la Muungano na hasa uwapo wa hoja ya Tanganyika ilikuwa kama mzimu na ilikuwa na gharama kubwa... Kwa hiyo kitendo cha Njelu Kasaka kuamua kuwasilisha hoja ya serikali tatu, tena ndani ya Bunge, kilikuwa cha ujasiri mkuu na cha kuvunja mwiko muhimu katika siasa za Tanzania," anasema Profesa Mkumbo.

Pia anasema kitabu hicho kitakuwa rejea muhimu kwa vijana wanaotaka kuingia katika uongozi wa kisiasa na wasomi wanaotaka kujua historia ya karibuni ya siasa za Tanzania.

**KASAKA NI NANI?**

Kasaka ambaye hivi karibuni alitimiza umri wa miaka 77 tangu kuzaliwa kwake, kabla ya kuwa Mbunge wa Chunya na baadaye Lupa mkoani Mbeya, alifanya kazi katika Benki ya CRDB wakati huo ilijulikana kama Benki ya Ushirika na Maendeleo Vijijini. Katika benki hiyo alishika nafasi mbalimbali ikiwamo Meneja wa Mkoa wa Iringa.

Msomi huo wa shahada ya uzamili katika Uchumi kilimo kutoka Chuo Kikuu cha Kentucky, Marekani, mwaka 1994 aliteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Kilimo, Mifugo na Ushirika, nafasi aliyoendelea nayo hadi mwaka 1998 alipoteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa wa Iringa na baadaye Tabora hadi mwaka 2000.

Katika kipindi cha ubunge mwaka 2002 hadi 2005, alikuwa Mwenyekiti wa kamati ya Kudumu ya Bunge ya Fedha na Uchumi. Katika kipindi hicho, ndipo lilipoibuka suala la ubinafsishaji wa NMB.

**• Nini kilitokea kabla na baada ya kuwasilishwa Bungeni kwa hoja ya Tanganyika? Usikose mfululizo wa makala hii Jumatano ijayo.**

# Brexit inapofunikwa kwa uhasama wa Ufaransa, Italia kuhatarisha EU

**Na Michael Eneza**

UHUSIANO kati ya Ufaransa na Italia umeingia katika hali ya kuzorota na hivyo kuanza kuwa tishio kwa Umoja wa Ulaya (EU), kwani ni mzozo wa kiitikadi wa kina uliochangiwa na kuendelea kupata mafanikio ya kisiasa kwa vikundi vya mrengo mkali wa kulia katika nchi hizo mbili.

Nchini Italia vikundi hivyo sasa vina wingi wa viti bungeni na kuongoza serikali kwa kushirikiana na baadhi ya vyama vikubwa vya siasa vya jadi, hali ambayo haijapata kutokea Ulaya tangu kumalizika kwa vita vikuu vya pili barani humo, mwaka 1945.

Nchini Ufaransa, kuna 'maandamano yasiyoisha' ambayo sasa yanakaribia wiki ya 15, yanayofanyika zaidi 'wikiendi.'

Kilichotokea ni kuwa Naibu Waziri Mkuu wa Italia, Luigi Di Maio akijitutumua kwa ajili ya wafuasi wake nchini Italia, alimtembelea kiongozi mmoja wa juu wa kundi la Vikoti vya Njano linaloratibu 'maandamano yasiyoisha' kutaka Rais Emmanuel Macron aondoke madarakani.

Hatua hiyo, ilimlazimisha Rais Macron kumrudisha nyumbani balozi wa Ufaransa nchini Italia, ambako wachunguzi wa habari wanasema hali hiyo ni wazi itaanza kuathiri uthabiti wa mahusiano ya kibiashara kati ya nchi hizo mbili, na kwa upande mwingine, Umoja wa Ulaya kwa jumla.

Ni hali ambayo inaweza hata kumsaidia Waziri Mkuu wa Uingereza Theresa May.

Ni mazingira ambako kanuni za uendeshaji wa umoja huo katika masuala ya fedha na kiuchumi, hasa viwango vya nakishi (pengo) la bajeti kwa Italia halafu Ufaransa na Ujerumani kwa upande mwingine ni sehemu ya vyanzo vya sokomoko linaloendelea.

Ni mazingira ambako usimamizi wa mifumo ya uchumi ili kulinda sarafu ya pamoja unaingia mashakani kutokana na kuwepo serikali ya 'uzalendo kichaa' nchini Italia, inayopinga umoja huo kusimamiwa kwa karibu na uhusiano maalum kati ya Ufaransa na Ujerumani.

Pia kuna tatizo la jinsi ya kukabiliana na uhamiaji haramu, ambako Italia ina serikali isiyotaka wahamiaji kabisa na Ufaransa inalalamika.

Kinachofanya hali hiyo isitabirike kwa EU ni kuwa Italia ni nchi ambayo muda wote iko katika mazingira ya uchaguzi, na washirika wake (vyama vinavyounda serikali hivi sasa) hawaelewani.



Rais wa Ufaransa, Emmanuel Macron.





Naibu Waziri Mkuu wa Italia, Luigi Di Maio

Kuzuka kwa mzozo huo kumetoa nafasi ya kujijenga kisiasa miongoni mwa makundi ya wafuasi wa 'uzalendo kichaa' nchini Italia, hata kuvuka mpaka na kuwakumbatia wanaofanya maandamano kila wiki kutaka serikali ya Macron iachie ngazi.

Mtandao wa habari na televisheni wa Booomberg unasema maafa yameanza kuonekana katika mahusiano ya kibiashara kati ya nchi hizo mbili na kuweka ulizo kwa mipango ya kuunganisha nchi za EU zaidi.

Baada ya kuwatembelea 'Yellow Vests' jijini Paris na kuchochea kuzorota kwa uhusiano kati ya nchi hizo mbili, Naibu Waziri Mkuu Di Maio amekaza uzi na kukataa kabisa kuunga mkono mradi wa kujenga njia ya treni ya mwendo kasi kati ya Turin na Lyon.

Yaani ni kutoka Kaskazini ya Italia hadi katikati ya Ufaransa, mradi ambao unatazamiwa kugharimu dola bilioni 10. Di Maio anasema waziwazi anadhani kuwa mradi huo ni upotevu wa fedha, na ingekuwa bora fedha hizo zitumike kujenga reli kuunganisha miji ya Italia, na si Italia na Ufaransa, mpangilio wa fikra ambao ni wazi hauendani na dhana ya utandawazi, kukuza biashara.

Di Maio aliliambia gazeti moja nchini Italia kuwa mradi huo hautatekelezwa, na chama chake cha Five Star Movement kiko serikalini, mazingira ambayo wachunguzi wa habari wanasema yanatokana na kuzorota kwa hali ya uchumi kwa wanachama wengi wa EU. Umoja huo sasa unaanza kuzingirwa na maadui zake, kwa mfano Russia imekuwa ikijitetea kuwa haijalamba midomo na kujipongeza kutokana na mtafaruku nchini Uingereza kuhusu kujitoa EU, ambao sasa unatazamiwa kufikiwa bila makubaliano yoyote.

Ni mazingira ambayo yanachochewa pia na utawala wa sasa wa Marekani, unaounga mkono 'uzalendo kichaa.'

Wakati mahusiano ya kijamii na kibiashara yakiwa yamejengeka kwa miaka mingi, ushindani na hisia nchini Italia kuwa kampuni za Ufaransa zimemeza nembo za Italia zenye sifa kwa kuzinunua katika soko na kuzigeuza za Kifaransa, kukuza ushirikiano ni kazi ngumu.

Wako raia wa Italia ambao wanaendelea kufungua biashara na kutafuta maisha mapya nchini Ufaransa na hali hii mpya imekuwa ni changamoto, wakisema ni aibu kwao wakifungua migahawa katika jiji la Paris yenye majina ya Kiitalia, vyakula vya Kiitaliana, na vinginevyo.

Mmoja kati ya wawekezaji hao alisema atalazimika kuomba radhi kwa wenyeji wake kuwa kitendo cha Di Maio hakimwakilishi yeye kama raia wa Italia na isingepasa Waitalia wasiruhusu kuingia katika uchokozaji wa wazi.

Hata hivyo, Italia bado inatafuta wapi imesimama kabla ya uchaguzi wa wajumbe wa Bunge la Umoja wa Ulaya mwezi Mei ambako manaibu mawaziri wakuu wawili, Di Maio na Matteo Salvini wanazozana kila uchao, licha ya kuwa wanatazamia kuwa itakuwa ni fursa nyingine ya kubomoka kwa hatua urasimu uliojijenga EU.

Kuhusu mpango wa ujenzi wa reli kasi kwa mfano, Ufaransa inataka ujenzi huo uendelee, ikiwa ni pamoja na kutoboa mlima kwa urefu wa kilometa 57 (maili 36) katika mkao wa milima ya Alps inayounganisha nchi za Italia, Ufaransa na Uswisi.

Salvini anaunga mkono mradi huo wakati Di Maio anaupinga, na wote wako serikalini, hali inayofanya Italia isiwe nchi yenye serikali inayoweza kuingia mikataba Ulaya halafu kuitekekeza.

Kati ya fedha zinazotazamiwa kujenga reli kasi hiyo, kiasi cha euro milioni 800 (dola 909 milioni) zilishapitishwa na Umoja wa Ulaya kutumika katika mradi huo, ambao kwa wapenzi wa michezo ungewezesha mashabiki wa timu zozote kati ya nchi hizo kwenda kuhudhuria mechi bila kuwa safarini, kwa mfano mechi zikichezwa nyakati za usiku baada ya kazi.

Treni za mwendo kasi zinachukua saa moja kumaliza kilomita 300 ambao ni karibu na umbali wa Turin kwenda Lyon, na saa moja nyingine shabiki angefika Paris, na saa tatu, angeingia Ujerumani.

Ila wanasiasa wa 'uzalendo kichaa' wanaona miradi hiyo inaongeza ustawishaji wa biashara za nje nchini kwao.

Baadhi ya wachunguzi wa habari na wataalamu wa uchumi wanaona mahusiano ya kina kati ya mkasa wa madeni ya Ugiriki na jinsi EU ilivyopata shida kumaliza tatizo hilo bila kuiondoa nchi hiyo katika umoja huo na hali inavyojengeka nchini Italia.

Kuna wasiwasi miongoni mwa baadhi ya wafuatiliaji wa masuala ya uchumi kuwa uchumi wa Italia unaweza kuingia katika mkwamo na hisa katika masoko yake ya fedha zianze kuuzwa kwa kasi, ambako baadhi ya benki kubwa za Ufaransa kama BNP Paribas na Credit Agricole zingeathirika.

Hata hivyo, baadhi ya wachunguzi wanaona mshikemshike wa aina hiyo unaweza pia kuiingiza Italia katika mikono ya wanunuzi hisa kutoka nje wenye fedha za ziada, wakati amana zake zikipungua thamani.

MAKALA

# Mvutano wa mpaka unavyotishia uhusiano kati ya Kenya na Somalia

SOMALIA imekanusha tuhuma kwamba imenadi maeneo ya mafuta yaliopo katika mpaka unaozozaniwa kati ya taifa hilo na Kenya.

Katika taarifa yake Jumapili iliyopita, serikali ya Somalia imesema 'haina mipango wala haikuwa na mipango ya kufanya hivyo'.

Taarifa hiyo ilitolewa baada ya kuwepo ripoti za kikao kilichofanyika katika mji mkuu Mogadishu cha maafisa wakuu serikalini, akiwamo rais mwenyewe Mohamed Abdullahi Mohamed Farmajo na Waziri Mkuu, Hassan Ali Khayre.

"Somalia kwa sasa haina mpango wala haikuwa na mpango wa kunadi sehemu yoyote katika eneo linalo zozaniwa baharini hadi pale mahakama ya ICJ itakapobaini mipaka ya nchi husika," imeeleza taaifa hiyo rasmi.

Imetoa ahadi kwa Kenya kuwa haitojihusisha katika shughuli zozote katika maeneo yalio kwenye mzozo hadi mahakama itakapotoa uamuzi wa mwisho.


Siku ya Jumamosi jioni, Nairobi ilitangaza kuwa inamrudisha balozi wake aliyeko Mogadishu, Luteni Jenerali mstaafu Lucas Tumbo, ikidai kuwa uamuzi wa Somalia kupiga mnada eneo moja la mafuta mjini London wiki iliyopita ni sawa na uchokozi dhidi yake na maliasili yake.

Vilevile Nairobi ilimrudisha nyumbani balozi wa Somalia nchini Kenya Mohamed Nur katika kile ambacho serikali ya Kenya baadaye ilifafanua kwenye vyombo vya habari nchini kuwa ni kutoa fursa ya majadiliano ya kila upande katika suala hilo.

"Kwa kupuuza suluhu ya sheria za kimataifa kuhusu mipaka ama makubaliano ya kisiasa kupitia diplomasia, serikali ya Somalia imeonyesha wazi bado haijakomaa kisiasa" , amesema katibu wa masuala ya kigeni nchini Kenya, Macharia Kamau.

Somalia kupitia wizara ya mambo ya nje, imeelezea masikitiko yake kufuatia hatua hiyo ya Kenya kumrudisha balozi wake pasi kuwepo mashauriano.

> Katika kesi yake, Somalia inataka mahakama hiyo ya Hague kutoa uamuzi kuhusu eneo hilo linalogawanya Kenya na Somalia katika bahari Hindi, ikiwa ni pamoja na eneo la bara lenye zaidi ya maili 200.




Chanzo: International Court of Justice (ICJ) BBC

**MAMBO 3 HATARI KWA MVUTANO HUU:**

Kumeshuhudiwa mvutano na malumbano kuhusu mipaka baina ya mataifa hayo mawili katika siku za nyuma. Baadhi ya wachambuzi wanaona kwamba hili ni jambo lisilohitajika kwa sasa.

Na huenda ni jambo ambalo mataifa yote mawili yanalitambua kutokana pia na kauli ya Somalia kwenye taarifa yake Jumapili iliyopita ya kukanusha madai hayo ya kupiga mnada mafuta na gesi katika eneo hilo linalozozaniwa, kwa kukiri kwamba 'mataifa hayo "yameshikana katika namna ambayo hayawezi kuvunjika" na kuwa yana uhusiano mzito wa kihistoria na kitamaduni, ambayo Somalia haitaki kuuvunja.

Kwa jumla, ni mataifa yanayotegemeana. Mchambuzi wa masuala ya Afrika, Ibrahim Aidid, anasema Kenya na Somalia ni mataifa ambayo yameweza kufanya vitu vingi kwa pamoja na kwa ushirikiano mkubwa.

Mataifa hayo mawili yamekuwa yakishirikiana katika masuala ya:

**USALAMA:**

Kenya inategemea ushirikiano mkubwa kutoka Somalia katika vita dhidi ya ugaidi, hususan dhidi ya kundi la wapiganaji wa Alshabaab, ambalo ni tishio sio tu kwa mataifa hayo mawili, lakini pia kieneo.

Wanajeshi wa Kenya pamoja na wanajeshi kutoka mataifa mengine kama Djibouti, Uganda na Ethiopia, chini ya mwamvuli wa kikosi cha kulinda amani - Amisom, wamekuwa wakiisaidia serikali ya Somalia katika vita hivyo.

Wanajeshi wa Kenya waliingia Somalia mnamo mwaka 2011, kuwapiga vita wanamgambo wenye uhusiano na mtandao wa al-Qaeda.

**BIASHARA:**

'Kenya inapeleka biashara Somalia. Imenufaika viivyo kifedha kwa bidhaa, kwa mfano miraa zinazosafirishwa hadi Somalia', anasema mchambuzi wa kisiasa, Ibrahim.

Usafirishaji wa miraa au mirungi hadi Mogadishu, ni biashara inayokisiwa kuwa na thamani ya karibu dola nusu milioni kila siku. 'Somalia kwa upande wake, inanufaika kwa biashara ya samaki wanaoingizwa Kenya' anasema Ibrahim.

**UHAMIAJI:**

Maelfu ya wakimbizi kutoka Somalia wamehifadhiwa katika mojawapo ya kambi kubwa duniani ya Daadab iliyopo nchini Kenya.

Kambi hiyo ya Dadaab ilijengwa mnamo 1991 kuzihifadhi familia za jamii zilizokuwa zinatoroka mzozo nchini Somalia, na baadhi ya watu wamekuwa wakiishi hapo kwa zaidi ya miaka 20.

Somalia inaitazama Kenya kama mshirika wake mkuu katika kufanya mageuzi ndani ya nchi hiyo.

Na huenda ndiyo mambo yanayostahili kupewa uzito kwa Rais Mohammed Abdullahi Farmajo na Rais Uhuru Kenyatta wanapotathmini na kutafuta suluhu kwa mvutano uliopo sasa, anasema mchambuzi Ibrahim.

Kiini cha mgogoro huo, ni eneo lililopo ndani ya bahari Hindi lenye ukubwa wa mraba maili 62,000. Haijulikani ni taifa gani linalomiliki eneo hilo lakini linaaminika kumiliki kiwango cha juu cha mafuta na gesi.

**UCHIMBAJI:**

Kenya inasisitiza kwamba mpaka huo unakwenda sambamba na laini ya latitude na tayari ilikuwa imeuza leseni za uchimbaji mafuta kwa makampuni ya uchimbaji madini katika eneo hilo kabla ya mzozo huo kuchipuka.

Katikati ya mgongano huo ni visima vya mafuta vilivyopewa kampuni za kigeni kwa muda.

Kenya sasa imedai kwamba uchimbaji wa mafuta katika eneo hilo umesimamishwa kwa muda kama ishara ya uhusiano mwema, lakini Somalia inasisitiza kuwa hiyo haitoshi.

Somalia vilevile inasisitiza kuwa mpaka wake unafaa kuwa sambamba na mpaka wake wa kusini.

Suala hilo liliwasilishwa katika mahakama ya kimataifa ya haki, ICJ mnamo mwezi Aprili 2014 baada ya majadiliano kugonga mwamba.

Kenya ilikuwa imepoteza kesi hiyo hapo awali na kulazimika kuwasilisha kesi yenye uzito mkubwa.

Wataalam wa baharini hapo awali wameonya kwamba Kenya huenda ikapoteza kesi nzima iwapo uamuzi wa hapo awali utarudiwa.

Hata hivyo, Kenya iliendelea na suala hilo huku aliyekuwa Jaji Mkuu, Githu Muigai akiliwakilisha taifa hilo mbele ya mahakama ya mjini Hague.

**VISIMA VYENYE MZOZO:**

Iwapo Kenya itapoteza kesi hiyo, basi italazimika kuwachilia visima vyake vitatu kati ya 20 katika bahari ya hindi kwa Somalia.

Visima vyenye mzozo ni L-21, L-23 na L-24 . Suala nyeti la mgogoro huo kati ya Kenya na Somalia ni alama ya mpaka wa baharini.

Huku Somalia ikisisitiza kuwa alama hiyo ya Mpaka inapita katikati katika mpaka wa Kenya na Somalia, Kenya inasisitiza kuwa mstari huo unafaa kuwa sawa.

Mstari wa mpaka wa Somalia unaonyesha eneo lenye pembe tatu la baharini ambalo linamilikiwa na Kenya na ambako visima hivyo vitatu vipo.

Nakala za mahakamani zilizowasilishwa zinaonyesha kuwa visima hivyo vitatu vilivyopo katika eneo hilo la pembe tatu vilipewa kampuni moja ya Kitaliano na serikali ya Kenya.

Katika kesi yake, Somalia inataka mahakama hiyo ya Hague kutoa uamuzi kuhusu eneo hilo linalogawanya Kenya na Somalia katika bahari Hindi, ikiwa ni pamoja na eneo la bara lenye zaidi ya maili 200.

Kenya nayo inasema kuwa makubaliano ya 2009 yalikuwa yamependekeza kwamba uamuzi wa mwisho wa kesi hiyo utafanyika baada ya kamishna wa UN kuhusu mipaka ya bara Afrika kuonyesha kiwango cha mpaka huo. **BBC**.





# Mauaji Njombe yamwibua Sugu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MBUNGE wa Mbeya Mjini, Joseph Mbilinyi 'Sugu', ameshauri uchunguzi wa kitaalamu ufanyike ili kuwabaini watuhumiwa wa mauaji ya watoto mkoani Njombe.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake 'Sugu' alisema ili kuwabaini wahutumiwa, kikosi maalum vikiwamo na vyombo vya dola watumie taaluma zao vyema kufanya uchunguzi wa kina bila shinikizo na mtu kuwamata wahusika.

"Hii kamatakamata ya watu bila ushahidi wowote haiwezi kuzaa matunda ya kukomesha vitendo hivyo vya mauaji dhidi ya watoto wetu, nashauri timu iliyoundwa ifanye uchunguzi wa kina kabla ya kukamata wanaoshukiwa itasaidia," alisema.

Aliongeza kuwa serikali na wadau wengine waongeze nguvu mkoani Njombe na kuhakikisha chanzo cha vitendo hivyo kinabainika.

Kuhusu vitendo hivyo kuhusishwa na imani za kishirikina kuelekea uchaguzi, Mbunge huyo alisema hakuna uhakika.

Alisema kama kweli wanasiasa wanahusishwa na mauaji hayo wakamatwe na kuchukuliwa hatua na kwamba mwanasiasa bora ni yule anayekubalika kwa utekelezaji wa shughuli za maendeleo.

"Kama mwanasiasa yeyote anahusika na mauaji ya watoto Njombe huyo ni mshamba kwa nini uamini ushirikina kwamba utakubalika badala ya kuchapa kazi walaaniwe," alisema 'Sugu'.

Hata hivyo, jaribio la vitendo vya ubakaji kwa watoto vimeripotiwa katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, ambapo watoto wanne katika kipindi cha mwezi Februari mwaka huu walinusurika kubakwa.

Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kata ya Nsalala, Felister Kaisi, alisema uongozi wa serikali ya kata uunde ulinzi shirikishi katika kila kitongoji ili kudhibiti vitendo hivyo.

Alisema ulinzi huo utasaidia kuwatambua wananchi ambao wanatiliwa shaka na kuhojiwa katika maeneo yao kwa kuwa wanafahamiana.

# Mpango, Kairuki wajitosa changamoto parachichi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philipo Mpango na Waziri wa Ofisi ya Waziri Mkuu-Uwekezaji, Angela Kairuki, wameanza kutekeleza agizo la Rais John Magufuli la kuhakikisha wanatatua changamoto za wakulima na wawekezaji wa maparachichi nchini.

Mawaziri hao pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), Godfrey Mwambe, waliwasili mkoani Mbeya juzi na kuzungumza na baadhi ya viongozi wa mkoa huo pamoja na wakulima wa maparachichi wa Wilaya ya Rungwe.

Waziri Mpango ambaye ndiye Mwenyekiti wa msafara huo, alisema serikali inataka kuimarisha sekta ya kilimo ambayo inaenda sambamba na maendeleo ya kilimo kinachozalisha malighafi kwa ajili ya viwanda hivyo.

Alisema ili kuhakikisha wakulima wa maparachichi wanazalisha kwa tija, ni lazima kuwapo na uwekezaji ikiwamo ujenzi wa maghala ya kisasa, zana bora za kilimo pamoja na kuwatafutia wakulima masoko ya kimataifa.

**Wilaya ya Mbarali ambayo inazalisha zaidi maparachichi pia inazalisha mazao mengine kama ndizi, viazi, kahawa na chai ambayo yanahitaji uwekezaji mkubwa ili uzalishaji wake uwe na tija zaidi.**

"Maparachichi ni miongoni mwa mazao ya kimkakati ambayo tunatakiwa kuimarisha uzalishaji wake, Rais alipoonana na wakulima pamoja na wawekezaji mwaka jana alipata malalamiko ya wakulima wa zao hili na akatuagiza tuje tuwasikilize na kuzitatua ndio maana tumekuja," alisema Dk. Mpango.

Alisisitiza kuwa nafasi ya kilimo nchini ni kubwa kwa madai kuwa zaidi ya theluthi mbili ya Watanzania wanategemea kilimo na kwamba kilimo ndicho kinazalisha chakula kwa asilimia kubwa zaidi kuliko sekta nyingine.

Mkuu wa Mkoa huo, Albert Chalamila, alisema mbali na kilimo cha maparachichi pia kuna mazao mengine ambayo yanahitaji uwekezaji ili yalete tija kwa wakulima.

Alisema mkoa huo ni miongoni mwa mikoa ukanda maalumu wa kilimo kwa madai kuwa kila wilaya ina zao lake ambalo inajivunia na kuzalisha kwa wingi.

Alisema Wilaya ya Mbarali ambayo inazalisha zaidi maparachichi pia inazalisha mazao mengine kama ndizi, viazi, kahawa na chai ambayo yanahitaji uwekezaji mkubwa ili uzalishaji wake uwe na tija zaidi.

Pia alisema mkoa huo ni miongoni mwa mikoa inayozalisha zao la pareto kwa wingi na kwa ubora, hivyo akaomba pia zao hilo liangaliwe vizuri ili lizalishwe kwa tija.

Alisema zao hilo linalimwa zaidi katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambako alisema inazalishwa pareto yenye viwango vizuri kuliko maeneo mengine nchini.

Mkurugenzi wa TIC, Mwambe alisema watahakikisha wakulima wa zao la parachichi wanazalisha kwa tija na wanafaidika na kilimo hicho huku serikali nayo ikikusanya kodi.

Alisema lengo la TIC ni kuifanya Tanzania kuwa nchi inayoongoza duniani katika uzalishaji wa parachichi na kulitumia zao hilo kama ajira kubwa hasa kwa vijana.



Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango (mwenye tai), akipokelewa na viongozi wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) tawi la Mbeya, alipohudhuria mkutano kati ya serikali, wawekezaji na wakulima wa zao la parachichi juzi. Wapili kulia ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angela Kairuki na (kulia) ni Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Albert Chalamila. **PICHA: WFM**

# Wachimbaji waandamana kumpa tano JPM

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

WACHIMBAJI wadogo wa madini ya dhahabu kutoka maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Chunya, wameandamana mpaka katika Ofisi ya Mkuu wa Wilaya hiyo kwa ajili ya kuwasilisha shukurani zao kwa Rais John Magufuli kufuatia baadhi ya kodi ambazo zilikuwa kero kwao.

Waliandamana juzi na kupokelewa na Mkuu wa Wilaya hiyo, Maryprisca Mahundi.

Walimshukuru Rais kutokana na kuonyesha kwa vitendo ahadi zake za kuwajali wananchi hasa wanyonge wakiwamo na wao ambao kwa muda mrefu walikuwa wanateseka.

Mwenyekiti wa wachimbaji wadogo wa Mkoa wa Mbeya, Leonard Manyesha, alisema kutokana na kitendo hicho alichokifanya Rais, wako tayari kuhakikisha maelekezo yote aliyoyatoa alipokutana na wachimbaji jijini Dar es Salaam yanatekelezwa.

"Tumekuwa tukichimba madini, lakini faida hakuna kutokana na mrundikano wa kodi, sasa Rais wetu ametusikia na ameamua kutuondolea kodi hizo, hatuna uwezo wa kuandamana kwenda Dar es Salaam, hivyo tumeona tufikishe salamu zetu kupitia kwa Mkuu wa Mkoa," alisema Manyesha.

Naye Gerge Mtasha alisema watahakikisha wanaitumia vema fursa waliyopewa na serikali ili kuhakikisha wananufaika na madini wanayochimba wilayani humo.

Aliwashauri wachimbaji wote nchini kumuunga mkono Rais Magufuli ili aweze kutekeleza majukumu yake vizuri kwa madai kuwa anafanya kwa vitendo kila linalotakiwa kufanyika.

Mbunge wa Jimbo la Lupa, Victor Mwambalaswa, alisema lengo la Bunge kupitisha sheria mpya ya madini ni kutaka wachimbaji wadogo wanufaike na kazi zao hivyo akawataka watumie vizuri fursa hiyo.

Alisema kitendo cha Serikali ya Wilaya hiyo kutaka kuanzisha soko la madini wilayani humo kitasaidia kukuza uchumi wa wananchi wa wilaya hiyo kwa madai fedha zote zitakuwa zinabakia ndani ya wilaya hiyo.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Sophia Kumbuli, alisema marekebisho hayo ya sheria ya madini yataisaidia pia halmashauri yake kuongeza ukusanyaji wa mapato.

Alisema wachimbaji hao watanufaika mara mbili kwa kuongeza kipato chao na kunufaika na miradi ya maendeleo itakayokuwa inatekelezwa kutokana na makusanyo ya kodi hizo za madini.

DC Mahundi aliwataka wachimbaji hao kuhakikisha hawaharibu mazingira kwenye maeneo wanayochimba ili kuihakikishia serikali kuwa fursa hiyo waliyoipata wanaitumia vizuri.



# Uhaba maji wakimbiza watumishi Chamwino

**Na Augusta Njoji,** CHAMWINO

IMEELEZWA kuwa baadhi ya watumishi wa Zahanati ya Ikowa wilayani Chamwino, wamelazimika kukimbia kituo chao cha kazi kutokana na uhaba wa maji.

Hali hiyo imesababisha Zahanati hiyo kuwa na mhudumu mmoja kwa sasa ambaye naye anaishi mbali na kituo hicho.

Hali hiyo ilibainika juzi wakati wa ziara ya Mbunge wa Jimbo la Chilonwa Joel Mwaka, alipotembelea vijiji vya Mulebe, Ikowa, Makoja na Msalamalo akiongozana na Mhandisi wa Maji wa Wilaya ya Chamwino, Godfrey Mbabaye.

Wananchi wa kijiji cha Ikowa walimwambia Mbunge huyo kuwa hali ya maji katika kijiji chao ni mbaya na yanapatikana kwa gharama kubwa.

**Naomba muwe wavumilivu tunalifanyia kazi tatizo hili lakini nasikitika kwamba mwekezaji angesaidia kuuza maji aliyochimba kwa gharama watakayomudu wananchi.**

Mmoja wa wananchi hao, Samweli Mtembwele, alisema kwa muda mrefu wanakabiliwa na tatizo hilo hali iliyosababisha watumishi wa serikali kuanza kukimbia ikiwemo wa zahanati hiyo.

"Tunavyozungumza watumishi wawili wa zahanati wameshakimbia na tumebakiwa na mmoja ambaye anaishi mbali na hapa kwenye eneo lenye huduma ya maji hivyo ukienda usiku unakutana na mlinzi tu, tunaomba serikali iingilie kati suala hili," alisema Mtembwele

Naye Mjumbe wa Serikali ya kijiji, Rosemary Mbezi alisema kuna mkandarasi ambaye amechimba kisima katika eneo hilo lakini anauza maji kwa Sh. 200 kwa ndoo yenye ujazo wa lita 20.

Mbezi alisema kwa maisha ya kawaida familia moja inatumia Sh 2,000 kwa siku ili kupata maji ambayo ni sawa na Sh. 60,000 kwa mwezi na kwamba ni vigumu wananchi wa kawaida kumudu gharama hizo.

"Wanawake ndiyo waathirika zaidi kwani hawapati maji na hata zahanati wanatakiwa kwenda na maji wanapoenda kujifungua,"alisema.

Akizungumzia hali hiyo, Mbunge Mwaka aliwaomba wananchi kuwa watulivu ili afikishe kilio chao kwa wahusika.

"Naomba muwe wavumilivu tunalifanyia kazi tatizo hili lakini nasikitika kwamba mwekezaji angesaidia kuuza maji aliyochimba kwa gharama watakayomudu wananchi,"alisema.

Katika ziara yake, Mwaka alisema wakati wowote kuanzia sasa wataalamu wataanza kuchimba kisima katika eneo Msalamalo ambalo walibaini kuna maji ya kutosha.



Mafundi wakiwa katika ujenzi wa vyumba vya madarasa katika Shule ya Msingi Busungu unaofanywa na wanakijiji kwa kushirikiana na serikali Musoma Vijijini mkoani Mara juzi, ili kupunguza mlundikano wa wanafunzi madarasani. **NA MPIGA PICHA WETU**

# Samia apigia debe viongozi waaminifu

**Na Elisante John,** SINGIDA

MAKAMU wa Rais, Samia Suluhu Hassan, amewataka Watanzania kutumia vyema fursa ya uchaguzi kwa kupata viongozi bora, waaminifu na weledi katika kusimamia mali za umma ili waharakishe maendeleo yaliyokusudiwa.

Alitoa rai hiyo kwenye ziara yake ya siku tano mkoani Singida alipokuwa akikagua ukarabati mkubwa wa Kituo cha afya Sokoine katika Manispaa ya Singida.

Alisema kupatikana kwa viongozi bora na wenye uchungu na taifa lao, kutachochea maendeleo ya wananchi kwenye miradi mbalimbali.

Ujenzi huo uliogharimu Sh. milioni 500 ambapo miongoni mwa majengo yaliyojengwa ni jengo la upasuaji.

Akizungumza katika ukaguzi wa miradi, Makamu wa Rais aliwaasa Watanzania kutumia vyema fursa hiyo kuchagua viongozi makini.

Aidha, alipongeza usimamizi bora wa fedha zilizotumika katika kutekeleza kazi hiyo na kutoa rai kwa halmashauri nyingine nchini kuiga mfano huo.

Awali, Mkurugenzi wa Huduma za Afya wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Dk. Ntuli Kapologwe, alisema mkakati wa Serikali ni kuboresha zaidi sekta ya afya kwa kujenga vituo vya kutosha vya kutolea huduma ya afya nchini.

Naye Naibu Waziri wa Ujenzi Elias Kwandikwa, alisema mkakati wa Serikali ya awamu ya tano ni kuhakikisha inaboresha barabara zote zinazoingia na kutoka katika Mkoa wa Singida.

Alisema serikali inatarajia kujenga barabara za kuchepuka nje ya mji wa Singida, ili kurahisisha mawasiliano kwa magari makubwa na abiria wanaohitaji kupitiliza moja kwa moja bila kulazimika kuingia katikati ya Manispaa hiyo.

Kadhalika, Meneja wa Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) Manispaa ya Singida, Mhandisi Lambert Bayona, alisema barabara ya Karume yenye urefu wa kilomita 6.5, iliyofadhiliwa na Benki ya Dunia imegharimu zaidi ya Sh. Bilioni 10.5.

# Ugonjwa wa macho wawatesa wakazi wa Dodoma

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

UGONJWA wa mtoto wa jicho na trakoma umetajwa kuwatesa kwa kiasi kikubwa wakazi wa Mkoa wa Dodoma huku chanzo chake kikitajwa kuwa ni kutoosha nyuso zao kutokana na uhaba wa maji.

Kufuatia hali hiyo, madaktari bingwa wa macho kutoka Marekani wamepiga kambi katika Hospitali ya Benjamin Mkapa iliyopo Chuo Kikuu cha Dodoma ili kutoa huduma ya matibabu ya macho na wanatarajia kuwafanyia upasuaji wa magonjwa hayo watu zaidi ya 400.

Hayo yalisemwa jana na daktari bingwa wa hospitali hiyo, Dk. Frank Sandi alipokuwa akizungumzia kuhusu kambi hiyo.

Alisema katika upasuaji wa macho uliofanyika, wakazi wengi wa Mkoa wa Dodoma wamebainika kusumbuliwa na matatizo hayo kutokana na kuugua mara kwa mara na sababu kubwa ni uhaba wa maji safi na salama.

Alisema kuwa tatizo la macho ni kubwa mkoani humo na limetokana na uhaba wa maji huko kwani zamani walikuwa hawana kawaida ya kuosha nyuso.

"Ndiyo sababu wengine wamepata ugonjwa wa vikope (trakoma) na imewasumbua sana watu wa Dodoma lakini sasa hivi maji yanapatikana ugonjwa unapungua lakini unaokuja kwa kasi sasa ni mtoto wa jicho,"alisema.

Alisema kwenye kambi hiyo waliyoifanya, asilimia 30 ya wagonjwa wamebainika wana ugonjwa wa mtoto wa jicho.

"Katika kuchunguza wagonjwa kuna magonjwa mengi, pamoja na hayo mengine kuna ugonjwa wa kutoona vizuri na majeraha kwenye macho inatokana na kurukiwa na vitu kwenye macho," alisema na kuongeza.

"Tuko hapa kwa ajili ya kutoa huduma za macho kwa wananchi ambao wapo kwenye mazingira ambayo hawafikiwi kirahisi na tunatoa huduma hii kwa kushirikiana na wadau kutoka Marekani na tunafanya huduma hii kila mwaka,"alisema.

Alisema lengo ni kuwafikia wagonjwa 1,500 kwaajili ya kuchunguzwa na watakaofanyiwa upasuaji ni wagonjwa 400 kwa kambi hiyo.

"Hadi sasa wagonjwa 150 wamefanyiwa upasuaji na hospitali inaendelea kutoa huduma za macho hivyo wananchi wajitokeze kupata huduma,"alisema.

Naye, Mkazi wa Chimendeli Marta Tuguti(110) alishukuru hospitali hiyo kwa kutoa huduma hiyo na kusema kuwa alikuwa haoni lakini kwasasa anaona.





# Marufuku uhamishaji holela watumishi ZBC

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Habari, Utalii na Mambo ya Kale, Mahmoud Thabit Kombo, amepiga marufuku uhamisho wa wafanyakazi kiholela wa Shirika la Utangazaji la Zanzibar (ZBC).

Kombo alitangaza marufuku hiyo wakati akijibu hoja za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliokuwa wakichangia ripoti ya Kamati ya Habari na Utalii ya Baraza la Wawakilishi.

Alisema yapo malalamiko ya watumishi wengi wa ZBC kuhamishwa kiholela na mkurugenzi wake, hivyo kusababisha malalamiko mengi.

"Mheshimiwa Spika, natangaza kuanzia sasa napiga marufuku uhamisho wa wafanyakazi wa ZBC... wale waliohamishwa awali sawa, lakini kwa sasa hapana," alisema.

Alieleza kwamba mtumishi wa idara au taasisi anaweza kuhamishwa kwenda sehemu nyingine, lakini kwanza anapaswa kujulishwa na kujua sababu za kuhamishwa kwake.

Baadhi ya wajumbe wa Baraza la Wawakilishi waliochangia ripoti hiyo, walisikitishwa na matukio ya kuhamishwa ovyo kwa wafanyakazi wa shirika hilo.

Mwakilishi wa Jimbo la Shauri Moyo, Hamza Hassan Juma, alisema matukio ya uhamisho holela yanayofanywa na Mkurugenzi wa ZBC yanavunja moyo watumishi wake na kuwatia hofu wengine.

Alisema watumishi wanatakiwa wajengwe kwa ari na moyo wa utumishi kwa ajili ya kuleta ufanisi wenye tija.

"Mheshimiwa Spika, tunataka tupewe sababu kwa nini mkurugenzi huyu amekuwa akihamisha wafanyakazi wake kiholela, huku akiomba serikali kuajiri wengine," alisema.

Mwakilishi wa Viti Maalumu, Panya Ali Abdalla, alisema wakati umefika kwa serikali kuliimarisha shirika ili matangazo yake yaweze kusikika vizuri nchini kote kwa faida ya wananchi.

"Shirika la habari la taifa ndiyo mdomo wa serikali, kwa hivyo tunaiomba serikali kulipatia fedha za kutosha ili liweze kutekeleza majukumu yake kikamilifu," alisema.

# Shein aeleza sababu uhaba wa mchanga

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amewataka wananchi watambue kuwa kuna uhaba mkubwa wa mchanga, na hali hiyo inasababishwa na uchimbaji mbaya wa rasilimali hiyo.

Dk. Shein aliyasema hayo jana katika ziara yake ya Wilaya ya Kaskazini'B' Unguja ya kutembelea maeneo yanayochimbwa mchanga huko Pangatupu, Chechele na Kiombamvua na kujionea jinsi maeneo hayo yalivyoathirika kutokana na rasilimali hiyo kuanza kumalizika kabisa.

Akiwa katika maeneo ya Pangatupu na Chechele, Dk. Shein, alieleza kuwa rasilimali ya mchanga Zanzibar imeanza kutoweka, hivyo kuna haja ya kuweka mikakati maalum ya kunusuru uliobakia, na kwamba serikali imeshaanza kazi hiyo.

Alisema serikali imeanza kuchukua hatua, ingawa hatua hizo hazina lengo la kuwakomoa wananchi, bali kuhakikisha rasilimali hizo zinawasaidia wananchi wote.

**Baada ya serikali kuanza kuchukua hatua kuanzia Machi na Novemba mwaka 2017, baadhi ya watu walianza kulalamika kuwa serikali inachukua mchanga wao.**

Alisema kuna wafanyabiashara wameshahodhi mchanga katika maeneo yao ya biashara hasa wale wanaofanya biashara ya tofali na kuwa wameuficha mchanga kwenye maeneo yao, hivyo kuwasababishia usumbufu wananchi wanaotaka kujenga.

Akizungumzia biashara ya mchanga, udongo, mawe na kifusi ulivyokuwa zamani, Dk. Shein alisema kuna tofauti kubwa kati ya sasa na miaka ya nyuma, kwa kuwa sasa taratibu hazifuati na ndiyo sababu ya uhaba huo.

Alisema katika shimo la mchanga la Pangatupu karibu mchanga umeisha, zimebaki tani 50,000 ambazo haufiki hata miezi miwili na kuongeza kuwa mchanga wa Chechele nao umebaki tani 2,000 tu ambao umehifadhiwa kwa ajili ya miradi ya serikali.

Alisema jengo la Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), limesitisha ujenzi wake kutokana na ukosefu wa mchanga na kusababisha mafundi wa ujenzi kutoka kampuni ya Hainan International kutoka China kukaa bila kazi.

Alieleza kuwa baada ya serikali kuanza kuchukua hatua kuanzia Machi na Novemba mwaka 2017, baadhi ya watu walianza kulalamika kuwa serikali inachukua mchanga wao.

Alisisitiza kuwa ni vyema wananchi wakaelewa kuwa ardhi yote ya Zanzibar ni mali ya serikali, hivyo rasilimali ya mchanga yote ni mali ya serikali kwa mujibu wa sheria na katiba ya nchi, na yeye ndie msimamizi wa ardhi hiyo.

Pia, alisema sababu nyingine ya uhaba wa rasilimali hiyo ni kutofuatwa kwa sheria za na kuwatupia lawama viongozi na wananchi wa wilaya hiyo kwa kuchangia uhaba huo.



Mwenyekiti wa UWT Taifa, Gaudensia Kabaka (kulia), akisalimiana na viongozi wa CCM Wilaya ya Muheza na wananchi wa Mtaa wa Majengo Shimoni wilayani humo juzi akiwa safarini kuelekea mkoani Kilimanjaro. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# SMZ yaeleza inavyowajali wenye ulemavu ajira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), imesema hakuna ubaguzi wa watu wenye ulemavu kupata ajira katika ofisi zake.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud, wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalum, Salma Bilali Mussa, aliyetaka kujua kwa nini watu wenye ulemavu hawapati ajira katika ofisi za serikali.

Alisema SMZ inatekeleza mkataba wa kimataifa wa haki na fursa sawa za watu wenye ulemavu wa mwaka 2006 ibara 27 (A) kinachokataza ubaguzi.

Mohamed alisema katika mwaka 2016-2018 jumla ya watu wenye ulemavu 268 wameajiriwa katika Ofisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na taasisi zake.

Alisema miongoni mwa watu wenye ulemavu walioajiriwa katika ofisi za serikali na kushika wadhifa wa juu ni wakurugenzi.

"Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Baraza la Wawakilishi kwamba hakuna ubaguzi kwa watu wenye ulemavu kuajiriwa katika ofisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar...tumeajiri jumla ya walemavu 268, wapo walioshika nafasi za ukurugenzi," alisema.

Aliwataja walemavu hao wapo 180 wanaume na 88 ni wanawake, na kuwa wakionyesha uwezo mkubwa wa kufanya kazi kwa nafasi walizoajiriwa.

Aidha, Mohamed alisema serikali inatekeleza mikataba ya kimataifa ikiwamo wa kulinda watu wenye ulemavu na kuona fursa na haki zote wanapata kwa mujibu wa sheria.

Alisema serikali iko katika mpango wa kuwasajili watu wenye ulemavu

Unguja na Pemba kwa ajili ya kuwatambuwa ili waweze kufaidika na fursa zinazotolewa na serikali.

"Tumeanza kazi ya kusajili walemavu wote Unguja na Pemba kwa ajili ya kuwatambua na kuona wananufaika na fursa za ajira katika ofisi za serikali," alisema.

# RATIBA

## CAPITAL TELEVISION

**Mon 18 Feb**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the spotlight rpt:
12:30 Drive it rpt
13:00 Series rpt : Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Usafiri wako rpt
15:00 Cookery rpt: Culinary Delight
15:30 Toyota world of wildlife rpt
16:00 CNN International
17:00 Eco@Africa rpt
17:30 Meza huru
19:00 The Décor rpt
19:30 Business edition
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 The Monday Agenda
21:30 Capital Prime News
22:00 Kipima Joto
00:00 Al Jazeera

**Tues 19 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 The Decor rpt
12:30 Mizengwe rpt
12:45 Aibu Yako
13:00 Series rpt: Grapes of justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:15 Local pgm rpt: Business Edition
15:00 Bundesliga kick off
15:30 Out and About rpt
16:00 Capchat rpt
17:00 Ripoti Maalum rpt
17:30 Meza huru
19:00 Innovation
19:30 Ripoti Maalum
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime
22:00 Turning the Spotlight rpt
22:30 Iron Chef rpt
23:30 Al Jazeera

**Wed 20 Feb**
06:00 Al jazeera
08:00 CNN International News
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Turning the Spotlight rpt
12:30 Culinary delight rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Local Pgm: The Monday Agenda Rpt
15:15 Capchat rpt
16:15 CNN International
17:00 Innovation rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Sports Gazette
19:30 Business edition rpt
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Dakika 45:
22:45 The Décor
23:15 Al Jazeera

**Thurs 21 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Sports Gazette
12:30 Out n' about rpt:
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Business Edition rpt
15:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
16:00 Dakika 45 rpt
17:00 In good shape
17:30 Meza Huru
19:00 Turning the spotlight
19;30 Usafiri wako
20:00 Series: Grapes of Justice
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Capchat rpt
23:00 Al Jazeera

**Frid 22 Feb**
06:00 Al Jazeera
08:00 CNN International News
09:00 Al Jazeera
10:00 Kumekucha
10:30 Kumekucha Michezo
11:30 Kumekucha Kishindo
12:00 Innovation rpt
12:30 The Decor rpt
13:00 Series rpt: Grapes of Justice
13:45 Series rpt: Ode To Joy
14:30 Ripoti Maalum rpt
15:00 Korean Dram rpt: Emperor of the sea
16:00 CNN International
16:30 The Monday Agenda rpt
17:30 Meza Huru
19:00 Drive it
19:30 Eco@Africa
20:00 Aibu yako
20:15 Local Pgm: Business Edition
20:45 Series: Ode To Joy
21:30 Capital Prime News
22:00 Malumbano ya hoja rpt
00:00 Al Jazeera

**Sat 23 Feb**
08:00 CNN International
09:00 Drive It rpt
09:30 Turning the Spotlight rpt
10:00 Culinary delight rpt
10:30 Innovation rpt
11:00 Out n'about rpt
11:30 Sports Gazette rpt
12:00 Usafiri wako rpt
12:30 Eco@Africa rpt
13:00 Business edition rpt
13:30 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
14:30 Telenovela rpt: Ode To Joy
17:15 Ripoti Maaalum rpt
17:45 Bundesliga kick off
18:15 Capchat rpt
19:15 Mizengwe
19:30 The Decor
20:00 Iron Chef.
21:00 Out n' about
21:30 Movie: Delirious
23:00 Grapes of Justice rpt
01:00 Al Jazeera

**Sun 24 Feb**
08:00 CNN International
09:00 In good shape
10:00 Capchat rpt
11:00 Sports Gazette rpt
11:30 Iron chef rpt
12:00 Out n about rpt
12:30 Bundesligga Kick Off rpt
13:00 Ripoti Maalum
13:30 Series rpt: Grapes of Justice
15:15 Aibu yako
15:30 Drive it rpt
16:00 Dakika 45 rpt
16:45 Mizengwe rpt
17:00 The Decor rpt
17:30 Meza huru
19:00 Turning the Spotlight rpt
19:30 Cookery pgm:Culinary Delights
20:00 Korean Drama rpt: Emperor of the sea
21:00 Shift
21:15 Capchat live
22:15 Telenovela: Ode To Joy
00:00 Al Jazeera

## ITV Daima WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY 18 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Kimya Milele
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jungu kuu rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Mjue Zaidi
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:10 Aibu yako rpt
18:15 Huduma ya kwanza
18:30 Shamba shape up
19:00 Afya ya Jamii
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Dakika 45
22:00 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**TUESDAY 19 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 Habari
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:15 Igizo: Mtego
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Afya ya jamii rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Uchumi na biashara
13:30 Kipindi Maalum rpt : TFDA
13:55 Habari za saa
14:00 Huduma ya kwanza
14:15 Telenovela: Destiny (Destino) rpt:
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Korean drama rpt: The Great Queen Seonduk
19:00 Jarida la wanawake
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Kipindi maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**WEDNESDAY 20 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Shamba shape up
10:55 Habari za saa
11:00 Korean: The Great Queen Seonduk
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Jarida la wanawake rpt
12:55 Habari za saa
13:00 Dakika 45
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino):
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi rpt
18:30 Ijue Sheria
19:00 Kipindi Maalum: TFDA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Aibu Yako! Hata wewe?
21:10 Kipindi Maalum : Tanesco
21:40 Kipindi Maalum:
22:15 Telenovela: Destiny (Destino)
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 Al Jazeera
02:00 CNN International

**THURSDAY 21 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Igizo: Hatua
10:55 Habari za saa
11:00 Igizo: Hatua
11:15 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al jazeera
12:30 Ijue Sheria
12:55 Habari za saa
13:00 Sanaa na wasanii rpt
13:30 Jungu Kuu
13:55 Habari za saa
14:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza Huru
16:30 Watoto Wetu
17:00 The Base
18:00 Jiji Letu
18:15 Huduma ya kwanza rpt
18:30 Kipindi Maalum: Ewura
19:00 Usafiri wako
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:00 Malumbano ya hoja
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**FRIDAY 22 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:30 HABARI
08:00 Kumekucha Michezo
08:55 Habari za saa
09:00 Kumekucha Kishindo
09:30 Isidingo
09:55 Habari za saa
10:00 Watoto wetu
10:30 Hawavumi lakini wamo
10:55 Habari za saa
11:00 Hawavumi lakini wamo
11:20 Usafiri wako
11:55 Habari za saa
12:00 Al Jazeera
12:30 Kipindi Maalum rpt: TCRA
12:55 Habari za saa
13:00 Kipindi maalum: Tanesco
13:30 Kipindi Maalum rpt - Ewura
13:55 Habari za saa
14:00 Mapishi
14:15 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:55 Habari za saa
15:00 Meza huru
16:30 Watoto wetu
17:00 The Base
17:30 Ibada ya kiislamu
18:00 Jiji Letu
18:15 Igizo: Mizengwe
18:30 Uchumi na biashara
19:00 Kipindi maalum: TCRA
19:30 Isidingo
20:00 Habari
21:05 Kipima joto
23:00 Habari
23:30 The Base
00:30 CNN International

**SATURDAY 23 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al Jazeera
09:00 Watoto wetu
10:00 Mjue Zaidi rpt
11:00 Jungu kuu rpt
11:30 Usafiri wako
12:00 Shamba Shape up
12:30 Telenovela rpt: Destiny (Destino)
14:45 Igizo rpt: Riziki
15:15 Igizo rpt: Hatua
15:45 Igizo rpt: Mizengwe
16:00 Igizo rpt: Kimya Milele
16:30 Igizo: Mtego rpt
17:00 Shamsham za Pwani
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Igizo: Riziki
19:00 Sanaa na wasanii
19:30 Jungu Kuu
20:00 Habari
21:00 Igizo: Kimya Milele
21:30 Hawavumi lakini wamo
22:30 Isidingo rpt
01:00 CNN International

**SUNDAY 24 Feb**
05:30 Uwanja wa Mazoezi
06:00 HABARI
06:40 Kumekucha
07:00 Habari
08:00 Al jazeera
09:00 Watoto Wetu
10:00 Isidingo
11:45 Aibu Yako
11:50 Hawavumi lakini wamo rpt
12:50 Bongo Movie rpt: Green Light 2
14:00 Tamasha la Michezo
15:00 Mwangaza
16:00 Korean drama: The great queen Seonduk
16:45 Mjue zaidi
17:30 Kipindi cha kikristo
18:00 Jiji Letu
18:15 Mapishi
18:30 Mizengwe rpt
18:45 Matukio ya wiki
19:30 Igizo: Mtego
20:00 Habari
21:05 Mizengwe
21:00 Bongo Movie: Kisasi cha utata
22:00 Telenovela rpt: Destiny (Destino)


LEO ASUBUHI SAA 5:00
EATV
DADAZ

JUMATANO
10:59 Jikoni Na Jane
11:00 DADAZ (live)
15:00 FUNGUKA
16:30 #HASHTAG
17:00 5SELEKT
17:55 Kurasa
18:00 eNewz
18:30 Music
19:00 EATV SAA 1
19:30 MJADALA
20:00 EPL REVIEW
21:00 Supa Mzuka Jackpot
21:30 Mid Week Movie
DADAZ Kipindi kinachompatia mwanamke nafasi ya kuzungumza maswala ya kijamii, afya, siasa na uchumi ambayo yanayoizunguka jamii

eastafrica RADIO
05:00 EA Breakfast
09:00 Supamix
12:00 Kipenga Xtra
13:00 Planet Bongo
16:00 EA Drive
20:00 Kipenga
21:00 The Cruise
88.1FM DAR ES SALAAM


## RADIO One WEEKLY-SCHEDULE

**MONDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | RADIO ONE DOCTOR |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DAKIKA 45 |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 -03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | DK 45 ( MARUDIO ) |
| 23.00 HRS | |

**TUESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA SHERIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00 - 03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**WEDNESDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA MICHEZO |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | DURU ZETU |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | AFRO TIZII |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**THURSDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 09.30 AM | KUMEPAMBAZUKA UKIMWI |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | YALIYOMO YAMO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18.30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05 HRS | MALUMBANO YA HOJA |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | AFRO TIZII |
| 01:00-03:00HRS | YALIYOMO YAMO ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**FRIDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | MATANGAZO |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 7:10 AM | MATANGAZO |
| 07.15 AM | TAARIFA ZA BARABARANI |
| 07.25 AM | UDONDOZI WA MAGAZETI |
| 07.40 AM | KUMEPAMBAZUKA II |
| 08.00 AM | HABARI NYEPESI |
| 08.10 AM | KUMEPAMBAZUKA III |
| 09.00 AM | HABARI ZA BIASHARA |
| 09.10 AM | MATANGAZO |
| 09.20 AM | BRAND TALK |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.10 AM | HIZI NAZO |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | DJ SHOW |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | HOJA YA LEO |
| 18:30 HRS | DIRA YA DUNIA BBC |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.10 HRS | UCHUNGUZI KAMILI |
| 21.0O HRS | NEWS BRIEF |
| 21.05HRS | KIPIMA JOTO |
| 23.00 HRS | WEEKEND SHOW |
| 01:00 - 03:00HRS | HIZI NAZO ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00HRS | HOJA YA LEO ( MARUDIO ) |

**SATURDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA KISWAHILI |
| 09.00 AM | WATOTO SHOW |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | MIWANI YA MAISHA |
| 11:00 AM | MTAA WA MAGOMA |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13:30 HRS | CHAGUO LAKO |
| 15:00 HRS | MUZIKI NA MICHEZO |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.15 HRS | MIDUNDO MOTOMOTO |
| 18:00 HRS | BONGO TEN |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20.15 HRS | CHEMSHA BONGO |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | WEEK END SHOW I |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | WEEK END SHOW II |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | WEEK END SHOW III |
| 01:00-03:00HRS | KISWAHILI ( MARUDIO ) |
| 03:00-05:00HRS | MUZIKI & MICHEZO ( MARUDIO ) |

**SUNDAY**

| TIME | PROGRAMME |
|---|---|
| 05.00 AM | HALI YA HEWA / KUMEPAMBAZUKA I |
| 06.00 AM | AMKA NA BBC |
| 06.30 AM | NIPASHE |
| 06.50 AM | COMMERCIALS |
| 07.00 AM | NEWS BULLETIN |
| 07.15 AM | NEWSPAPERS REVIEW |
| 07.30 AM | KUMEPAMBAZUKA - FAMILIA |
| 10.00 AM | NEWS BRIEF |
| 10.03 AM | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 10.15 AM | SUNDAY SPECIAL |
| 11: 00 HRS | TOP 20 |
| 13.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 13.10 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 13.30 HRS | NANI ZAIDI |
| 16.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 16.03 HRS | DEATH ANNOUNCEMENTS |
| 16.30 HRS | MAMBO YA PWANI |
| 18:00 HRS | AFRICAN PANORAMA |
| 19.30 HRS | SPOTI LEO |
| 20.00 HRS | NEWS BULLETIN |
| 20:10 HRS | MBAVU ZANGU |
| 21.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 21.03 HRS | MAMBO MSETO |
| 22.00 HRS | NEWS BULLETIN (24 HRS) |
| 22.15 HRS | RAFIKI I |
| 23.00 HRS | NEWS BRIEF |
| 23.03 HRS | RAFIKI II |
| 01:00 - 03:00 | FAMILIA ( MARUDIO ) |
| 03:00 - 05:00 HRS | RED CARPET ( MARUDIO ) |

## CAPITAL RADIO

### CAPITAL RADIO 2017 101.3 FM
### FAHARI YA MSIKILIZAJI/THE LISTENERS PRIDE

**MONDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-20:00HRS BOZOUK TIME
20:00-21:00HRS HALI HALISI
21:00-22:00HRS SPORTS
22:00-01:00HRS LADHA LAINI

**TUESDAY - FRIDAY**
05:00-09:00HRS MORNING JAM
09:00-13:00HRS LETE RAHA
13:00-14:00HRS DW-RADIO
14:00-16:00HRS CLUB 101
16:00-18:00HRS DALA DALA
18:00-18:10HRS HABARI
18:10-21:00HRS BOZOUK TIME
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI
01:00-05:00HRS MUSIC & JINGLES

**SATURDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS DK 90 DUNIANI
09:00-10:00HRS MUZIKI
10:00-12:00HRS KADOGOO
12:00-13:00HRS BONGO HITS 1
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS BONGO HITS 2
15:00-16:00HRS ZAIDI YA UMJUAVYO
16:00-18:00HRS THE SPLASH
18:00-21:00HRS LAID BACK
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS AK 47 LIVE
01:00-05:00HRS MUSIC

**SUNDAY**
05:00-07:30HRS MUZIKI
07:30-09:00HRS GOSPEL MUSIC
09:00-11:00HRS THE SUNDAY
11:00-13:00HRS TOP TWENTY
13:00-14:00HRS DW RADIO
14:00-15:00HRS CAPITAL MICHEZONI
15:00-16:00HRS UKURASA WA MBELE
16:00-18:00HRS UNLIMITED REQUEST
18:00-21:00HRS JIACHIE
21:00-21:30HRS SPORTS
21:30-01:00HRS LADHA LAINI

# Majimbo 16 Marekani yamshtaki Rais Trump

**WASHINGTON, Marekani**

JIMBO la California nchini Marekani pamoja na majimbo mengine 15 yamefungua mashtaka dhidi ya uamuzi wa rais wa nchi hiyo Donald Trump wa kujenga ukuta katika mpaka unaozitenganisha Marekani na Mexico.

Wanaoiunga mkono California ni wanasheria wakuu kutoka majimbo ya; Colorado, Connecticut, Delaware, Hawaii, Illinois, Maine, Maryland, Michigan, Minnesota, Nevada, New Jersey, New Mexico, New York, Oregon, na Virginia

Mwanasheria Mkuu wa California, Xavier Becerra alitoa taarifa rasmi inayosema mashitaka hayo yanapinga hatua ya utawala wa Trump ambayo inakiuka sheria ya nchi hiyo.

Becerra alisema kwamba Rais Trump anautumia utawala wa sheria kwa kudharau na anajua hakuna mgogoro wa mpaka, anajua tamko la hali ya dharura ya taifa halikubaliki, na anakiri kwamba huenda akashindwa katika kesi hii ikifika mahakamani.

Wiki iliyopita akizungumzia ujenzi wa ukuta huo, Rais Trump alisema kwamba chama cha Democratic kinampinga kwa sababu kinafikiri kufanya hivyo kutakisaidia kushinda uchaguzi ujao.

"Ninaweza kuujenga ukuta kwa kipindi cha muda mrefu. Sijakuwa na lazima ya kuchukua hatua hii ya haraka. Lakini ningependa kuujenga haraka. Na sina haja ya kufanya hivyo kwa ajili ya uchaguzi," alisema na kuongeza.

"Nishafanya vya kutosha kwa ajili ya uchaguzi wa 2020. Na sababu pekee tunalijadili suala hili ni uchaguzi. Wanatafuta ushindi wa uchaguzi, ambao inaonekana kama watashindwa. Na hii ni moja wapo ya njia wanayodhani inaweza kuwasaidia kushinda, kwa kuleta pingamizi na mengi yasiyokuwa na maana," alisema Trump.

Majimbo yote yanayohusika na kesi hiyo yana wanasheria wakuu wanaotoka chama cha Democratic. Trump alitangaza hali ya dharura ya kitaifa ili kutimiza ahadi yake ya kujenga ukuta wa Mexico. Hatua hiyo itamruhusu Rais Trump kulikwepa bunge kutumia fedha kutoka Wizara ya Ulinzi ya Marekani Pentagon na bajeti nyingine.

Majimbo hayo yanasema utumiaji wa fedha za jeshi kujenga ukuta utaumiza uchumi na kuzinyima kambi za kijeshi kufanyiwa ukarabati unaohitajika.

DW

# Kenya yatangaza kufunga kambi ya wakimbizi

**NAIROBI, Kenya**

KENYA imeuomba Umoja wa Mataifa (UN) kufunga kambi ya wakimbizi ya Dadaab, kwa kile walichokieleza ni sababu za kiusalama.Kambi ambayo

ilifunguliwa miaka ya 1990, karibu na mpaka wa Somalia.

Katika miaka ya nyuma kambi hiyo iliwahi kuwa mojawapo ya kambi kubwa ya wakimbizi duniani na bado ina wakimbizi zaidi ya 200,000 wengi wao wakiwa ni Wasomali na ilifunguliwa miaka ya 1990 katibu na mpaka wa Somalia.

Kenya imeomba Shirika la Umoja wa Mataifa linalohudumia Wakimbizi (UNHCR) kuhamisha wakimbizi kutoka Dadaab kwenda Somalia au katika nchi nyingine kwa wanaotafuta hifadhi.

Ombi hilo lilitolewa na Wizara ya Mambo ya Nje katika barua ya Februari 12 mwaka huu, ambayo ilikabidhiwa UNHCR.

Sababu iliyotolewa bado haijaeleweka kwa UN lakini serikali ya Kenya inasema kuwa Dadaab inatumiwa kama kambi ambako kunafanyika shughuli zinazohatarisha usalama wa taifa, ikiwa ni pamoja na ugaidi.

Kauli hiyo ya serikali ya Kenya inakuja siku chache baada ya shambulizi la wanamgambo wa Kiislam wa Al Shabab dhidi ya hoteli ya kifahari ya Dusit jijini Nairobi mwezi uliopita. Shambulio ambalo liligharimu maisha ya watu 21.

Tangu wakati huo, uchunguzi ulionyesha kuwa mwanamgambo mmoja wa kundi hilo alipitia kambi ya Dadaab kabla ya tukio hilo ambapo aliweza kupata msaada wa kutekeleza shambulio hili.

RFI



Kambi ya wakimbizi ya Dadaab, iliyopo mpaka wa Somalia, yenye wakimbizi zaidi ya 200,000, ambayo Kenya imetangaza kuifunga. **PICHA: REUTERS**

# Rais Buhari atoa onyo watakaovuruga uchaguzi

**LAGOS, Nigeria**

ZIKIWA zimebaki siku tatu kufanyika kwa uchaguzi wa urais nchini Nigeria, Rais wa nchi hiyo Muhammadu Buhari amesema amewaagiza polisi na jeshi kutomuonea huruma mtu yeyote atakayejaribu kuvuruga uchaguzi wa rais unaotarajiwa kufanyika Jumamosi ya wiki hii.

Tume huru ya uchaguzi ya Taifa Nigeria (INEC) ilitangaza kuhairisha uchaguzi huo saa kadhaa kabla ya vituo vya kupiga kura kufunguliwa kwamba uchaguzi utaahirishwa kwa wiki moja.

INEC ilisema uchaguzi wa rais na wabunge utafanyika Jumamosi, wakati uchaguzi wa magavana na baraza la wawakilishi utasogezwa mbele hadi machi 9.

Vyombo vya habari nchini humo vimeeleza baadhi ya matatizo yaliyokuwapo katika kusambaza vifaa vya uchaguzi katika maeneo mbalimbali ya taifa hilo la Afrika Magharibi.

Buhari, mwenye umri wa miaka 76, akizungumza katika mkutano wa dharura wa chama chake cha All Progressives Congress (APC) aliishutumu INEC kuwa haina uwezo na kumwonya yeyote atakayejaribu kuharibu masanduku ya kupigia kura na vifaa vya uchaguzi.

"Yeyote anayefikiria anaushawishi katika eneo lake kuongoza kikundi cha wahuni au kuiba masanduku au kuvuruga mfumo wa uchaguzi, atafanya hivyo kwa kulipa thamani ya maisha yake," alisema Rais Buhari.

Chama cha APC na chama cha upinzani cha People's Democratic Party vimekuwa vikituhumiana kwa jaribio la kutaka kuiba kura. Rais Buhari anakabiliwa na changamoto kutoka mgombea wa chama cha upinzani PDP, Atiku Abubakar, ambaye alikuwa ni makamu wa rais wa zamani.

*VOA*

## Balozi atuhumiwa unyanyasaji kijinsia

**PORT VILA, Vanuatu**

BALOZI wa Ufaransa nchini Vanuatu, Robby Judes anashutumiwa kwa kuwanyanyasa kimapenzi baadhi ya wanawake katika eneo hilo.

Judes, aliyeteuliwa miezi minne iliyopita kwenye nafasi hiyo, anakabiliwa na mashitaka mawili katika ofisi ya mwendesha mashitaka ya Noumea huko New Caledonia.

Wizara ya mambo ya Nje ya Ufaransa, imemuita nyumbani jijini Paris kwenda kumsikiliza na anatarajiwa kusikilizwa na Mkurugenzi Mkuu wa Utawala kwenye wizara hiyo. Inaelezwa kuwa mkasa huo ulitokea wakati wa chakula cha jioni kati ya viongozi wa kampuni na wawakilishi wa vyama vya siasa, siku nane zilizopita huko Nouméa.

"Balozi Robby Judes alipita nyuma yangu, akagusa makalio yangu. Wakati huo, nilidhani alikosa nafasi na hivyo kunisukuma kidogo ili aweze kukaa, wala sikufikiria chochote. Lakini baadaye alirudi na wakati huo, alinigusa mgongoni na kwenye makalio, akaniambia kwamba anataka kuniona tena, "alisema Cherifa Linossier ambaye ni mmoja wa waathirika."

Taarifa zinaeleza kuwa wanawake saba wamesha nyanyaswa kijinsia, kutukanwa na balozi Robby Judes katika miezi ya hivi karibuni. = "Kunaweza kuwa na wanawake wengi waliofanyiwa kitendo kama hicho, Ni vitendo ambavyo havikubaliki na ambavyo vinatakiwa kukemewa au kuchukuliwa hatua," "alisema Linossier.

Hadi sasa mashitaka mawili tayari yamewasilishwa, lakini Wizara ya Mambo ya Nje ya Ufaransa imejibu mara moja tu.

*RFI*

## Bosi wa PSSSF atumbuliwa

**Na Mwandishi Wetu**

Rais John Pombe Magufuli amemteua Hosea Ezekiel Kashimba kuwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF).

Kashimba anachukua nafasi ya Eliud Sanga ambaye uteuzi wake umetenguliwa.

Kabla ya uteuzi huo, Kashimba alikuwa Mkurugenzi wa Ukaguzi wa Ndani wa Shirika la Hifadhi ya Jamii la NSSF.

Wakati huo huo, Rais Magufuli amefanya uteuzi wa viongozi wengine 2 ambao ni Augustine Emmanuel Mbokella kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Biashara ya TIB.

Poa amemteua Latifa Mohammed Khamis kuwa Naibu Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Biashara za Nje (TANTRADE).

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi Mhe. Balozi John Kijazi jana ilieleza kuwa uteuzi wa viongozi hao ulianza jana.

## Waziri alaani mauaji watoto

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Faustine Ndugulile, amelaani mauaji na matendo ya kikatili yanayofanywa dhidi ya watoto, huku akivishukuru vyombo vya dola kwa hatua za haraka vinazoendelea kuchukua katika kudhibiti matukio hayo.

Dk. Ndugulile aliyasema hayo jana alipofanya ziara ya kukagua hali ya Makazi ya Watoto wanaoishi katika mazingira magumu, Kurasini jijini Dar es salaam.

Alisema serikali haiwezi kuvumikia mambo yakikatili yanayofanywa dhidi ya watoto na haki zao, hivyo itamchukulia hatua yeyote atakayebainika kuvunja sheria zinazomlinda mtoto.

"Tunalaani sana mauaji haya ya watoto na tunavishukuru vyombo vya dola vimechukua hatua za haraka kuhakikisha vinadhibiti matukio haya," alisema Dk. Ndugulile

Pia alitoa rai kwa waganga wote wa tiba asilia na tiba mbadala kuacha kutumia viungo wala miili ya watoto kama njia ya kutatua matatizo kwa wateja wao, hivyo hatua kali zitachukuliwa kwa watakaokaidi agizo hilo.

Aliongeza kuwa waganga hao ni lazima wahakikishe wanajisajili katika mamlaka na baraza husika ili kuepuka usumbufu na hatua kali dhidi yao pindi watakapobainika hawajafanya hivyo.

# Wakili Takukuru akwamisha kesi ya hakimu ya rushwa

**Na Enock Charles**

KESI ya kupokea rushwa inayomkabili Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ya Ukonga jijini Dar es Salaam, Dickson Mwasenga (46), imeahirishwa baada ya Wakili wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kushindwa kufika mahakamani.

Mwendesha Mashtaka wa Mahakama ya Wilaya ya Ilala, Anna Chimpaye, aliieleza Mahakama hiyo kuwa Wakili wa Takukuru hakufika mahakamani hapo hivyo aliiomba mahakama iahirishe kesi hiyo.

Akiahirisha kesi hiyo, Hakimu Mkazi wa Mahakama hiyo, Samuel Obasi aliwataka watuhumiwa kufika mahakamani hapo Machi 13 mwaka huu kesi hiyo itakapo tajwa tena.

Hakimu huyo alifikishwa katika Mahakama ya Ilala kwa mashtaka matatu ya kupokea rushwa ya jumla ya Sh. 710,000.

Akisoma mashtaka hayo mbele ya Hakimu Samuel Obasi, Mwendesha Mashtaka, Devota Mihayo alidai kuwa mshtakiwa huyo alipokea rushwa hiyo ili kufanya upendeleo katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017 iliyokuwa ikimkabili ofisa wa benki ya CRDB, Ngomoi Mmbaga (42).

Katika shtaka la kwanza, ilidaiwa kuwa Februari 22 mwaka juzi mshtakiwa huyo alipokea Sh.210, 000 kutoka kwa Ngomoi Mmbaga kupitia tigo pesa ili kumpa upendeleo ofisa huyo wa benki katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Aprili 14 mwaka juzi mshtakiwa huyo alipokea Sh 100,000 kutoka kwa Ngomoi Mmbaga kupitia tigo pesa ili kumpa upendeleo afisa huyo wa benki katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017.

Katika shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa Mei Mosi mwaka juzi, mshtakiwa Dickson Mwasenga alipokea Sh. 400 000 kutoka kwa Ngomoi Mmbaga kupitia tigo pesa ili kumpa upendeleo ofisa huyo wa benki.

katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017, jambo ambalo alisema ni kinyume cha Sheria ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa kifungu 15 (1) namba 11 ya mwaka 2017.

Wakati huo huo, mshtakiwa wa pili, Ngomoi Mmbaga, alisomewa mashtaka matatu na Mwendesha Mashtaka, Devota Mihayo kwa kutoa rushwa ili kufanyiwa upendeleo katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017 katika mahakama hiyo ya mwanzo.

Katika shtaka la kwanza, ilidaiwa kuwa Februari 22 mwaka juzi mshtakiwa Ngomoi Mmbaga alituma Sh 210,000 kwenda kwa Dickson Mwasenga kupitia tigo pesa ili kupewa upendeleo katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa Aprili 14 mwaka juzi mshtakiwa huyo alituma Sh. 100,000 kwenda kwa Dickson Mwasenga kupitia tigo pesa ili kupewa upendeleo katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017.

Katika shtaka la tatu tatu, ilidaiwa kuwa Mei Mosi mwaka juzi mshtakiwa Ngomoi Mmbaga alituma Sh. 400 000 kwenda kwa Dickson Mwasenga kupitia tigo pesa ili kupewa upendeleo katika kesi ya jinai namba 352 ya mwaka 2017.



Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TAN TRADE), Edwin Rutageruka, akizungumza na wajasiriamali jijini Dar es Salaam jana, kuhusu namna watakavyopata elimu ya kuchangamkia fursa ya kuuza bidhaa zao ndani na nje ya nchi. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Mpango kuwalinda faru wausi waja

**Na Salome Kitomari**

TAASISI ya Utafiti wa Wanyamapori (Tawiri), inaandaa mpango mkakati wa miaka mitano ambao pamoja na mambo mengine una lengo la kuwalinda faru weusi Tanzania.

Mtafiti Mwandamizi wa Tawiri, Dk. Alex Lobora, aliyasema hayo hivi karibuni wakati wa mkutano wa pamoja wa kiufundi uliwajumuisha wataalamu kutoka Mfuko wa Kimataifa wa kulinda Viumbe vya Asili (WWF), Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori (Tawa), Tawiri na shirika la Frankfurt Zoological Society (FZS).

Alisema ili kuwa na kizazi endelevu cha faru, zinahitajika nguvu za pamoja baina ya serikali na wadau wa mazingira katika kuwalinda wanyama hao na kuwatafuta kwenye Pori la Akiba la Selous kujua eneo sahihi walilopo. Tangu mwaka 1993, alisema serikali imekuwa na mpango wa taifa kwa awamu tatu tofauti ambayo imekuwa ikiboresho umekuwa ukiboreshwa kila baada ya miaka mitano ikiwamo kufuatilia utekelezaji wake.

Alisema kwa sasa wanauboresha ili kuhakikisha wanyama hao anaendelea kuwepo nchini ikiwamo kutangaza utalii.

"Kuwapo kwa mpango mkakati na utawala wa faru, tumeandaa mipango mkakati kumi ambao umetokana na wadau wenyewe, umeziangazia changamoto zinazowakabili Faru katika mazingira waliyopo," alisema.

Mratibu wa Ukanda wa Ruvuma wa WWF Tanzania, James Nshare, alisema lengo kuu la mkutano huo ni kuwa na mbinu za pamoja za ufuatiliaji wa Faru na namna bora zaidi ya kuwalinda dhidi ya ujangili na vitendo vinginevyo. "WWF inashirikiana na wadau wa serikali na wengine katika kuhakikisha uhifadhi wa Faru unaongezeka na kunakuwa na utaratibu sahihi katika eneo la Pori la Akiba la Selous," alisema Nshare.

Naye Mtafiti Mwandamizi wa Tawiri, Dk. Edward Kohi, alisema kwa sasa watabadili mbinu kwa kuwaangalia Faru kupitia angani na kujenga jengo maalum la Faru ambalo litakuwa na vifaa muhimu vya ulinzi.

Mwikolojia Pori la Akiba la Selous, ambaye pia ni Mratibu wa Faru wa Tawa, Singira Parsais, alisema changamoto kubwa kwa sasa ni ujangili wa Faru katika eneo la Msitu mnene wa Miombo na hivyo wakati mwingine kushindwa kujua idadi yao.

Aidha, alisema lipo hitaji la kufanya mabadiliko ya sheria ya wanyamapori ya mwaka 2009, ikiwa ni pamoja na kurejesha mpango wa kitaifa wa Faru, ili kuwa na sheria na kanuni kali dhidi ya uhifadhi.

Miaka ya 1960 ilikadiriwa kuwa Tanzania ina Faru weusi 10,000, lakini idadi yao iliendelea kupungua hadi mwanzoni mwa miaka ya 1970 kutokana na ujangili.

Tanzania ina Faru weusi kwenye Hifadhi za Taifa za Mkomazi na Serengeti pamoja na kwenye Mapori ya Akiba ya Grumeti na Maswa.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## HUDUMA MBALIMBALI

**MKOPO WA HARAKA NA NAFUU** Pata mkopo wa dharura ndani ya siku 2. Kwa wafanyakazi na Wafanyabiashara kutoka ENTERPRISE FINANCE LIMITED (EFL). Kwa mawasiliano Zaidi piga: 0768 928516 / 0653 258662. KARIBU EFL.

## MASHAMBA/VIWANJA

**KIWANJA KINAUZWA,** Kipo Kisongo Arusha jirani na Braebun School Kina upana wa 43,urefu 93 . Bei Milioni 40 kimepimwa. Maji, barabara na umeme vipo. Mawasiliano:-0755 907 520.

**SHAMBA LA ACRE 2 LINAUZWA** liko kilometre 3 toka chanika mjini ,mtaa wa > zogo ally kata ya homboza wilaya ya kisarawe bei ni milioni 43. No ya cm ni 0653019311

## NAFASI ZA KAZI

**LOOKING FOR TOYOTA** NOAH for hiring long term contract. price 30,000 - 40,000 per day. Please call 0627301010 for details.

**TUNAAJIRI WASICHANA WA MAUZO (SALES).** SIFA KIDATO CHA NNE. UMRI KUANZIA MIAKA 25 – 38 AWE MTANZANIA. MASLAHI MAZURI. PIGA SIMU NAMBA 0714 634046.

*Uza Chenye Thamani Kubwa*
*Kwa Kutangaza Nasi*
*Kwa Bei Poa*
*Tupigie 0767 223311*

## KUPOTEA KWA CHETI




**Nickiza Daniel Musula** anatangaza kupotelewa na cheti cha Degree ya Sheria chenye namba **LLB/013/113** kilichotolewa na Chuo cha Kikuu cha Tumaini mwaka 2013-2016.

**Yeyote atakekiona atoe Taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: 941/2019**

115069301

## KUPOTEA KWA CHETI



**Eripidius Eradius** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S.0339-0046** kilichotolewa na Baraza la Taifa mwaka 2015 katika shule ya Sekondari Omumwani .

**Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.**

**Polisi Taarifa: SBR/RB/355/19**

115069102

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**WAHABU BAKARI NGULANGWA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **ISUZU - TIPPER** yenye namba za usajili **T 718 ASX** .Chassis namba **NKR68E7174915.** Engine namba. **NBE -1164791.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DOMR/TR/276/2019**

115069702

**JAUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAM A**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya mwanzo DODOMA mjini**

**Usimamizi wa mirathi no.10/2019**

**Ombi la HULGA NELSON SHOO kuteuliwa Msimamiliz wa mirathi NELSON EPHRAHIM SHOO**

**Kwa yeyote anayehusika Tanzania Bara**

Watu wote anaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanalikw kuhudhuria kesi wakitaka mnano 12/3/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyoupo mahakamni waweza kukaguliwa Tarehe 19/2/2019

Tarehe 19/2/2019

215069502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM 11**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MAKOLE**

**Usimamizi wa Mirathi No.1/2019.**

**Ombi la WILSON RICHARD SONGORO kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu ZIPORA MAREBI HABELI**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 23/1/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia yamarehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa. Tahehe 02/01/2019

215069602

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KONDOA**

**MAOMBI NA. 74 MWAKA 2018**

**RINGO E. MARTIN...... MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

**HAPPINESS PHARES MUSHI .... MUOMBAJI**

**WITO/KUITWA SHAURINI**

**KWA HAPPINESS PHAREES MUSHI**
Fahamu kwa shauri hili limepangwa kutajwa/kusikilizwa tarehe 21 mwezi 2 saa 3 Asubuhi mbele ya Mh. M. KHASIM mwenyekiti wa Baraza. Hivyo unaamuriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri/Muhuri wa Baraza hii leo 12/2/2019.

MWENYEKITI

215071202

## WITO WA MAHAKAMA

**Bwana Rupaji Donati** Msingi mmiliki wa Gari namba **T 780 DLK** na dereva wake Bw. Shazili Ally Mkagunde na wenzake wawili wafike Mahakama ya Hakimu mkazi Kisutu mnamo tarehe **25/3/2019** kusikiliza kesi inayowakabili.

215071202

## MNADA WA HADHARA

Kwa idhini tuliyopewa na **TUJIJENGE TANZANIA LTD, JOSINA CO. LTD & Auctioneer** tutauza kwa mnada wa hadhara Gari la Ndugu **Mayunga Jija Isonzo T. 703CQS MISTUBISH ROSA** ili kufidia/ kupunguza deni lake la mkopo analodaiwa. Mnada utakafanyika **Tarehe 27/02/2018,** Buzuruga Plaza – Mwanza. **JOSINA Co. Ltd : 0768203040 MWANZA: 0712194936**

115070902

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PUYO ELENOR NZALAYAIMISI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 614 DNN,** aina ya Suzuki SWIFT.Yenye chassis namba **HT515742848** na engine namba **2223FY.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TaarifayaPolisi: **KJN/RB/2812/2019.**

115070002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SEIF ZAHORO CHOMOKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 979 DGY,** aina ya TOYOTA MARK X.Yenye chassis namba **GRX1203012138** na engine namba **4GR098KD591.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi. TaarifayaPolisi: **KJN/RB/2812/2019.**

115069902


# JE UNAHANGAIKA PA KUUZA BIDHAA YAKO?

**Nipashe**

NI JIBU LAKO NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, Tupigie 0767 223311

*Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku*
*Tupigie 0767 223 311*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Timu iliyofungwa 20-0 Italia yaondolewa kwenye ligi

**ROME, Italia**

TIMU ya Pro Piacenza imeondolewa kwenye Ligi Daraja la Tatu nchini Italia, Serie C, baada ya kuwachezesha wachezaji saba tu wakati wakifungwa mabao 20-0 Jumapili.

Wachezaji wote hao saba waliocheza dhidi ya Cuneo walikuwa ni vijana wadogo, huku nahodha, Nicola Cirigliano mwenye umri wa miaka 18, akihudumu pia kama kocha.

Kabla ya mchezo huo wa Jumapili, walitoka kufungwa katika mechi tatu mfululizo. Klabu hiyo ambayo imekumbwa na matatizo ya kifedha ilikuwa inaburuza mkia kwenye Ligi Daraja la Tatu, uongozi ulishindwa kuwalipa mishahara wachezaji wake pamoja na benchi la ufundi.

Mchezaji wa nane alishindwa kucheza kwenye mchezo huo wa Jumapili baada ya kusahau kitambulisho chake na daktari wa viungo wa timu hiyo aliingia kucheza kama mchezaji wa akiba.

Jumatatu bodi ya ligi hiyo ilisema baadhi ya wachezaji walikuwa hawajasajiliwa na hawakuwa na viwango na wameiondoa timu hiyo kwenye mashindano hayo na kuipa Cuneo ushindi wa mabao 3-0.

Bodi hiyo ya ligi pia imewatoza Pro Piacenza faini ya euro 20,000 kwa tabia ambayo haikubaliki kwenye ligi hiyo.

Shirikisho la Soka la Italia (FIGC), lilieleza kushangazwa na kitendo hicho na kutoa wito kisijirudie kwa timu nyingine, kwa kuwa adhabu kali itatolewa.




# RAIS INTER
## AGOMA ICARDI KUTUA JUVE

**TURIN, Italia**

RAIS wa Inter Milan, Steven Zhang, amesisitiza kwamba hakuna nafasi ya Mauro Icardi kujiunga na mabingwa wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Juventus.

Ofisa wa Juve, Fabio Paratici, alibainisha kwamba vinara hao wa Ligi Kuu wamepeleka maombi ya kutaka kumsajili Icardi ambaye kwa sasa majaliwa ya ndani ya Inter hayajulikana.

Icardi alipokonywa unahodha wiki iliyopita, huku pia akikosa mchezo wa Ligi ya Europa dhidi ya Rapid Vienna na kwenye mchezo wa ushindi wa Serie A dhidi ya Sampdoria.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, na mke wake, Wanda Nara ambaye ni wakala wake, amesema Icardi hana mpango wa kuondoka Inter.

Aipoulizwa kuhusu uwezekano wa Icardi kuchukuliwa na Juve, Zhang alisema: "Katika soka kamwe huwezi kusema kamwe hasa kwa timu kama Juventus."

"Hata hivyo, kwa hali jinsi ilivyo hakuna nafasi ya Icardi kwenda Juventus. Tulizunguza wiki iliyopita, tunataka kusema inatosha kuhusu habari hii.

"Tupo kwenye mazungumzo ya kumpa mkataba mpya, na falsafa yetu ni kuhakikisha kwamba mchezaji huyu anabakia na sisi hapa."

# Solskjaer: Pogba kiungo bora duniani

**MANCHESTER, England**

KOCHA wa muda wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer, amesema Paul Pogba ni mmoja wa viungo bora zaidi washambuliaji duniani kwa sasa, baada ya kuonyesha kiwango cha juu kwenye ushindi wa mchezo wa Kombe la FA raundi ya tano dhidi ya Chelsea.

Kiungo huyo wa United, Pogba alifunga bao na kutengeneza moja na alitajwa kuwa nyota wa mchezo huo uliopigwa Jumatatu usiku na kuwafurumusha Chelsea kwa mabao 2-0.

Pogba alimtengenezea pande zuri Herrera aliyefunga bao la kwanza katika dakika ya 31 kabla ya mshindi huyo wa Kombe la Dunia kufunga la pili kwa kichwa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, ambaye alitolewa nje kwa kadi nyekundu kwenye mchezo wa kwanza wa Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya mtoano wa timu 16-Bora dhidi ya Paris Saint-Germain, amehusika katika mabao 15 tangu Solskjaer kuchukua nafasi ya Jose Mourinho aliyetimuliwa Desemba mwaka jana na amefunga jumla ya mabao tisa na kutoa pasi za mwisho sita.

"Alikuwa na mchezo mgumu dhidi ya PSG, lakini pengine alikuwa mchezaji wetu bora," alisema Solskjaer akiwaambia waandishi wa habari. "Mara zote alikuwa amezungukwa na wachezaji wawili au watatu.

"Usiku wa Jumatatu aliwajibu vizuri, akicheza dhidi ya safu imara zaidi ya viungo duniani (akiwamo N'Golo Kante), lakini alionyesha kiwango cha juu.

"Tunajua kwamba ni mmoja wa viungo washambuliaji bora duniani. Ana kipaji na alitengeneza pasi nzuri kwa Ander na akafunga bao zuri.

"Halafu kwa namna alivyocheza mpira na Marcus (Rashford) ilivutia zaidi na kuonyesha uwezo wake."



## HABARI MICHEZO



# KLOPP

## AFUNGUKA LIVER KUMSAJILI SANCHO

**LIVERPOOL, England**

KOCHA Jurgen Klopp amethibitisha kwamba, Liverpool walikuwa na mpango wa kutaka kumsajili nyota wa Borussia Dortmund, Jadon Sancho wakati akiwa pale Manchester City, lakini mabingwa hao wa Ligi Kuu ya England hangeweza kuwauzia mchezaji huyo.

Sancho aliondoka City kwenda Bundesliga Agosti mwaka 2017 na amekuwa na kiwango kizuri Ujerumani, akifunga mabao saba na kutengeneza mengine tisa kwenye mechi 22 za ligi msimu huu. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 18, alipata nafasi ya kuitwa kwenye timu ya wakubwa ya England mwishoni mwa mwaka jana na anaonekana atakuwa na nafasi ya kuichezea zaidi kutokana na kipaji alichokionyesha.

"Kuwanunua wachezaji wa Kiingereza ni wazo zuri, lakini hatungeweza kupata nafasi ya kumnunua Sancho," alisema Klopp akiwaambia waandishi wa habari kabla ya mchezo wake wa jana Jumanne wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich.

"Sisi si vipofu. Tulimuona yeye (Sancho), tulimpenda na baadaye tukafikiria tunaweza kweli kumpata?"

"Hapana, kwa sababu klabu za Uingereza haziuziani wachezaji. Na sijui kwa sababu gani, lakini hawafanyi hivyo."

# GRIEZMANN:

## Hamasa ni kubwa kwetu Ulaya

**MADRID, Hispania**

ANTOINE Griezmann amebainisha kwamba kucheza fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu huu katika uwanja wao wa nyumbani wa Wanda Metropolitano kumewapa wachezaji wa Atletico Madrid hamasa ya ziada.

Atletico imefika robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya katika misimu mitano iliyopita na leo Jumatano wanacheza na miamba wa Italia, Juventus kwenye mchezo wa kwanza wa hatua ya mtoano wa timu 16-Bora.

Na Griezmann anaamini kwa uwanja wao kupata nafasi ya kuchezewa fainali ya michuano hiyo ya msimu huu, anaamini hiyo imekuwa hamasa kubwa zaidi kwa kikosi hicho kinachonolewa na kocha Diego Simeone.

"Imetupa sisi hamasa kubwa zaidi," alisema akiiambia UEFA.com.

"Mara zote kuna kuwa na hali ya hewa nzuri na hicho ndicho tunachokihitaji kama wachezaji.

"Fainali kuchezwa kwenye uwanja wetu wa nyumbani ni hamasa kubwa zaidi kwa wachezaji wote wa Atletico.

"Mchezo dhidi ya Juve utakuwa mgumu kwetu, lakini tumejindaa vizuri na tutajaribu kucheza katika ubora wetu, na halafu tutaona."

# Sarri sasa awajibu mashabiki Chelsea

**LONDON, England**

KOCHA wa Chelsea, Maurizio Sarri, amesema timu yake ilicheza mchezo wa 'Kugawanyika' baada ya Man United kupata ushindi katika Uwanja wa Stamford Bridge na kufanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Kombe la FA.

Matokeo hayo yanamweka Muitaliano huyo katika hali mbaya ya kuwa na uwezekano wa kutimuliwa.

Ander Herrera alifunga krosi iliyopigwa na Paul Pogba na kufanikiwa kuipatia United uongozi kunako dakika ya 31, kabla ya Pogba kufunga bao la pili kwa kichwa na kuipatia timu yake fursa nzuri baada ya krosi iliyochongwa na Marcus Rushford.

Huku Chelsea wakishindwa kwa mara nyingine, mashabiki wao walimshutumu kocha wao Sarri.

Lakini Sarri amesema; "Tulicheza kana kwamba tumechanganyikiwa katika kipindi cha pili, lakini katika kipindi cha kwanza tulionyesha mchezo mzuri. "Nina wasiwasi kuhusu matokeo haya, lakini si kuhusu mashabiki kwa sababu naelewa hali yao. Ninawaelewa mashabiki wetu kwa sababu matokeo hayo si mazuri na tumetolewa katika Kombe la FA.

"Nilikuwa na wasiwasi mkubwa zaidi nilipokuwa kocha katika Ligi ya Daraja la Pili nchini Italia, lakini si sasa."



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# BANEGA KUMRITHI RAMSEY ARSENAL

**LONDON, England**

Arsenal imerudia mpango wake wa kumsajili kiungo wa kati wa Sevilla, Ever Banega baada ya kushindwa kufanikisha dili hilo majira ya joto, imeelezwa.

Gazeti la 'The Mirror', limeeleza kuwa Kocha wa 'Gunners', Unai Emery ni shabiki mkubwa wa kiungo huyo na amefanya kazi na Banega mara mbili wakati akiinoa Sevilla na Valencia na ni chaguo lake la kwanza katika mtu sahihi wa kumrithi Aaron Ramsey kwenye idara ya kiungo Arsenal.

Arsenal haikufanya usajili dirisha la Januari kwa sababu ya kukosekana kwa fungu, lakini itatazama tena uwezekano wa kwenda sokoni majira haya ya joto kwa mara nyingine ikiwa na upungufu wa fedha katika kukamilisha dili za maana.

Banega anaweza kuigharimu takriban pauni milioni 17 kwa Arsenal kulipa kiasi hicho kinachotakiwa ili kuvunja mkataba wake, lakini shida kubwa itakuwa umri wake kwani Juni atakuwa na miaka 31.

Arsenal inahitaji beki mpya wa kushoto, kiungo pamoja na winga mshambuliaji ili kuimarisha kikosi chake, ingawa inatumai kuwa mcheza kwa mkopo Denis Suarez atathibitisha kwa kuonyesha uwezo na kujiunga na Gunners moja kwa moja kwa pauni milioni 18 zinazohitajika kutoka Barcelona.

Tayari Ramsey amesaini mkataba wa awali wa makubaliano ya kujiunga rasmi na Juventus mwishoni mwa msimu, hivyo Arsenal italazimika kwenda sokoni kutafuta mbadala wa mchezaji huyo majira ya joto.

Nyota huyo wa kimataifa wa Wales, atahitimisha ushirikiano wake wa muda mrefu na Arsenal baada ya kukubaliana malipo binafsi ya mkataba wake wa miaka minne ambao umeripotiwa kuwa utamfanya awe analipwa pauni 400,000 kwa wiki.

Kiungo Mjerumani Mesut Ozil, kuna uwezekano mkubwa wa kuachana na klabu hiyo ya kaskazini mwa London kutokana na kuonekana kutokuwa katika mipango ya Unai Emery hapo Emirates.

Alhamisi Ozil aliachwa katika kikosi cha Arsenal kilichoifuata FC BATE Borisov ya Belarus na kulala kwa bao 1-0 kwenye mechi hiyo ya awali ya hatua ya mtoano.

Ozil ambaye hata katika mechi za Ligi Kuu hapewi nafasi kikosi cha kwanza mara kwa mara, baada ya kutojumuishwa katika kikosi hicho, aliamua kukwea pipa na kwenda kupumzika Uturuki.

Hata hivyo, Kocha wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, ameeleza kuwa kiungo huyo wa zamani wa Ujerumani, Ozil, anaweza kuwa katika "ukanda wa kusumbuana" na klabu hiyo kutokana na kusaini mkataba mnono na 'Gunners' mwaka jana.

## KWA UFUPI

**LIVERPOOL KUMRUDIA SANCHO**
Liverpool inaweza kurudi tena kujaribu kumsajili winga wa Borussia Dortmund na England, Jadon Sancho, 18, baada ya kushindwa kufanikisha mchakato huo wakati akiwa Manchester City. ***(Mirror)***

**ZIYECH AWINDWA CHELSEA**
Chelsea inamtupia jicho nyota wa Ajax, Mmorocco Hakim Ziyech, ambaye hadi sasa ameshatupia mabao 15 na kutoa pasi za mwisho 13 katika mashindano yote akiwa na Ajax msimu huu. ***(Calciomercato).***

**JOVIC AVUTA VIGOGO ULAYA**
Barcelona inapewa nafasi zaidi ya kumsajili straika wa Benfica, Luka Jovic, 21, ambaye anacheza kwa mkopo Eintracht Frankfurt. Real Madrid, Chelsea na Bayern Munich pia zinavutiwa kumsajili Mserbia huyo. ***(Goal)***

**MILITAO MTEGONI MADRID**
Real Madrid inaongoza mbio za kumsajili beki wa Porto, Eder Militao, 21, na itamsajili nyota huyo wa kimataifa wa Brazil kwa takriban pauni milioni 44. ***(Marca)***

**WENGER AMFUNGUKIA OZIL**
KOCHA wa zamani wa Arsenal, Arsene Wenger, ameeleza kuwa kiungo wa zamani wa Ujerumani Mesut Ozil, 30, anaweza kuwa katika "ukanda wa mtifuano" kutokana na kusaini mkataba mnono na 'Gunners' mwaka jana. ***(Mail)***

**ICARDI AULIZIWA JUVENTUS**
Juventus imeiuliza Inter Milan kuhusu mustakabali wa baadaye wa Mauro Icardi, 25, lakini haijafanya mazungumzo na straika huyo wa kimataifa wa Argentina, ama na wakala wake. ***(Radio Rai via Four Four Two)***

**MRUNDI WA STOKE KUUZWA**
PINDI dirisha la usajili la majira ya kiangazi litakapofunguliwa Stoke itajaribu kumuuza straika Mburundi Saido Berahino, 25, haraka iwezekanavyo. ***(Mail)***

**WOLVES YAKARIBIA KWA SAISS**
Wolves inakaribia kukubaliana mkataba mpya na kiungo Mmorocco, Romain Saiss, 28. ***(Telegraph)***


**PJANIC NUSURA ATUE UNITED**
KIUNGO wa Juventus na Bosnia, Miralem Pjanic, 28, angeweza kujiunga na Manchester United majira ya joto yaliyopita kabla ya kuamua kubaki Italia na mabingwa hao wa Serie A. ***(Il Gironale, via Star)***

**BARCA, VITAO KIMEELEWEKA**
MIAMBA ya Hispania, Barcelona ipo katika hatua za mwisho za kumsajili beki wa kati Mbrazil Vitao, 19, kutoka Palmeiras. ***(Marca)***

**DIAME KUJIFUNGA NEWCASTLE**
KIUNGO wa Newcastle, Msenegal Mo Diame, 31, anakaribia kukubali kuongeza mkataba mpya hapo St James' Park. ***(Chronicle)***

**SAMUELSEN KUITEMA WEST HAM**
KIUNGO wa West Ham na Norway, Martin Samuelsen, 21, ambaye anacheza kwa mkopo VVV Venlo, anataka kurudi nyumbani kwao kuichezea FK Haugesund. ***(Inside Futbol)***

**HARPER, WEST BROM KUJIFUNGA**
KIUNGO wa West Brom na England U-19, Rekeem Harper, 18 "amepiga hatua moja mbele na kukaribia" kusaini mkataba mpya. ***(Express and Star)***



## HABARI MICHEZO

# NGASSA AIONYA MBAO FC

**Na Faustine Feliciane**

KIUNGO wa Yanga, Mrisho Ngassa, amesema baada ya Jumamosi kupoteza mchezo wao wa Ligi Kuu dhidi ya Simba, hasira zao watazimalizia kwa Mbao FC watakapokutana leo kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Ngassa ambaye katika mechi hiyo ya Jumamosi aliingia akitokea benchi kuchukua nafasi ya Ibrahim Ajibu, aliliambia Nipashe jana kuwa Mbao wasitarajie mteremko kwao na wamejipanga kuwafuta machozi mashabiki wao kufuatia kupoteza mchezo huo dhidi ya watani wao wa jadi.

"Hautokuwa mchezo mwepesi, lakini Mbao wasitarajie sisi kupoteza mchezo uliopita kutawapa wao nafasi ya kupata ushindi, tumejipanga kuhakikisha tunapata pointi tatu," alisema Ngassa.

Aidha, alisema licha ya matokeo ya mchezo uliopita bado wana hamasa na morali ya kuhakikisha wanafanya vizuri kwenye michezo iliyobakia.

"Matokeo ya mchezo uliopita yamepita na tumeyaweka pembeni, kwa sasa tumeelekeza nguvu zetu kwenye michezo ya mbele, tunaanza na kesho (leo) dhidi ya Mbao," aliongeza kusema Ngassa.

Yanga iliyopo kileleni mwa ligi hiyo ikiwa na pointi 58 baada ya kushuka dimbani mara 24, imekuwa na wakati mgumu inapocheza na Mbao kwenye Uwanja wa CCM Kirumba ambapo katika michezo mitatu ya karibuni iliambulia vipigo.

Mchezo wa leo ni muhimu kwa Yanga kujaribu kuwafuta machozi mashabiki wake kufuatia kipigo cha bao 1-0 walichokipata Jumamosi iliyopita kutoka kwa Simba

**16-BORA LEO...**



Kushoto mbele ni Raheem Sterling na Kevin De Bruyne, wakiwa na wenzao mazoezini jana, kujianda na mechi ya hatua ya 16-Bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Schalke 04 leo. **PICHA: DAILY MAIL**

# Kambi riadha sasa kuanza leo

**Na Renatha Msungu**

KAMBI rasmi ya wanariadha wanaounda timu ya Taifa ya Riadha, inatarajiwa kuanza kesho badala ya leo kama ilivyopangwa awali kabla ya mabadiliko hayo.

Hayo yamesemwa na Katibu wa Shirikisho la Riadha nchini (RT), Wilhelma Gidabuday, wakati akizungumza na gazeti hili jana.

Alisema jumla ya wanariadha 28 wamechaguliwa kuunda timu hiyo ya taifa itakayoshiriki mashindano ya dunia ya Mbio za Nyika yanayotarajiwa kufanyika nchini Denmark mwishoni mwa mwezi ujao.

Gidabuday alisema timu hiyo itakuwa chini ya jopo la makocha saba, na imechaguliwa baada ya mashindno ya wazi ya Taifa ya Mbio za Nyika yaliyofanyika juzi mjini Moshi chini ya udhamini wa DStv pamoja na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro.

Alifafanua kuwa timu hiyo inajumuisha idadi hiyo ya wachezaji ambao wako katika makundi manne ya umri na umbali tofauti tofauti kwa jinsia zote.

Wanariadha watakaounda timu ya wanaume wenye umri wa zaidi ya miaka 18 ni Faraja Damas, Joseph Panga, Sylvester Marco na Stephano Huche (Arusha), Deogratius Nade (Manyara), Yohane Elisante (Arusha) na Bazil Sule (Polisi).

Kwa upande wa wanawake katika kundi hilo la wakubwa waliopo ni Failuna Abdi (Arusha), Magdalena Shauri (JKT), Anjelina Daniel, Amina Mohamed, Marselina Issa na Neema Msuad (Arusha).

Alilitaja kundi la wavulana chini ya miaka 18 kuwa litakuwa na wachezaji saba, ambao ni Michael Kishimba (Arusha), Daniel Sinda (Arusha) Emmanuel Joseph (Manyara), Francis Damiano (Mbulu), Saimon Francis (Arusha) na Nicodemo Joseph (Mbulu) wakati wasichana watakuwa ni Agnes Protus (Arusha), Anastazia Ndoromongo (Arusha), Aisha Luguna (Arusha), Sara Hiti (JKT), Gace Jackson (JKT), Noela Lemmy (Arusha) na Catherine Philipo (Manyara).

Kambi hiyo itakuwa chini ya jopo la wataalamu nane wakiongozwa na Kocha Mkuu Meta Petro kutoka Klabu ya Riadha ya Rift Valley, wengine ni Anthony Mwingereza (JWTZ), Andrea Panga (JKT), Thomas Tlanka (Arusha) na Juma Jambau (Singida) wakati mwanariadha wa zamani Marcelina Gwandu ameteuliwa kuwa matron wa kambi hiyo, huku Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Dk. Hamad Ndee akipewa jukumu la kuratibu mafunzo hayo.

# Ninje: Serengeti Boys ipo vizuri

**Na Faustine Feliciane**

WAKATI ikiwa imebaki miezi miwili kabla ya kuanza kwa fainali za Afrika kwa vijana wenye umri chini ya miaka 17, Mkurugenzi wa Ufundi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Ammy Ninje, amesema kikosi cha Tanzania kitakachoshiriki michuano hiyo 'Serengeti Boys' kinaendelea na maandalizi vizuri.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Ninje alisema kikosi cha timu hiyo ambacho kimeweka kambi mkoani Arusha, kipo kwenye maandalizi kabambe huku kila kitu kikienda sawa na kuwataka Watanzania na vyombo vya habari kukisapoti.

Alisema kikosi hicho kinatarajia kundoka nchini Machi Mosi, mwaka huu kuelekea Uturuki kwa ajili ya kushiriki michuano maalum iliyoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Ulaya, Uefa.

**"Tunategemea michuano hii ya Uturuki itaipa msaada mkubwa timu yetu kuelekea kwenye mashindano ya Afrika yatakayofanyika hapa nyumbani, kule Uturuki watakutana na timu za Ulaya na baadhi kutoka Afrika," alisema Ninje.**

Alisema vyombo vya habari viendelee kutoa hamasa kwa timu hiyo na wananchi wanapaswa kuiunga mkono.

"Baada ya michuano hiyo ya Uturuki timu itarejea nchini kwa ajili ya maandalizi ya mwisho kuelekea kwenye michuano ya Afrika ambayo Tanzania tutakuwa wenyeji," alisema.

Michuano hiyo ya Afrika imepangwa kufanyika Aprili mwaka huu ambapo itachezwa kwenye viwanja vya Taifa na Chamazi huku Serengeti Boys ikiwa Kundi A sambamba na timu za Uganda, Nigeria na Angola.



Michezo

Jumatano Februari 20, 2019

Nipashe



Banega kumrithi Ramsey Arsenal

HABARI UK. 30

BAO HILO...



Paul Pogba akiruka na kufunga bao kwa kichwa katikati ya mabeki wa Chelsea, Antonio Rudiger na Cesar Azpilicueta kwenye mechi ya Kombe la FA iliyopigwa Uwanja wa Stamford Bridge juzi na Manchester United kushinda 2-0. Kwa matokeo hayo United sasa itakutana na Wolves katika hatua ya robo fainali. **PICHA: MTANDAO**

# Simba yazidi kunoga

## ●●● Bila Okwi, Kagere na Chama, kikosi kipana chaonekana wakiifyatua African Lyon vitatu huku...

**Na Mwandishi Wetu**

UPANA wa kikosi cha Simba umeonekana wakati timu hiyo ikizidi kunoga baada ya kuifyatua African Lyon kwa mabao 3-0 katika mechi ya Ligi Kuu Bara, iliyopigwa Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha jana.

**Mabingwa hao watetezi wa Ligi Kuu Bara, jana waliwakosa washambuliaji wake watatu hatari wa kikosi cha kwanza, Emmanuel Okwi, Meddie Kagere na Clatous Chama, lakini bado wakaweza kuonyesha ubora dhidi ya wenyeji wao, African Lyon.**

Mabao ya vijana hao wa kocha Patrick Aussems, yalifungwa na nahodha John Bocco aliyetupia mawili pamoja na Adam Salamba aliyefunga moja.

Kwa matokeo hayo, Simba sasa imecheza mechi tatu mfululizo bila kuruhusu bao ['clean sheet'] kufuatia kuifunga Al Ahly bao 1-0 kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, iliyopigwa Uwanja wa Taifa kabla ya kuibuka na ushindi kama huo dhidi ya watani wao wa jadi, Yanga, katika mchezo wa Ligi Kuu Bara.

Katika mechi hiyo ya jana, Simba ilicheza pasi ndefu ndefu kutokana na uwanja kutokuwa rafiki kwa pasi fupi, na iliwachukua dakika 27 kupata bao lililofungwa na Bocco kwa mkwaju wa penalti iliyotokana na beki wa Lyon, Roland Msonjo kuunawa mpira eneo la hatari.

Kabla ya kuingia bao hilo, Simba ilipata bao dakika ya sita tu ya mchezo hata hivyo, lilikataliwa na mwamuzi wa mchezo huo baada ya mwamuzi msaidizi kuashiria mfungaji alikuwa ameotea.

Ikiwa imebaki dakika moja kabla ya mapumziko, Salamba aliipatia Simba bao la pili akimalizia mpira uliotemwa na golikipa wa Lyon, Deo Kisejo kufuatia shuti la Bocco. Mpaka timu hizo zinakwenda mapumziko Simba walikuwa mbele kwa mabao 2-0.

Kipindi cha pili kilianza kwa kasi na dakika moja tu tangu kuanza kwa mchezo, Bocco aliipatia Simba bao la tatu kwa shuti akiunganisha krosi ya Rashid Juma kutoka upande wa kushoto wa uwanja.

Kocha Aussems alifanya mabadiliko kipindi cha pili kwa kuwatoa Juma na Pascal Wawa na nafasi zao kuchukuliwa na Jonas Mkude na Yusuph Mlipili.

Kwa ushindi huo wa jana unaifanya Simba kufikisha pointi 42 kutokana na michezo 17 waliyocheza wakiwa nyuma kwa pointi 16 dhidi ya vinara Yanga ambao wamecheza michezo 24 na leo wanacheza mechi ya 25 dhidi ya Mbao FC kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Baada ya mchezo wa jana, Simba itarejea jijini Dar es Salaam na kushuka dimbani tena Jumamosi kuumana na Azam FC iliyopo nafasi ya pili kufuatia kujikusanyia pointi 50 baada ya mechi 24.

Baada ya mechi hiyo itaifuata Lipuli FC ya Iringa na kisha kurejea Dar es Salaam kujianda kwa safari ya Algeria kwenda kuivaa JS Saoura Machi 9, kwenye mechi ya Kundi D ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Kwingineko katika Uwanja wa Mkwakwani jijini Tanga, Azam FC ililazimishwa sare ya bao 1-1 na wenyeji Coastal Union.

# Zahera: Mwisho wa Mbao ni leo

**Na Faustine Felician**

KOCHA wa vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, Mwinyi zahera, amesema mashabiki na wadau wa soka wanatakiwa kujua kuwa historia haichezi mpira na kwamba leo watavunja uteja wa kufungwa na Mbao kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza.

Katika mechi hiyo ya Ligi Kuu, Mbao leo watakuwa wenyeji wa Yanga ambayo haijawahi kupata ushindi wowote kwenye michezo mitatu waliyokutana na timu hiyo katika uwanja huo.

Yanga inaingia kwenye mchezo huo ikitoka kupokea kipigo cha bao 1-0 kutoka kwa watani zao wa jadi, Simba kwenye mchezo uliochezwa Jumamosi iliyopita Uwanja wa Taifa.

Akizungumza na gazeti hili mara baada ya mazoezi ya timu hiyo jana, Zahera alisema mchezo huo ni muhimu sana kwao na anajivunia morali ya wachezaji wake licha ya kufungwa kwenye mechi iliyopita.

Zahera, alisema hana shaka na kikosi chake na leo watapambana kurejesha hamasa ya timu hiyo kwenye michezo yake ijayo.

"Nafahamu Yanga imekuwa ikipata matokeo mabaya kwenye mechi za hivi karibuni dhidi ya Mbao kwenye uwanja huu, lakini historia haichezi mpira, tumekuja tumejipanga kwa ajili ya ushindi, kwa morali tuliyonayo tutapambana kuhakikisha tunaibuka na ushindi," alisema Zahera.

Alisema baada ya mchezo dhidi ya Simba aliwataka wachezaji wake kusahau matokeo waliyoyapata na kujiandaa kwa mchezo huo wa leo.

Kwa upande wake kocha wa Mbao FC, Ally Bushiri, alisema mchezo huo ni mgumu na watacheza kwa tahadhari kubwa ili kupata matokeo mazuri.

"Hautakuwa mchezo mwepesi, tunaiheshimu Yanga na tunajua wametoka kupoteza mchezo wao uliopita, hivyo watakuwa na kila sababu ya kutaka kupata matokeo mazuri, lakini na sisi tumejipanga kukabiliana nao," alisema Bushiri.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >